# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## Kikao cha Tano – Tarehe 8 Aprili, 2019

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwa mwaka ulioisha tarehe 30 Juni, 2018 *(The Annual Report of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority for the year ended 30th June, 2018).*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza maswali na Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, sasa aulize swali lake.

Na.33

## Kujenga Zahanati kwa kila Kijiji na Kituo cha Afya kwa kila Kata

**MHE.DKT. DALALY P. KAFUMU** aliuliza:-

Katika Ilani ya CCM kuhusu huduma za afya nchini ni kujenga zahanati katika vijiji na kituo cha afya katika kila kata; kwa sasa Jimbo la Igunga lina vituo vya afya viwili tu katika kata 2 kati ya 17 na zahanati kwenye vijiji 19 tu kati ya vijiji 68:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga vituo vya afya kwenye kata 15 zilizosalia?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga zahanati kwenye vijiji 49 vilivyosalia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri (TAMISEMI), majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa NaibuSpika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 kwa ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya kote nchini kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo. Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ilipokea shilingi milioni 800 kwa mwaka wa fedha 2018 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya vya Igurubi na Simbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kituo cha Afya cha Simbo ambacho ujenzi wake upo asilimia 97, fedha hizo zilitumika kumalizia majengo mawili ambayo ni jengo la upasuaji, nyumba ya mtumishi pamoja na ujenzi wa majengo mapya manne ambayo ni maabara, jengo la uzazi, jengo la kufulia na jengo kuhifadhi maiti. Aidha, kituo hicho kimeanza kupokea vifaa tiba kutoka Bohari Kuu ya Dawa (*MSD*). Kwa upande wa Kituo cha Afya Igurubi, ujenzi unaendelea na umefikia asilimia 70. Jumla ya majengo manne mapya yamejengwa ambayo ni maabara, jengo la uzazi, jengo la kufulia na jengo la kuhifadhi maiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutekeleza ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya kwa awamu katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pia naishukuru Serikali kwa kutuletea fedha kwa ajili ya kujenga vituo vya afya viwili. Pamoja na majibu hayo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaelekeza kwamba tujenge zahanati kila kijiji na Wilaya ya Igunga na Jimbo la Igunga mahsusi kuna vijiji ambavyo zahanati zimejengwa zikakamilika zaidi ya vijiji 10 kikiwepo Kijiji cha Kagongwa, Mgongolo, Makomelo, Chagana, Imalanguzu, Mwamakona na vijiji vingine. Ni lini Serikali itakwenda kukamilisha yale yaliyobaki pia kuleta watumishi ili zahanati hizo ziweze kuanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Wilaya ya Igunga pamoja na Jimbo la Igunga na nchi nzima kwa ujumla wananchi walijenga maboma mengi sana ya zahanati ili kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini

mpaka sasa hivi maboma hayo yapo tu na tumeomba sana tangu mwaka juzi Serikali itusaidie maboma haya yakamilike ili zahanati zianze kutumika kwa wananchi wetu katika vijiji vyetu. Je, ni lini Serikali itakamilisha maboma hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Dkt. Kafumu ameshatoa taarifa hii katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI na ukilinganisha Igunga na maeneo mengine pia kuna maboma na zahanati nyingi ambazo zimekwishafanyiwa kazi. Tumeshaomba kibali kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi (Utumishi) ili tupate kibali cha kupata watumishi na wataalamu wa tiba katika maeneo haya ili waweze kutoa huduma. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvumilia, tukipata kibali hicho na kadri fedha zitakavyopatikana basi tutaajiri na kuhakikisha kwamba vituo vyote vinafanya kazi kama ambavyo nguvu za wananchi zimetumika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kweli kwa taarifa tuliyonayo maboma ambayo yamekamilishwa nchini ni mengi kama ambavyo Jimbo la Igunga na Tabora kwa ujumla wamefanya. Hili nalo tunaomba tuahidi kwamba huu ni mwaka wa fedha, tumetenga fedha kwa bajeti ya mwaka 2019/2020 ili tumalizie maboma haya. Tunaomba wananchi waendelee kuisaidia Serikali kujenga maboma, tujitahidi kukamilisha ili huduma iweze kupatikana. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaita maswali ya nyongeza niwakumbushe uende kwenye swali moja kwa moja kwa sababu muda wetu hautoshi, ukianza kwa kuchangia kwa kirefu itabidi tu nikukalishe chini. Mheshimiwa Qulwi Qambalo swali la nyongeza.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ni sera ya Serikali kuwa na hospitali katika kila wilaya. Wilaya ya Karatu haina Hospitali ya Wilaya na hivi karibuni Halmashauri imetenga eneo la kutosha kwa ajili ya kujenga hospitali hiyo na wananchi kwa kutumia mapato yao ya ndani pamoja na wadau mfano Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro wameanza kujenga…

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali lako Mheshimiwa Qulwi.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa iko tayari kutoa fedha ili kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni kweli kwamba sasa hivi Serikali ipo kwenye hatua ya kujenga Hospitali za Wilaya mbalimbali nchini na hatua ya kwanza tulianza na hospitali 67 na awamu ya pili inaendelea. Tunawapongeza wananchi wa Karatu kwa kuendelea kuchangia huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tukamilishe kwanza hizi zilizopo baada ya hapo tutachangia na kumalizia Hospitali ya Mheshimiwa wa Karatu pia na maeneo mengine nchini. Hatua ya kwanza majengo yamekamilika tunapeleka vifaa tiba na kuna hatua ya pili ya wataalam mbalimbali. Tukianza kutoa huduma katika vituo hivyo nafikiri tutaenda na eneo letu la Karatu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tunashukuru Serikali kwa kujenga Kituo cha Afya cha Kaloleni katika Jiji la Arusha pamoja na kutujengea jengo la mionzi lakini kituo hiki hakina mashine ya *X-ray*. Je, ni lini

Serikali itatuletea mashine ya *X-ray* katika Kituo cha Afya cha Kaloleni katika Jiji la Arusha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Serikali iko katika maandalizi ya mpango wa kufanya uboreshaji wa huduma za mionzi nchini na tumeanza kwanza katika Hospitali za Rufaa za Kanda, Mikoa na baadhi ya Wilaya. Tutakapomaliza hapo tutakuja sasa kuangalia vituo vya afya ambavyo vina uwezo kuweza kupata hizo huduma na wataalamu ambao wanaweza kutoa hizo huduma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Mufindi, swali la nyongeza.

**MHE. MENDRARD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kuna Vituo vya Afya vya Mtwango, Nunga na Iramba tushaezeka na kila kitu tayari. Je, Serikali itamalizia lini yale majengo ili wananchi waanze kuvitumia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Mufindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mufindi kuna kituo cha afya kimekamilishwa na wananchi lakini vituo vingi vya afya vimejengwa nchini kama nilivyosema katika jibu langu la msingi. Tunawapongeza wananchi kwa kushirikiana na

Serikali kuiunga mkono katika hatua hii muhimu ya kuboresha huduma za afya. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutawasiliana tuone wamefikia hatua gani kwa kushirikiana na Halmashauri na kama kuna mpango wao basi tuone namna ya kumaliza kituo hiki ili kuunga mkono nguvu za wananchi ili zisipotee bure.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Ryorya, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Alhaj Abdallah Bulembo.

Na. 34

**Daraja Linalounganisha Tarafa ya Luoimbo, Suba na Nyancha**

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO (K.n.y. MHE. LAMECK O. AIRO)** aliuliza:-

Wakati wa ziara ya Kampeni za Uchaguzi Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga daraja la kuunganisha Tarafa tatu za Luoimbo, Suba na Nyancha na tayari Halmashauri imeshapeleka makadirio Wizarani:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja linalounganisha Tarafa za Luoimbo, Suba na Nyancha ni miongoni mwa ahadi

za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizozitoa maeneo mbalimbali nchini wakati wa Kampeni ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* umefanya tathmini ya gharama za ujenzi huo na wamepata kiasi cha shilingi bilioni 1.15. Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hilo. Azma ya Serikali ni kuhakikisha ahadi hiyo pamoja na ahadi nyingine zilizotolewa na viongozi wakuu wa kitaifa zinatekelezwa ndani ya kipindi cha miaka mitao ijayo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alhaj Abdallah Bulembo, swali la nyongeza.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swali la kwanza, Tarafa za Luoimbo, Suba na Nyancha ni tarafa zinazounganika, watu wanapita sehemu hiyo na Mheshimiwa Rais alitoa ahadi na muda wa ahadi za Rais kweli zitatekelezwa zote, je, imo ndani ya bajeti inayokuja kwamba inaanza kutengenezwa hata kama haitaisha kwa mwaka huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni lini wananchi wa Rorya wataweza kuwa na matumaini kwamba Serikali yao inawakumbuka katika kilio chao hiki cha mafuriko ya kila mwaka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Bulembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwamba ipo kwenye bajeti ya mwaka huu, naomba anipe muda tupitie bajeti ya mwaka huu tutaangalia kama ipo. Cha muhimu ni kwamba mimi nilienda Rorya, nimefanya ziara ya kikazi, ni miongoni mwa wilaya za mwanzo kabisa nimezitembelea. Nimeenda

Luoimbo, Suba na hii ni wilaya moja ilikuwa Tarime na Rorya imegawanywa hivi karibuni na imekuja na changamoto. Naomba wananchi wa Rorya, Mara na Watanzania wote waendelee kuiamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ahadi hizi zote zitatekelezwa kabla ya uchaguzi wa mwaka wa fedha ujao. Tathmini imeshafanyika, tunahitaji shilingi bilioni 1.15 ya kukamilisha kazi hii. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kazi kubwa inayofanywa na *TARURA* inapunguzwa faida au kufifishwa faida yake kutokana na ukosefu wa fedha za kujenga madaraja muhimu. Wananchi wa Korogwe wamekuwa wakipata shida ya muda mrefu ya Madaraja yao ya Mbagai, Makondeko na Mswaha. Serikali haioni kwamba iko haja ya kuweka jicho maalum kwenye bajeti inayokuja kwa ajili ya madaraja kwenye barabara ambazo zinatengenezwa na *TARURA?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Korogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge, ni Mbunge mpya lakini anafanya kazi kubwa sana ya kutetea wananchi wake wa Korogwe. Jambo la pili ni kwamba huu mpango mkakati ni wa kudumu na ndiyo maana imeanzishwa *TARURA* ili wataalam wetu hawa wakilala, wakiamka wafikirie barabara zetu za vijijini na mijini. Kwa hiyo, naomba tu aamini kwamba kazi hii inaendelea kufanyika vizuri na huu ni mwaka wa bajeti na bajeti ya barabara hizi inabidi ianzie katika vikao vyao vya ndani kuanzia kwenye mtaa, kijiji, halmashauri yao na hatimaye hapa Bungeni. Sisi kama Serikali tupo tayari kushirikiana na

wananchi wa Korogwe na Mheshimiwa Mbunge wao ili kuhakikisha kazi hii inafanyika vizuri na kuondoa kero zilizopo pale.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, sasa aulize swali lake.

Na. 35

**Barabara ya Vikindu- Vianzi hadi Sangatini**

**MHE. ZAYNABU M. VULU** aliuliza:-

Barabara ya Vikindu – Vianzi hadi Sangatini ni muhimu kwa wakazi wa Jimbo la Mkuranga na Kigamboni:-

Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Vikindu - Vianzi hadi Sangatini yenye urefu wa kilomita 18.65, inaanzia Kijiji cha Vikindu -Vianzi na Kitongoji cha Sangatini (Mkuranga) Mkoa wa Pwani na kuungana na barabara ya Kibada, Mwasonga hadi Tundisongani iliyopo Wilaya ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii kwa upande wa Wilaya ya Mkuranga inahudumiwa na Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (*TARURA)* na kwa upande wa Wilaya

ya Kigamboni inahudumiwa na Wakala wa Barabara nchini (*TANROADS)* Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, *TARURA* Wilaya ya Mkuranga wameiomba Serikali shilingi milioni 270 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 za kuifanyia matengenezo maeneo korofi kwa urefu wa kilometa 18 na kujenga boksi kalvati moja lenye midomo miwili. Aidha, *TARURA* watafanya tathmini ya ujenzi kwa kiwango cha lami kipande wanachokisimamia na itakapokamilika, Serikali itazingatia matengenezo hayo kwa kutegemea na upatikanaji wa rasilimali fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkuranga na wanaotumia barabara hiyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wanozunguka eneo hilo; na kwa kuwa kuna haja ya kuiboresha; na kwa kuwa Serikali imesema wanasubiri *TARURA* wafanye tathmini ndiyo barabara hiyo ijengwe, je, hawaoni kwamba wakati wakifanya tathmini barabara hiyo iweze kutengenezwa angalau kwa kiwango cha kokoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa barabara hii inaungana na barabara ya Kigamboni Mkoa wa Dar es Salaam ambayo iko *TANROADS.* Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya barabara hii kuipandisha hadhi na kuiweka *TANROADS* ili iweze kupata huduma ambazo zinalingana na kule inapoishia ambapo inahudumiwa na *TANROADS? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, jirani yangu Mheshimiwa Zaynabu Vulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ni kwamba barabara hii inaweza ikapata matengenezo wakati tunasubiri mpango wa fedha ujao. Naomba niwaelekeze *TARURA* wa Wilaya hii ya Mkuranga wafanye utaratibu wa kukarabati maeneo korofi. Bahati nzuri katika mwaka huu wa fedha wametenga fedha shilingi milioni 270 ili zipelekwe katika eneo hili lakini tunaomba wafanye kazi hiyo mapema ili iendelee kupitika wakati wote na wananchi wasiendelee kupata shida katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kupandishwa hadhi kwa barabara hii. Suala la kupandishwa hadhi lina taratibu zake na mwongozo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri yake wawasiliane na *TANROADS,* watafanya tathmini kama ikikidhi vigezo basi itakuwa ni vizuri ikapandishwa hadhi ili kupata huduma kubwa kidogo kulingana na mgao wa fedha ambao unatolewa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi ili nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo kubwa la barabara hiyo ambayo inatoka Vianzi kwenda Marogoro mpaka Tundisongani ni daraja lililopo pale Tundisongani. Daraja hilo imekuwa ni shida mvua zinaponyesha wananchi wa Tundisongani na Wilaya ya Mkuranga wanakosa mawasiliano kabisa, hali ambayo imefanya Wabunge wa sehemu zote mbili Mkuranga na Kigamboni wamekaa

pamoja lakini mpaka leo hakuna matunda yoyote juu ya barabara hii.

Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuboresha angalau lile daraja ili mvua zitakaponyesha wananchi wa Kigamboni na Mkuranga waweze kuwa na mawasiliano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba nimjibu Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wangu wa Mkoa wa Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ambavyo ameuliza swali hili kwa uchungu na maeneo haya yote muhimu, kule Mkuranga kuna Naibu Waziri mwenzangu na kule Kigamboni Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, naomba niwaelekeze *TARURA,* Mkoa wa Dar es Salaam walifanyie tathmini eneo hili na leo kabla ya saa saba nipate majibu nini kinaweza kufanyika ili kuondoa kero hii ya wananchi katika eneo hili. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rafael Chegeni, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba na mimi awaelekeze *TARURA* ili washughulikie barabara ya kutoka Shigara kwenda Ruangwe. Kijiji cha Ruangwe ni Kisiwa katika Wilaya ya Busega. Naomba maelekezo ya Waziri yaende kwa *TARURA* vilevile.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, maelekezo kwa *TARURA*.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niwaelekeze *TARURA* katika Wilaya ya Busega, watembelee maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge Chegeni na wapate majibu ya kero hiyo ambayo ameitaja hapa Bungeni. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Naona na Mheshimiwa Cosato Chumi anaomba utoe maelekezo *TARURA* Mafinga. Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona na kunipa nafasi. Pamoja na kazi nzuri wanayofanya *TARURA* Mkoa wa Iringa na katika Mji wa Mafinga, hali ya barabara za Mji wa Mafinga ambao ni kitovu cha shughuli za kiuchumi katika Wilaya ya Mufindi siyo ya kuridhisha, ni asilimia 24 tu ya baraba ambazo zinapitika kwa mwaka, ile tunaita *good and fair.* Je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia Mji wa Mafinga kwa macho mawili ili kuhakikisha kwamba barabara za Mji wa Mafinga zinapitika kwa uzuri kwa mwaka mzima ili kusudi *ku-speed up* ukuaji wa uchumi ambao ndiyo kitovu cha Wilaya nzima ya Mufindi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nimjibu Mheshimiwa Cosato Chimi, Mbunge wa Mafinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzo wa kuanzishwa *TARURA* ilikuwa ni kuondoa kero ambazo Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wanazungumzia. Kwa hiyo, naomba niwaelekeze *TARURA* nchi nzima, wafanye tathmini ya kero kubwa na za muda mrefu katika maeneo yao. Tunatarajia kwenye bajeti ambayo tunakwenda kuijadili, maeneo haya ambayo yanazungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maeneo ambayo yatakuwa yamezingatiwa kuondoa kero katika maeneo hayo kwa pamoja na eneo la Mafinga,

*TARURA* kufanya kazi pale na Mkoa wa Iringa, naomba wataalam wetu, Mainjinia nchi nzima wa *TARURA*, wafanye tathmini na walete kero mahsusi ambazo Wabunge wamezungumza na Viongozi mbalimbali wamewasilisha ili ziondolewe katika maeneo hayo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Nadhani hilo la mwisho linawahusu Wabunge wote hapa, kwa hiyo, Wabunge wote jamani majibu yenu yameshatoka hapa.

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 36

**Kero za Muungano**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Moja kati ya majukumu ya kuimarisha Muungano ni pamoja na kuhakikisha kuwa kero zote za Muungano zinatatuliwa; na vikao vingi vimekaa na kujadili kero hizo:-

Je, ni kero ngapi tayari zimetatuliwa na zipi ambazo hadi sasa zimeshindikana kupatiwa ufumbuzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambazo zimekwishapatiwa ufumbuzi ni 11 kati ya 15 zilizowasilishwa na kutafutiwa ufumbuzi. Changamoto nne zilizobaki zinaendelea kutafutiwa ufumbuzi na hakuna changamoto iliyoshindikana kupatiwa ufumbuzi. Dhamira ya Serikali zetu zote mbili ni kumaliza changamoto zote zinazoukabili Muungano wetu ili uendelee kuwa nguzo pekee ya kuimarisha amani, umoja na mshikamano wa nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu ambayo yalikuwa ni madogo ila hakutoa ufafanuzi, lakini nitakuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa sababu jambo lolote linalokuwa linataka lifanikiwe linakuwa na ratiba au linakuwa na mpangilio maalum. Hata hivi vikao wanavyovifanya kwa vyovyote inabidi viwe na maandalizi na maandalizi yake kuwe na ratiba.

Sasa nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri kabla ya kufanya hivi vikao vyao vya pamoja vya mashirikiano, wanajiandaa kwa ratiba ya pande zote mbili baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sababu baadhi ya Mawaziri huwa hawashiriki vikao kwa kuwa wanapotaarifiwa hivyo vikao wanakuwa nje ya nchi au wanakuwa na dharura nyingine za vikao vingine ambavyo wameshajipangia. Sasa nataka anijulishe, wanapokuwa wanakaa kufanya vikao hivyo wanakuwa wameandaa ratiba mapema baina ya SMZ na SMT ili wahakikishe kwamba viongozi wote hao wanatakiwa kushiriki? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wamesema kwamba changamoto zilikuwa 15, changamoto 11 zimepatiwa ufumbuzi zimebakia nne, sasa hizo changamoto nne ambazo anasema bado ziko katika maandalizi ya kupata ufumbuzi, ni zipi za SMT na zipi za SMZ katika hizo nne ambazo bado zimo katika changamoto zinazopatiwa ufumbuzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la pili nakupa uhuru wa kujibu kama unazo hapa, lakini kama huna utayatafuta majibu ili umpatie Mheshimiwa Mbunge kujua zipi ni upande wa SMZ na zipi ni za upande wa Tanzania Bara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumjibu Mheshimiwa Fakharia Shomar maswali yake mawili ya nyongeza. Moja kila kikao kinaandaliwa ratiba mapema sana na nimkumbushe tu kwamba tarehe 9 Februari, 2019 kulikuwa na kikao cha Kamati ya Pamoja cha SMT na SMZ kujadili changamoto zote hizi na hasa hizi nne nazo pia zimetolewa maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni kweli hizi changamoto nne kwa mujibu wa swali lake la msingi alivyokuwa ameliuliza, ningependa pia nizitaje, moja ni mgawanyo wa kodi ya misaada; lakini ya pili, ni usajili wa vyombo vya moto; ya tatu, ni hisa za SMZ katika Bodi ya Sarafu ya Afrika ya Mashariki na Benki Kuu; na ya nne ni Tume ya Pamoja ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee katika majibu mazuri sana yaliyotolewa na Naibu Waziri katika suala hili hasa la ratiba na utaratibu. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mwezi uliopita zimepitisha rasmi utaratibu mpya wa kushughulikia changamoto za Muungano na kuweka ratiba mahsusi ya vikao. Kwa hiyo, kile kikao kikubwa kabisa cha Makamu wa Rais ambacho ni cha Serikali zote Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Mawaziri la SMZ kinakutana mara moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna kikao cha Mawaziri na chenyewe kinakutana mara moja kwa mwaka, kikao cha Makatibu Wakuu wote kinakutana mara mbili kwa mwaka na kikao cha Wataalam wa Serikali zote na chenyewe kinakutana mara mbili kwa mwaka. Kwa hiyo ratiba zimetolewa na Waraka wa Serikali *(circular)* imesambazwa na kueleza Wajumbe wote wa vikao hivi na utaratibu wa kuviitisha, utaratibu wa kuleta ajenda katika vikao ili kuwepo na utaratibu unaotabirika na unaoeleweka na ambao umepitishwa katika mfumo wa Serikali kushughulikia suala hili.

Vilevile, zimeundwa Kamati za hii Kamati ya Pamoja, Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ili zile changamoto ambazo ni za kutafutiwa majawabu haraka haraka zisingoje kikao kikubwa, Mawaziri waweze kukutana haraka katika hizi Kamati zao na kuzishughulikia. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeweka utaratibu madhubuti kabisa wa kushughulikia changamoto za Muungano katika Serikali hii ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Nassir, swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwanza kabisa nipende kuzipongeza Serikali zote mbili kwa jitihada ambazo zimekuwa zikichukua katika masuala haya. Kwa kuwa jitihada hizi, wananchi wengi hawana taarifa nazo na hawana uelewa nazo, Serikali sasa haioni umuhimu wa kuanza kuweka utaratibu maalum wa kutoa taarifa hizi ili wananchi waweze kupata uelewa wa pamoja? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Khadija Nassir lakini pia nipokee ushauri wake, tufike mahali

sasa tuanze kuziweka wazi taarifa hizi japo tumekwishaanza lakini kuweka kwa mapana zaidi. Kwa hiyo, napokea ushauri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yusuph, swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Wabunge hawa wanapouliza kuhusu kero za Muungano na vipi zinatatuliwa, ni kwamba tunaporudi kwa wapiga kura wetu tunazikuta. Kwa hiyo, inaonesha kwamba kero za Muungano zinatatuliwa kwenye meza, lakini kwenye vitendo hakuna. Kwa mfano, msafirishaji wa ng'ombe kutoka Zanzibar akija akichukua ng'ombe Bara kupeleka Zanzibar analipishwa ushuru sawasawa na anayesafirisha kupeleka Kenya kwa Sh.37,500 badala ya Sh.7,500. Sasa ni ipi faidi ya Wazanzibari kuwa ndani ya Muungano? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli haikutazamiwa kwamba Mheshimiwa Mbunge atauliza ni zipi faida za kuwepo Muungano, kwa sababu hata yeye kuwepo kwake hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano. Muungano huu kwa pale tulipofikia hata haihitajiki kueleza faida zake kwa sababu zinaonekana dhahiri. Ukweli upo kwamba, zipo changamoto katika shughuli za kila siku za maingiliano na mahusiano hiyo haikataliwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko changamoto kubwa za kisera ambazo ndiyo zinashughulikiwa katika vikao vya viongozi, lakini kuna yale mambo ya kila siku kwamba Afisa Forodha pale ameamua mwenyewe kwa anavyoona afanye jambo. Tunachosema sisi kwa wananchi wa pande zote mbili ni kwamba yanapojitokeza mambo kama haya, kama hili alilosema Mheshimiwa Mbunge, yaletwe kwetu haraka kwa sababu ni masuala ya kiutendaji ambayo yanashughulikiwa haraka. Yako mambo mengi ya namna hii ambayo yametatuliwa kwa taarifa tu kwamba, kuna jambo hili sisi tunadhani haliendi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi tunasema kwamba, changamoto hizi ndogondogo zisitumike kuupa jina baya Muungano, kwa sababu wakati mwingine ndipo makosa yanapofanyika, kwamba inatokea tatizo ambalo lipo tu, ni la kiutendaji, la kibinadamu, lakini linatumika kwamba Muungano wetu haufai kwa sababu kuna kitu hiki. Muungano huu ni mpana zaidi na ni mkubwa zaidi na una maana kubwa zaidi kuliko changamoto zinazojitokeza kila siku. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa vijana wengi hasa wa kizazi hiki kipya hawaelewi vizuri umuhimu wa kuuenzi Muungano, Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu ya kutosha hasa kwa vijana wa sasa na hata wale wa zamani ili kujua umuhimu wa kuuenzi Muungano? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakasaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimdhihirishie tu kwamba Serikali inaendelea na mchakato na imeendelea kutoa elimu juu ya faida za Muungano na labda kama bado ziko changamoto ambazo elimu hii haiwafikii vijana walio wengi, nadhani ni wakati muafaka sasa wa kuendelea kuhimiza kuhakikisha kwamba elimu hii inawafikia vijana wote.

Na. 37

**Matumizi ya Mifuko ya Plastiki**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Matumizi ya mifuko ya plastiki hapa nchini yamekuwa na athari kubwa kwenye uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa miji yetu:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuondoa matumizi ya plastiki hapa nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa matumizi ya mifuko ya plastiki yameongezeka hasa kutokana na mifuko hii kutolewa bure kwenye maduka, masoko, migahawa na maeneo mbalimbali. Aidha, kutokana na baadhi ya nchi jirani kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki na kuruhusu uzalishaji kwa ajili ya soko la nje ya nchi, kumekuwa na wimbi kubwa la uingizaji wa mifuko ya plastiki nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hali hii na mwelekeo wa Jumuiya ya Kimataifa wa kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na taka za plastiki, Serikali inadhamiria kusitisha uzalishaji na matumizi ya mifuko ya plastiki katika siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, imeanza kuchukua hatua zifuatazo katika kuelekea kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki:-

(a) Kuhamasisha wajasiriamali, vikundi vya akinamama na vijana, sekta binafsi na viwanda kuwekeza katika uzalishaji wa mifuko mbadala ikiwemo vikapu vya asilia, mifuko ya karatasi na vitambaa;

(b) Ofisi imeendesha mikutano miwili ya wadau katika Mikoa ya Dar es Salaam tarehe 6 Novemba, 2018 na Mwanza tarehe 18 Novemba, 2018, kuelimisha umma kuhusu changamoto na athari za mifuko ya plastiki na kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji wa mifuko mbadala kutokana na dhamira ya Serikali kusitisha matumizi ya mifuko ya plastiki katika siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikutano hii, wadau na wananchi waliishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika uzalishaji wa mifuko mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii, kwa mara nyingine tena kuhimiza viwanda vinavyozalisha mifuko ya plastiki na wadau wengine kujitayarisha kwa kubadili teknolojia na kutathmini fursa zinazojitokeza katika kuzalisha mifuko mbadala hasa katika kipindi hiki cha mpito wakati taratibu za maamuzi ya Serikali zikikamilishwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya, swali la nyongeza.

**MHE. MAGDALENA HAMIS SAKAYA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Majibu ya Serikali yaliyotolewa hapa Bungeni leo, hayaoneshi dhamira ya dhati kupiga marufuku mifuko ya plastiki hapa nchini. Ukiangalia majibu ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, inadhamiria siku zijazo, siyo kesho wala mwakani, hatujui. Hivi tunavyoongea, kwenye masoko yetu wajasiriamali wengi wanauza mifuko mizuri, mifuko

ambayo ni rafiki kwa mazingira, mifuko ambayo ni vikapu vya ukili na mifuko mingine ambayo inaweza kutumika isiharibu mazingira. Mifuko hiyo haina masoko, hainunuliwi kwa sababu mifuko ya plastiki inatolewa bure masokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni kwamba tatizo siyo kukosekana kwa mfuko mbadala, tatizo ni Serikali kuendelea kulinda viwanda vinavyotengeneza mifuko hii inayoharibu mazingira?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, hakuna Mtanzania yeyote au mdau yeyote asiyejua madhara ya mifuko ya plastiki hapa nchini. Serikali hioni kuendelea na makongamano, sijui na vikao vya wadau ni kupoteza muda na gharama na Serikali sasa ichukue hatua za haraka kupiga marufuku mifuko hii hapa nchini kama ambavyo wenzetu wamefanya, Zanzibar wameweza, Rwanda wameweza, Kenya wameweza, maeneo mengine yote wameweza. Sisi tatizo nini? Naomba majibu ya uhakika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana sana Mheshimiwa Sakaya kwa kuongea kwa uchungu kabisa na kuonesha ni mwanamazingira kabisa fasaha. Naomba nimhakikishie kwamba, katika hotuba yetu ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, ambayo itakuja tarehe 16 kwa mujibu wa ratiba ya mwezi huu, tunaweza kutangaza hatua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu wiki hii mimi nimeelekezwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kasim Majaliwa Majaliwa, nikutane na Taasisi za Serikali zinazohusika na jambo hili, *NEMC, TBS, TRA*, Uhamiaji, Polisi na *Customs* ili kuweka utaratibu wa namna tunavyoweza kupiga marufuku. Hapa nilipo, tayari ninazo kanuni nimeshazitengeneza ambazo zinangoja kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali. Kwa hiyo, kama tutakubaliana katika vikao vya wiki hii na vinayokuja,

basi tarehe Mosi, Julai, inawezekana kabisa ikawa ndiyo mwisho wa matumizi ya plastiki hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni jambo ambalo Serikali inalichukulia kwa uzito na tunalifanyia kazi. Ni kweli kabisa tumeongea na wadau wote, hakuna sababu yoyote ya kuendelea kutumia plastiki hapa nchini. Mimi kama Waziri wa Mazingira nakubali hilo. Mbadala upo na inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tukubaliane kwamba tutakapopiga marufuku, basi tuwe tumejiandaa kufanikiwa. Kwa sababu zipo nchi ambazo zimeamua kuchukua hatua hii, lakini hazikujipanga kwenye kufanya lile zoezi; mkajikuta kwamba mmetoa tangazo tu, lakini kitaasisi hamjajipanga, kiuratibu hamjajipanga, kwa hiyo, inakuwa ni bure tu. Kwa hiyo, tunataka tukitangaza tulifanye zoezi hili kwa namna ambayo tutafanikiwa. Tunaamini kabisa kwamba hatua hii itaibua ajira nyingine nyingi zaidi kuliko hata zile zilizopo kwenye mifuko ya plastiki.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tuko pamoja kwenye hili.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ally Keissy.

Na. 38

**Mgogoro wa Shamba la Efatha – Rukwa**

**MHE. ALLY K. MOHAMED (K.n.y. MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro wa shamba la Efatha Mkoani Rukwa?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu wa matumizi ya Shamba Na. 48/1 la Malonje kati ya mmiliki ambaye ni Mdhamini wa Efatha na wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba hili, hususan Vijiji vya Songambele, Sikaungu na Msanda Muungano. Madai ya wananchi hao ni kuwa sehemu ya shamba hili imeingia ndani ya vijiji vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo awali Shamba la Malonje lilikuwa likimilikiwa na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo likiwa halina upimaji ambapo lilipimwa mwaka 1997 likiwa na ukubwa wa hekta 15,000. Mwaka 2007 shamba hili liligawanywa ambapo hekta 10,000 ziliuzwa kwa wamiliki ambao ni *Efatha Ministry* na hekta 5,000 zilizobaki zilipimwa vitalu na kugawiwa wafugaji. Mwaka 2010 baada ya kupokea malalamiko na kuyafanyia kazi, ilibainika kuwa upimaji wa vijiji uliofanyika umeingiliana na mipaka ya shamba husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na Mkoa wa Rukwa, imefanya jitihada mbalimbali za kumaliza mgogoro huo. Baada ya jitihada hizo kutozaa matunda, tarehe 7 Novemba, 2017 nilikutana na Mwenyekiti wa Bodi ya Huduma ya Efatha na baadhi ya Watendaji wake kwa lengo la kukubaliana namna bora ya kumaliza mgogoro huu ili kuboresha mahusiano ya ujirani mwema kati ya mmiliki na wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba hilo. Wizara yangu ilipendekeza kwamba Efatha iridhie kuachia sehemu ya ardhi ya shamba yenye ukubwa wa ekari 8,392.9 na kuigawa kwa wananchi wa vijiji husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bodi ya Wadhamini kukaa, waliridhia kutoa ekari 3,000 kwa Vijiji vya Songambele, Sikaungu na Msanda Muungano kwa maana ya kila kijiji kigawiwe ekari 1,000. Hata hivyo, Kijiji cha Sikaungu kimekataa kupokea ekari hizo kwa kuwa wao wanataka kiasi cha ardhi kama ilivyoonekana kwenye vyeti vyao vya ardhi ya kijiji.

Aidha, majadiliano bado yanaendelea kati ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Efatha na Serikali ya Kijiji cha Sikaungu. Baada ya majadiliano hayo kukamilika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri itasimamia upimaji wa ardhi hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsnate sana. Tangu alipouziwa hilo shamba, leo ni miaka 12, lakini mpaka leo hajaendeleza hata ekari moja, imekuwa ni shamba pori na kusababisha vijiji vilivyozunguka hilo shamba vya Sikaungu, Songambele na Msanda Muungano kukosa sehemu ya kulima. Mkoa wa Rukwa, wananchi wote wanategemea kilimo, sasa kwa nini wanasitasita wasimpelekee Mtukufu Rais kulifyekelea mbali hili shamba, kulifuta kama alivyofuta mashamba mengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Hilo shamba linamilikiwa na Halmashauri ya *Sumbawanga DC* na Manispaa. Cha ajabu, vigezo gani vilitumika, mkataba uliingia peke yake na Manispaa ya Sumbawanga kuuza hilo shamba bila Manispaa ya *Sumbawanga DC* kushirikishwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Keissy kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ufutaji mashamba halianzii kwenye Wizara ya Ardhi, suala la ufutaji mashamba kama halijaendelezwa wahusika wa kwanza ni zile mamlaka zenyewe za upangaji miji katika maeneo yao. Kwa hiyo, kama wao waliona kwamba hili shamba pengine halijakidhi vigezo, linatakiwa kufutwa, walitakiwa wao walete mapendekezo hayo kwa Waziri na Waziri angemshauri Mheshimiwa Rais kulifuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, walikuwa pia na mgogoro naye na walipelekana Mahakamani. Halmashauri yenyewe husika ikatoa shauri Mahakamani na wakakubali ku-*settle* nje ya *court.* Kwa hiyo, sisi kama Wizara hatuwezi kuingilia makubaliano yao. Kwa hiyo, kama bado wanaona hajaendeleza, basi warudi tena wao wachukue maamuzi kama waliyokuwa wamechukua mwanzoni ya kuchukua hatua. Wakileta, sisi tutashughulikia vinginevyo itakuwa kidogo ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili anaongelea kwamba shamba lile linaingia katika Halmashauri mbili; nadhani katika ziara yangu niliyofanya mwaka 2017 suala hili nililipata na nililitolea maelekezo. Nilisema kama pale ambapo unakuta shamba la mwekezaji limeingia katika Halmashauri mbili tofauti, ni jukumu la Halmashauri husika kuzungumza naye kuweza kuona ni namna gani Halmashauri zote mbili zitafaidika na mwekezaji huyo kama ameingia katika maeneo yao. Sasa sisi kama Wizara hatuwezi kuwapangia namna ya kukubaliana, kwa sababu ni mazungumzo kati ya mwenye eneo na mwenye mamlaka ya upangaji miji na yule mwekezaji aliyeko katika eneo lao. Kama itashindikana, wanahitaji ushauri kutoka Wizarani, tuko tayari kuwasaiia kwa suala hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Haule, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami niulize swali dogo la nyongeza. Kumekuwa na migogoro ya muda mrefu sana katika Jimbo

la Mikumi, hasa kwenye Kata ya Kilangali kati ya wananchi na *SumaGrow;* Kata ya Masanze kati ya *Miyombo Estate* na wananchi; Kata ya Tindiga kati ya *Mauzwi Estate* na *NARCO* na wananchi lakini pia Kata ya *Kisanga Estate* na wananchi pamoja na *WEDO* na Stignati:-

Je, Serikali imejipanga vipi kumaliza migogoro hii ambayo ipo katika Jimbo la Mikumi ambayo kwa kweli inahatarisha sana maisha ya wananchi wa Jimbo la Mikumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro hii ameileta hapa na hatujajua wao wenyewe wamefikia wapi. Kwa sababu migogoro mingi Wizara inaingilia kati pale ambapo Halmashauri inakuwa imeshindwa. Mheshimiwa Mbunge amezungumza ni migogoro ya muda mrefu lakini katika ile migogoro ambayo tuko nayo mgogoro anaotaja hatuko nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwahidi tu kwamba kama kuna migogoro kati ya wawekezaji na kata alizozitaja, basi tuko tayari kusaidiana nao kuitatua ili mradi tu tuweze kujua wao wenyewe wamefikia wapi. Kwa sababu mazungumzo lazima yaanzie kwenye eneo husika. Wizara haiwezi kuingia moja kwa moja mpaka ijue wapi wamekwama. Hatujalipokea na wakilileta tutalifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza. Matatizo yaliyoko huko kwenye Shamba la Efatha Mkoa wa Rukwa yanafanana kabisa na matatizo yaliyoko katika Halmashauri ya Itigi shamba lililokuwa linamilikiwa na shirika ambalo limekufa la *Tanganyika Packers.* Serikali haitoi

tamko la moja kwa moja, liko chini ya Msajili wa Hazina, lakini hakuna mwekezaji aliyejitokeza hadi leo hii.

Je, Serikali imekubali sasa kulirudisha shamba hili kwa wananchi kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Itigi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli suala analolizungumzia Mheshimiwa Massare ni la muda mrefu, lakini naomba tu nimpe uhakika kwamba masuala yote ambayo yanasimamiwa na Msajili wa Hazina alishaanza kuyapitia na kuweza kuona mashamba yale au uwekezaji ambao ulikuwepo na ukakwama uko chini ya Hazina sasa hivi, anapitia shamba moja baada ya lingine na akishakamilisha basi anaweza kutoa nini kitawezakufanyika. Hatuwezi kusema sasa hivi kwamba tunalirudisha kwa wananchi wakati Msajili wa Hazina bado anafanyia kazi mashamba hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 39

**Ahadi ya Serikali Kupima Maeneo ya Wananchi Nchini**

**MHE. RHODA E. KUNCHELA** aliuliza:-

Serikali iliahidi kumaliza migogoro ya ardhi kwa kupima maeneo ya wananchi mapema ili kuepuka bomoa bomoa bila fidia:-

Je, ni lini jambo hilo litafikia mwisho?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba kila kipande cha ardhi nchini kinatambuliwa, kinapangwa na kinapimwa. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imenunua vifaa vya kisasa vya upimaji ambavyo vimesambazwa katika kanda zote nane na vinatumiwa na Hamashauri zote ili kurahisisha na kuharakisha upimaji wa maeneo ya wananchi na kutoa hatimiliki za ardhi. Vile vile Wizara inaendelea na utekelezaji wa mkakati wa kupima kila kipande cha ardhi nchini ambapo awamu ya kwanza ya mkakati huu inatekelezwa kupitia Mradi wa Majaribio wa Kuwezesha Umiliki wa Ardhi *(Land Tenure Support Programme)* unaotekelezwa katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi katika Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa kiasi cha shilingi 6,400,000,000 kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 25 kwa ajili ya kupima, kupanga na kumilikisha ardhi. Halmashauri hizo ni Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Halmashauri ya Sumbawanga, Manispaa ya Shinyanga na Iringa, Halmashauri za Miji ya Makambako, Njombe, Kondoa, Nzega, Kahama, Bariadi na Halmashauri za WIlaya za Misungwi, Sengerema, Geita, Nzega, Bukombe, Magu, Chato, Ukerewe, Busega, Simanjiro, Gairo, Songea, Namtumbo na Itilima. Serikali inaendelea kutafuta fedha katika vyanzo mbalimbali ili jambo hili lifikie mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na utekelezaji wa kupima kila kipande cha ardhi nchini, Wizara imeendelea na utekelezaji wa Programu ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa katika maeneo mbalimbali nchini kwa kushirikiana na makampuni binafsi ya kupanga na kupima ardhi yaliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria. Lengo la Serikali ni kuhakikisha maeneo yote yanapangwa na kupimwa ili kukidhi mahitahi ya sasa na ya baadaye na hivyo kuzuia uendelezaji

holela ambapo husababisha migogoro na adha kwa wananchi ikiwemo bomoa bomoa ya makazi yasiyo rasmi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rhoda Kunchela, swali la nyongeza.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Waziri ambayo kimsingi hayajaonesha kutatua migogoro ya ardhi katika Taifa hili, swali la kwanza; migogoro hii imekuwa ni mingi katika mikoa, hususan Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Mwanza na maeneo mengine. Cha kushangaza, majibu haya ya Serikali yanasema kwamba wametenga shilingi bilioni nne. Lengo hapa ni kutatua, kwamba wanapokuwa wanawaondoa wananchi kwenye maeneo yao, kwa sababu Serikali ndiyo inakuwa imefanya uzembe kuwashirikisha wananchi moja kwa moja kuwaondoa katika maeneo yao lakini pia katika suala la kuwalipa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kata ambazo zimeathirika katika Manispaa ya Mpanda ni Kata ya Misunkumilo ambayo iliondolewa na Jeshi, Kata ya Shanwe ambayo ilipisha ujenzi wa barabara lakini pia Kata ya Uwanja wa Ndege ambayo kulikuwa na ujenzi wa Chuo cha Kilimo. Sasa wananchi hawa wanapata shida na hawaelewi hatma yao ya kulipwa fidia zao. Sasa Serikali imepanga nini ii kulipa wananchi hao? *(Makofi)*

swali la pili ni suala la upimaji shirikishi. Serikali imekuwa ikitoa vifaa kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, lakini hakuna ushirikishwaji wa moja kwa moja kwa wananchi kwa maana ya kwamba wanapima maeneo yao lakini kwa wananchi ambao wanakuwa hawana pesa ya kulipia viwanja, angalau basi Serikali ione namna ya kuweza kuchukua; kwa mfano, kama mwananchi ana viwanja vitatu au vine, basi anapimiwa eneo lake na anapewa hatimiliki ili baadaye aweze kulipa hiyo fedha au achukuliwe baadhi ya viwanja ili kukamilisha mchakato wa ulipaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, la pili nadhani ni ushauri. Majibu kwa swali la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimfahamishe Mheshimiwa Rhoda kwamba Serikali imeshachukua hatua za dhati kuhakikisha ya kwamba migogoro yote ya ardhi iliyoko kati ya wananchi na Taasisi mbalimbali ikiwemo Jeshi na wengineo inafikia ukomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameunda Tume ambayo ina Mawaziri wanane, ambao wamepitia maeneo karibu ya mikoa yote na kuweza kupitia maeneo yenye migogoro ili waweze kumshauri Mheshimiwa Rais nini kifanyike katika maeneo hasa ambayo yamekuwa na migogoro mingi. Kwa hiyo, kama kuna eneo lake ambalo pia lina mgogoro na Wanajeshi, nadhani hilo linachukuliwa hatua na baada ya muda siyo mrefu, basi Serikali itatoa maelekezo nini kifanyike katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika suala la kusema kwamba unamwachia mwananchi eneo lake, nadhani Halmashauri nyingi; nimepita katika mikoa zaidi ya 18 na nikatoa maelekezo na nilikuta wengine wameshaanza kufanya kazi yao vizuri. Mfano mzuri ni Halmashauri ya Kalambo ambao walikuta kwamba tayari wana makubaliano na wananchi, wanamwachia asilimia 60 na wao wanachukua 40; na ile asilimia wanammilikisha yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo kwa wananchi wetu, hata ungempa yote, hawezi kuilipia yote. Tumewaelekeza ya kwamba lazima ifanyike kama walivyokubaliana na ukishaipima ile ardhi inakuwa imeshaongezewa thamani. Kwa hiyo, hata kama atauza, yeye mwenyewe hawezi kumiliki, tayari umeshaongeza thamani na iko katika mpango ambao ni wa kimipango miji, kwa hiyo, haiwezi tena kuwa na ujenzi holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba tu Halmashauri zisimamie mambo haya kwa sababu ziko

Halmashauri nyingi ambazo zinafanya wakiwemo Chemba na wengineo ambako tumepita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasisitiza Mheshimiwa Mbunge afuatilie kwenye Halmashairi yake ambayo ni Mamlaka ya Upangaji. Alichosema kwamba Serikali imetoa shilingi milioni nne, siyo shilingi milioni nne, ni shilingi 6,400,000,000/= ambazo zimekwenda kwenye hizo Halmashauri nilizotaja. Tuna imani wakizitumia vizuri wakapanga miji yao, suala la ujenzi holela halitakuwepo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Kibamba sasa aulize swali lake.

Na. 40

**Kumaliza Matatizo ya Maji Nchini**

**MHE. JOHN J. MNYIKA** aliuliza:-

Tarehe 4 Februari Serikali ikijibu hoja binafsi kuhusu upatikanaji wa maji iliahidi kuwa ifikapo mwaka 2016 matatizo ya maji yangekuwa yamemalizika katika Jiji la Dar es Salaam:-

(a) Je, ni kwa nini ahadi hiyo haijatekelezwa kwa wakati?

(b) Je, ni Mitaa ipi katika Jimbo la Kibamba maji hayatoki na ni lini *DAWASA* itahakikisha maji yanatoka katika maeneo hayo?

(c) Je, Serikali iko tayari kuwasilisha katika kila Mkutano wa Bunge Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini kama ilivyokubali katika Bunge la Kumi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Myika,

Mbunge wa Jimbo la Kibamba, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam yanapata maji kama Serikali ilivyoahidi kupitia Bunge lako Tukufu baada ya kukamilisha miradi mikubwa ya maji ambayo ilikamilika mwaka 2016. Serikali inatambua kuna baadhi ya maeneo ya jiji hilo hayajapata maji kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ongezeko la watu na ukuaji wa Jiji la Dar es Salaam pamoja na upatikanaji wa maeneo ya kupitisha miundombinu ya miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 80 ya wakazi wa Jimbo la Kibamba wanapata huduma ya maji. Maeneo ambayo hayapati maji kwa sasa ni maeneo ambayo yapo kwenye miinuko mikubwa. Ili kuhakikisha wananchi wote wa Jimbo la Kibamba wanapata maji, hasa wanaoishi katika miinuko mikubwa, Serikali inaendelea na ujenzi wa matenki katika eneo la Msakuzi Kusini na Maramba Mawili Juu kwa lengo la kuhakikisha wananchi wote wa Jimbo hilo wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi Kiti kilishalitolea mwongozo suala hili katika Mkutano wa Pili, Kikao cha Tisa kilichofanyika tarehe 5 Februari, 2016. Katika mwongozo wa Kiti ilielekezwa kama ifuatavyo; naomba kununukuu; “Bunge la Kumi na Moja litakuwa linaweka utaratibu wake wa namna bora kufikisha maelezo kwa Waheshimiwa Wabunge kwa nyakati tofauti.”

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John John Mnyika, swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, katika majibu yake, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba asilimia 80 ya wananchi wa Kibamba wanapata maji ya bomba, jambo ambalo ni taarifa ya uongo imetolewa Bungeni. Kwa sababu ukiangalia mtandao wa maji ulivyo, kuna maeneo

mengi hayana kabisa mabomba ya maji na hata yenye mabomba ya maji, bado kuna maeneo ambayo hayatoi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoa mfano, kuna kata sita tu Jimbo la Kibamba; Kata ya Goba, Mitaa ya Goba, Matosa, Tegeta A, na kadhalika. Pamoja na Mheshimiwa Waziri kuahidi kwamba Februari maji yatatoka, lakini hayatoki; Kata ya Mbezi, Mitaa ya Mbezi Luisi, Makabe, Msakuzi hakuna kabisa mabomba; Makabe mabomba yapo lakini maji hayatoki; Fijimagohe na Msumi hakuna mambomba; Kata ya Kibamba kule Hondogo, Kibwegere, hakuna mtandao wa maji wa kuwezesha maji kutoka; Kata ya Kwembe, Kinazi B na mitaa mingine kwa ujumla; Kata ya Msigani, maeneo ya Msingwa, maeneo ya Malamba na maeneo mengine yote yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa jibu la Uongo Bungeni, sasa je, yuko tayari kutoa Takwimu ya ukweli ya hali halisi ya upatikanaji wa maji Jimbo la Kibamba na orodha mtaa kwa mtaa ya upatikanaji wa maji na hatua za utekelezaji? Hilo swali la kwanza.

Swali la pili, siku chache zilizopita, Mheshimiwa Rais akiwa ziarani, amesema kwamba Wizara ya Maji ni kati ya Wizara ambayo ina ma-*Engineers* wana-*perform* ovyo ovyo. Kuna miradi mingi ya maji kwa *assessment* ya Wizara ya Maji ambayo ni miradi hewa, badala ya kutoka maji, inatoka hewa. Sasa kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameshatoa hiyo kauli na naamini kauli ya Rais ni agizo:-

Je, Wizara ya Maji iko tayari kuleta Bungeni taarifa ya *assessment* ya Wizara ya Fedha aliyoisema Mheshimiwa Rais ili tupitie hatua kwa hatua, tuchukue hatua juu ya miradi hewa katika maeneo mbalimbali nchini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nimhakikishie kaka yangu Mheshimiwa Mnyika, Serikali imefanya kazi kubwa sana, naye anafahamu kabisa. Kipindi cha nyuma kulikuwa kuna mgao mkubwa sana, lakini sasa hivi kuna utekelezaji zaidi ya asilimia 85 ya upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mnyika anasema taarifa tuliyoisema ni ya uongo. Nisome swali lake kipengele cha (b), anataka kujua ni mitaa ipi katika Jimbo la Kibamba maji hayatoki. Sasa kama Mbunge mitaa yako hujui ipi inayopata maji, unawezaje kuniuliza mimi Mheshimiwa Waziri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwa ushauri mdogo tu, nimshauri kaka yangu, afanye ziara katika Jimbo lake, aone kazi kubwa inayofanywa na Serikali. Aende Hodongo aone utekelezaji wa mradi unaofanyika, aende katika katika Kata ya Matosa aone utekelezaji wa miradi unavyofanyika. Nami niko tayari kuongozana naye nikamwonyeshe kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie, anayelala na mgonjwa ndio unayejua mihemo ya mgonjwa. Namshauri aende Jimboni na afanye ziara aone kazi kubwa inayofanyikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu swali la pili, tunatambua kabisa baadhi ya utekelezaji wa miradi ya maji imekuwa ya kusuasua. Sisi kama Wizara ya Maji tumekuwa tukichukua hatua kwa Wahandisi wababaishaji, lakini pia tumeanzisha Wakala wa Maji Vijijini. Nataka niwahakikishie, tumejipanga vizuri katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. Wahandisi wote wababaishaji hawana nafasi katika Wizara ya Maji, tumejipanga katika kuhakikisha Wakalaa huu unaenda kutatua tatizo la maji vijijini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Masala, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Maeneo ya Mji wa Nachingwea katika Kata za Namatula, Nangwe, Mteruka, pamoja na Kilimanihewa yamekuwa yanapata maji kwa kusuasua sana, lakini wakati huo huo tuna chanzo kikubwa cha maji kinachotokana na chanzo cha maji ya Mbwinji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua mpango wa Serikali juu ya kutoa fedha ili kuweza kufanya utanuzi wa kusambaza maji katika maeneo ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Mbunge. Nimepata nafasi ya kutembelea katika Jimbo lake, lakini kiukweli katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji, lazima tuangalie namna gani tunaweza tukatumia kile chanzo kikubwa cha Mbwinji. Sisi kama Wizara ya Maji tuko tayari na tumejipanga katika kuhakikisha tunatafuta fedha ili tuweze kutumia chanzo kile cha maji ili wananchi wake waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Tatizo la maji la Jiji la Dar es Salaam linafanana kabisa na tatizo la maji la Jiji la Mbeya. Katika Jiji la Mbeya, wataalam wameshasema, *solution* ya tatizo ni kutoa maji kutoka mto Kiwira, *feasibility study* imeshafanyika, taarifa tunazo na mto Kiwira hauko mbali, ni kilomita chache sana kutoka Mbeya. Naamini Mheshimiwa Waziri anajua hata bajeti inayotakiwa kutokana na ile *feasibility study.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni lini fedha itapelekwa katika ile *project* ili ile *project* ifanyike tuondoe tatizo la maji kwenye maeneo ya Uyole, Mwakibete na hususan maeneo kama Shewa ambako wananchi wanapata taabu sana na wako Jijini, wanalipa kodi za Jiji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu kwa swali hilo muhimu sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge wa Jiji la Mbeya, kaka yangu Sugu, amezungumza suala la msingi sana. Kweli tunatambua kabisa katika suala zima la maji katika Jiji la Mbeya kumekuwa na ongezeko kubwa sana la watu, lakini tunaona kabisa tukiyatoa maji mto Kiwira na kuyaleta tutakuwa tumetatua kabisa tatizo la maji. Nataka nimhakikishie kwamba utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara ya Maji tumejipanga katika kuhakikisha kupitia mapato yetu ya ndani lakini pia kwa wafadhili mbalimbali tupate fedha ili tuwekeze na wananchi wa Mbeya waondokane na tatizo hili la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Bulembo, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara ya Maji kuhakikisha inawafikishia wananchi wote maji Tanzania, lakini kumekuwa na kero kubwa na mbaya zaidi kutoka Wizara ya Maji ya kubambikia wananchi bili. *(Makofi)*

Je, ni lini Wizara hii itaweka mkakati wa kutatua kero hii kwa wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni haki ya mwananchi kupatiwa maji, lakini pamoja na haki hiyo ya kupatiwa maji, mwanachi naye ana wajibu wa kulipia bili za maji, lakini siyo kulipia tu, anatakiwa alipie bili za maji ambazo siyo bambikizi. Sisi kama viongozi wa Wizara tumeshawaita Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Maji na tukawapa agizo na kuwaandikia hadi mkataba, kwa maana ya kuhakikisha kwamba hili tatizo wanaliondoa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba ambao tumekubaliana ni katika kuhakikisha Mamlaka zote tunatoka sasa katika mfumo wa zamani tuwe katika *pre-paid meter*. Nataka nitumie nafasi hii tena kuwaagiza kuanzisha suala zima la *pre-paid meter* katika kuhakikisha tunaondokana na malalamiko haya ili kuhakikisha kwamba wananchi wanalipia maji kadri wanavyotumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Profesa Norman Adamson Sigalla, Mbunge wa Makete, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Venance Methusela Mwamoto.

Na. 41

**Ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme Katika Mto Rumakali**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA KING)** aliuliza:-

Kumekuwa na maandalizi ya kuzalisha umeme katika Mto Lumakali uliopo Balogwa Makete na ni miaka 11 sasa wananchi wanaendelea kusubiri ambapo mwaka 2015/2016 Serikali ilitoa kauli kwamba ujenzi huo ungeanza mwaka 2017.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga bwawa hilo kwa ajili ya kuzalisha umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Norman Adamson Sigalla, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kuzalisha umeme katika mto Lumakali unahusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa *MW* 222 na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 220 kutoka eneo patakapojengwa mitambo ya kuzalisha umeme Lumakali hadi Kituo cha Kupooza umeme cha Mbeya. Jumla ya gharama za mradi inakadiliwa kuwa Dola za Marekani milioni 388.22.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Lumakali ulifanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 1998. Kwa sasa Mshauri Mwelekezi wa Mradi anakamilisha mapitio ili kuboresha Upembuzi Yakinifu uliofanyika mwaka 1998 na kazi hiyo itakamilika Mwezi Machi, 2020. Utekelezaji wa Mradi huu utaanza Mwezi Januari, 2021 na kukamlisha mwezi Juni, 2023.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwamoto, swali la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri na kazi nzuri ambayo Wizara ya Nishati na Madini inafanya, sasa naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ulianza toka mwaka 1998, mpaka leo ni takribani miaka 20. Namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri, kama atakuwa tayari sasa kuambatana na Mheshimiwa Profesa Norman King Sigalla ili kwenda kujionea mwenyewe hali inayoendelea ili wananchi wa Makete ambako kumekuwa na matatizo mengi kule yanatokea na barabara hawana, waweze kuwa na imani na Serikali yao.

Swali la pili linalohusu umeme; kwa kuwa kilio na hamu ya Watanzania ni kuona umeme unapita kila sehemu: Je,

sasa, Mheshimiwa Naibu Waziri aliwahi kutoa ushauri kwamba sehemu ambako kuna miradi mikubwa na hakuna umeme, umeme uweze kupelekwa; kikiwepo Kijiji cha Iyai, ambako Mheshimiwa Naibu Waziri ulifika, Kijiji cha Kising'a, Winome, Nyanzwa, Ilindi, Msosa, Kitimbo na Ikula? Je, ni lini sasa Serikali itahakikisha hizo ambazo ilitoa ahadi yenyewe umeme unafika ili wananchi wale waweze kupata umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ya Mheshimiwa Mwamoto ameuliza kwa niaba ya Mheshimiwa Profesa Norman, kwamba ni lini nitakuwa tayari kutembelea Jimbo la Makete? Nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba tulifanya ziara Jimbo la Makete mwaka 2018 mwezi Desemba. Katika mambo mbalimbali ambayo nilishuhudia ni uwepo wa uhitaji wa umeme, lakini uwepo wa vyanzo vingi vya kuzalisha umeme hususan vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Serikali kupitia agizo la Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwamba sasa mchakato wa ujenzi wa bwawa la Lumakali uanze na kwa hatua za awali tumepata mfadhili ambaye ni *World Bank* ambaye ana-*support* hatua hizi za kurudia tena upembuzi yakinifu kwa sababu ulichukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kama jibu langu la msingi lilivyosema, kwamba mradi huu utaanza kama ilivyokusudiwa, mapema mwezi Januari, 2021, kwa sababu Serikali ina dhamira ya dhati ya kuongeza uzalishaji wa umeme kupitia chanzo hiki cha maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge ameyataja maeneo. Ni kweli tumefanya ziara katika Jimbo la Kilolo zaidi ya mara tatu. Mwezi Machi, 2018, mwezi Novemba, 2018 na hivi karibuni tulikuwa na Kamati ya Bunge katika Jimbo lake katika maeneo ya Dinganayo, Ikuvala, lakini maeneo hayo pia

tumewasha umeme na wiki hii tutawasha umeme katika maeneo ya Ngelango, Itungi na Mlavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameeleza jambo la msingi, kwamba kwa kuwa Serikali tulitoa maelekezo, maeneo yote ambako miradi hii ya umeme vijijini yanaunganishiwa, taasisi za Umma na hasa maeneo ya viwanda yapewe kipaumbele. Naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge, mara baada tu ya kujibu swali hili, naomba tukutane naye, tuelekee ofisini tuone namna ya kufuatilia na kwa kuwa amekuwa mfuatiliaji mzuri sana wa miradi ya nishati vijijini na hasa hili eneo la viwanda ambalo amelitaja, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha, eneo hilo litakuwa limepatiwa umeme ili wananchi wale wapate ajira na pia Serikali ipate mapato kupitia vile viwanda. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la umeme limekuwa na kasi na hali ni mbaya katika Jimbo la Mbulu Vijijini na Mheshimiwa Naibu Waziri amefika na vile vijiji alivyoahidi mpaka sasa umeme haujapatikana: Je, atatusaidiaje angalau umeme uweze kupatikana kwenye vijiji alivyoahidi Mbulu Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nilitaarifu Bunge lako, kwamba miradi inayoendelea ya kupeleka umeme vijijini, miradi hii inachukua miezi 24. Kwa mujibu wa taratibu na kwa kuwa hizi *LC (Letter of Credit)* zilifunguliwa mwezi wa Saba mwaka 2018, naomba

niwatie moyo Waheshimiwa Wabunge kwamba tunao muda wa kutekeleza huu mradi na kasi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Flatei amekuwa mfuatiliaji mzuri, msimamizi mzuri, nimeshafanya ziara kwenye Jimbo lake, Mheshimiwa Waziri ameshaenda, tutamsimamia karibu Mkandarasi ambaye anafanya mradi katika maeneo hayo na miradi itakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tumalizie swali la mwisho, Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 42

**Fidia kwa Wananchi Waliopitiwa na Mradi wa Umeme - Babati Mjini**

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

Je, ni lini wananchi wanaodai fidia ya maeneo yao yaliyopitiwa na mradi wa *KV* 400 katika Jimbo la Babati Mjini watalipwa.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, Mbunge wa Babati Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* linatekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Singida hadi Namanga kupitia Arusha. Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 414 na upanuzi wa vituo vya kupozea umeme vya Singida

na Arusha na usambazaji wa umeme katika vijiji 14 vinavyopitiwa na mradi. Gharama za mradi huu ni Dola za Kimarekani milioni 258.82.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulipaji fidia ulianza mwezi Agosti, 2018 baada ya kukamilika kwa zoezi la uthamini na uhakiki wa mali na mazao yatakayoathirika na utekelezaji wa mradi. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2019 fedha zaidi ya shilingi bilioni 31.87 zimeshalipwa kwa waathirika 2,815 kutoka Wilaya za Arusha, Monduri, Babati pamoja na Hanang'.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wilaya ya Babati, fedha zaidi ya shilingi 6,200,800,000 zimeshalipwa kwa wananchi 995 hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2019. Wananchi 86 waliobaki watalipwa fedha zao shilingi milioni 638.18 wakati wowote baada ya kukamilika kwa zoezi la uhakiki linaloendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauli Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Mimi nina mambo mawili, la kwanza ni ombi, la pili ni swali.

Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza naipongeza Serikali. Hivi ninavyoongea leo, tangu siku ya Ijumaa na leo asubuhi Jumatatu watu wa *KV 400* wako Babati eneo la Singu wakilipa wananchi fidia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ombi langu kwa Serikali, kwa kuwa kuna sintofahamu kati ya wananchi na Mwekezaji katika shamba la Singu, wananchi walikuwepo tangu miaka ya 1970, mwekezaji amepewa hati mwaka 2011 na wananchi wanalipwa asilimia 34 leo ya ardhi. Hebu niiombe Wizara ya Ardhi, ilitazame hili jambo upya, waone kati ya wananchi na mwekezaji, ni nani mvamizi, ili haki itendeke wale wananchi walipwe asilimia 100 ya ardhi.

Swali sasa kwa Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Naibu Waziri, siyo wananchi wote wanaolipwa, leo wanalipwa tu Sigino pale, lakini mtaa wa Sawe, Maisaka Kati, Kijiji cha Kiongozi na Malangi, wao cheki zao hazijaandaliwa mpaka sasa. Naomba nifahamu, ni lini Wizara ya Fedha na Mipango nao watamaliza kukamilisha cheki hizi ili na hao wananchi waweze kulipwa? Maana mazao yao yameshafyekwa na mradi unaendelea. Ni lini cheki zao zitafika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo la pili kwa sababu la kwanza ni ombi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo umesema, swali la kwanza ni ombi; lakini kabla sijaendelea, naomba nitoe pole kwa wakazi wa Mkoa wa Manyara, kufuatia kifo cha Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa huo wa Manyara, pamoja na Meneja wa *TANESCO* wa Wilaya ya Mbulu ambao walifariki siku za hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, napenda nijibu hili swali la pili, ambalo Mheshimiwa Pauline Gekul ameuliza Mitaa ya Sawe, Mwaisaka Kati, Kiongozi, lini watalipwa fidia zao? Kwa kuwa Wizara ya Fedha ilifanya uhakiki na kukabainika baadhi ya changamoto na ikapelekea sasa kupeleka watathmini wengine ambao walifanya mapitio; hivi ninavyosema, jedwali jipya ambalo linawasilishwa kwa Ofisi ya Mtathimini Mkuu wa Serikali, limeshafika Dodoma na Mtathimini Mkuu wa Serikali yuko katika hatua za mwisho za kusaini na kisha malipo yataandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake wa hili suala mara kwa mara, pamoja na wananchi wake. Nimwahidi tu kwamba, hili suala kwa kweli kwa kuwa amesema na yeye na sisi tumepokea pongezi, malipo yameanza kwa wakazi wa maeneo hayo ya Sawe, Mwaisaka Kati, Kiongozi, kwamba malipo yatafanyika siyo muda mrefu kuanzia sasa kama ambavyo jibu letu la msingi limesema. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Tatizo la fidia lililopo Babati linafanana kabisa na tatizo la fidia lililopo katika mradi wa umeme wa Rusumo Wilaya ya Ngara. Je, ni lini wananchi wa Kata ya Mlukulazo na Mtobee watalipwa fidia kwa maeneo yao yaliyoathiriwa na mradi wa Rusumo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oliver la masuala ya fidia katika mradi wa bwawa la kuzalisha umeme la Rusumo la megawati 80 pamoja na njia yake ya Msongo wa *KV* 220 kutoka Rusumo - Nyakanazi. Kwanza Mheshimiwa Mbunge Oliver nimpongeze kwa kufuatilia suala hili la malipo ya fidia; lakini kwa kuwa mradi umeanza na fidia ililipwa pengine wapo wananchi ambao wana malalamiko au bado hawajalipwa, naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge, baada ya hapa tu nitalifuatilia kuona wakazi wa Kata ya Mlukulazo na Kata nyingine ambayo ametaja kwamba wanalipwa stahiki zao kwa sababu mradi ule unaendelea mpaka sasa ambao una manufaa makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Sasa niwaletee matangazo tuliyonayo siku ya leo, tutaanza na matangazo ya wageni.

Kwanza ni wageni waliopo jukwaa la Spika, wageni watano wa Mheshimiwa Spika ambao ni Wabunge na

Watumishi wa Bunge la Uganda waliokuja kwa ziara ya kikazi ya siku sita, wageni hao ni Mheshimiwa Ssemujju Ibrahim ambaye ni Mnadhimu Mkuu wa Upinzani, karibu sana, tunaye pia Mheshimiwa Muhindo Harold ambaye ni Naibu Mnadhimu Mkuu wa Upinzani, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Simon Oyet, huyu ni Waziri Kivuli wa Nishati, karibu sana. Tunaye pia Ndugu Sabiti Francis ambaye ni Mchambuzi wa Sera Mkuu, karibu sana, tunaye pia ndugu Ntanda Arinaitwe ambaye ni Mchambuzi wa Sera Mwandamizi, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Ndugu zetu za Uganda siku hizi wanaongea Kiswahili kizuri sana. Kwa hiyo wameelewa yote tuliyosema hapa mbele. *(Makofi)*

Tunao pia wgeni 54 wa kwangu mimi ambao ni viongozi wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM Taifa), kutoka Mikoa yote ya Tanzania wanaongozwa na Ndugu Abdulghafar Idrissa ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa CCM kupitia Vijana, karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Tunza Issa Malapo ambao ni Viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kutoka Mkoani Mtwara na hawa wanaongozwa na Diwani wa Viti Maalum Mheshimiwa Lulu Ngachinja, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni tisa wa Waheshimiwa Wabunge kutoka Mkoa wa Simiyu, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Simiyu na hao wanaongozwa na Ndugu Enock Yakobo ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Simiyu. Wako pia na Ndugu Emmanuel Gungu ambaye ni m-*NEC* Mkoa wa Simiyu, wameongozana pia na Ndugu Donald Magesa ambaye ni Katibu wa CCM Mkoa, wameongozana pia na Ndugu Mayunga George ambaye ni Katibu Mwenezi, Ndugu Jackson Iyuma ambaye ni Mwenyekiti Wazazi - Mkoa, Ndugu

Mariam Manyangu ambaye ni Mwenyekiti wa UWT - Mkoa, Ndugu Lameck Mathias ambaye ni Mwenyekiti UVCCM , yupo pia Ndugu Salu Mleasele ambaye ni Mjumbe na Ndugu Daniel Salamba ambaye ni Mjumbe. Karibuni sana Viongozi kutoka Mkoani Simiyu. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanachuo 61 kutoka Chuo cha Serikari za Mitaa Hombolo kilichopo Jijini Dodoma wanaosoma kozi ya Utawala ambao wamekuja kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunayo pia matangazo mengine; Ofisi ya Mheshimiwa Spika imepata taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo Bungeni na kwa hivyo shughuli zake zitatekelezwa na Mheshimiwa George Mkuchika.

Baada ya matangazo hayo, Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na utaratibu wetu, lakini Mheshimiwa Chenge atakuja kunipokea.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti*

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Ngoja nitulie basi jamani, ndiyo nimechukua meza tulieni kwanza.

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika na nani, Mheshimiwa Sophia.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Taifa la Tanzania tumejiunga na tupo

katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini tumeanza kuonesha ubaguzi ndani ya Bunge letu na sasa tunavuka mipaka ya Taifa letu. Nasimama kwa kanuni 68(7) leo hii Mheshimiwa Naibu Spika wakati anatambulisha wageni, tuna wageni kutoka Bunge la Uganda, lakini wakati anatambulisha kwa sababu ni watu wa Upinzani Ndugu zetu wa CCM hatukuona wakiwakaribisha kama Wabunge wenzetu wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako sisi kama wawakilishi wa wananchi na pia kama tunaosimamia mambo yanayoendeshwa kwa Afrika Mashariki. Naomba Mwongozo wako kujua, je, hata sisi tukitoka kwenye mipaka ya nchi hii kama Wapinzani tukiliwakilisha Bunge lako Tukufu, tukapokuwa hatupokelewi kama tutakuwa tunafanya sahihi?. Naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mapema leo asubuhi tumekabidhiwa orodha ya shughuli za leo Mkutano wa 15, Kikao cha Tano, Tarehe 8 Aprili 2019, ambayo pamoja na mambo mengine kulikuwa na hati za kuwasilishwa mezani, lakini Katiba ya nchi Ibara ya 143(4) inasema:

*"Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha kwa Mheshimiwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ndogo ya (2) ya Ibara hii. Baada ya kupokea taarifa hiyo Mheshimiwa Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Mheshimiwa Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho. Iwapo Mheshimiwa Rais hatachukua hatua za kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Bunge (au Naibu Spika ikiwa kiti cha Spika ki wazi wakati huo au ikiwa kwa sababu yoyote Spika hawezi*

*kutekeleza shughuli zake)ambaye atawasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa sababu taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha kwamba tarehe 28 Machi, Mheshimiwa Rais alipokea ripoti za ukaguzi kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Juni 2018, na kikao cha kwanza cha Bunge kilianza tarehe 2 mwezi huu Aprili ambapo taarifa aliyopokea Mheshimiwa Rais tarehe 28 mwezi Machi hazikuwasilishwa, tarehe 3,4,5 hazikuwasilishwa na Katiba imezungumzia siku saba, haikusema vikao saba wala haikusema siku sana za kazi au zisizokuwa za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mwongozo wako, ni kwa nini katika orodha ya shughuli ya leo hakuna ripoti ya *CAG* kwenye hati zilizowasilishwa mezani, ni kwa nini orodha hii ya shughuli isibadilishwe ili tukaletewa *Supplementary Order Paper* yenye orodha ya shughuli na kama hailetwi leo basi ni tarehe ngapi hasa Mheshimiwa Rais ataagiza wanaohusika walete ripoti ya *CAG* Bungeni kabla haujapita muda wa siku saba ambao Mheshimiwa Rais ametakiwa kwa mujibu wa Katiba kuwasilisha ripoti za *CAG* Bungeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti,, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa kiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni, naomba nami kuomba Mwongozo wako. Kwa kuwa kwa mujibu wa utaratibu wa shughuli za

Bunge, kanuni naijua Mheshimiwa Mnyika kanuni ya 68(7). Kwa hiyo niko hapa mimi ni mtaalam wa kanuni kushinda wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mijadala iliyoendelea Bungeni leo na kwa kuwa Mheshimiwa Mnyika pia wakati akiomba Mwongozo wako ameonesha kujua kuitafsiri Katiba, amejua ku-*quote* vifungu vya Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali; lakini hakwenda mbali zaidi kusoma na Sheria nyingine ambazo zinaambatana na maagizo hayo ya Kikatiba na ya kisheria katika kufanya tafsiri ya siku ambazo zimeandikwa kwenye Katiba na kwenye Sheria zinazohusika na uwasilishaji wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hasa Sheria ya tafsiri za Sheria na hivyo kuonesha wazi anataka kukusudia kuonesha kwamba Serikali haitaki kuwajibika ama haijawajibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, linapotokea jambo kama hili kiti chako kiko tayari kumtafsiria Mheshimiwa Mnyika, tafsiri ya Sheria hizo zote ili asiendelee kulipotosha Bunge na akatuacha Serikali tuendelee kujipanga kwa kuzingatia Sheria, Katiba na taratibu ambazo zinahusika katika utekelezaji wa jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Haule.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nasimama kwa kanuni ya 68(7), nikiwa hapa Bungeni nimepata taarifa za kushtua sana kutoka Jimboni, kwamba katika Kata ya Ruhembe kuna wenzetu kumi wamepotea katika maeneo ya Hifadhi ya pale Mikumi. Wananchi hawa kumi wanatoka kwenye Vijiji vya Ruhembe, Kidogobasi, Kidodi pamoja na maeneo ya Ruaha. Kumekuwa na taaruki kubwa, majonzi, lakini vilio vingi sasa hivi huko katika Jimbo la Mikumi na imekuwa ni tabia watu wakiwa wanalima pembezo mwa hifadhi au wakiwa wanafanya shughuli zao mbili tatu za kuokota kuni na vitu vingine kupotea na kwa kweli imekuwa hatuwapati hao ndugu zetu na tumekuwa kuzika nguo mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeomba, kwa kuwa tuko kwenye Bunge lako Tukufu na Serikali imo humu ndani, naomba Mwongozo wako tuone Serikali inawezaje kuwasaidia hao wananchi wa Ruhembe ili waweze kuwaona ndugu zao kama wako salama au wako maeneo gani ili kuondoa taharuki na majonzi haya ambayo yametawala sasa hivi katika Jimbo la Mikumi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nianze na Mheshimiwa Haule siyo jambo ambalo limetokea mapema humu Bungeni, lakini kwa vile ni tukio ambalo linahusu Watanzania katika Jimbo lako na Serikali na vyombo vyake imo humu Bungeni nadhani wamekusikia vizuri sana na watafanya kila lililo ndani ya uwezo wa Serikali na vyombo vyake kufuatilia.

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, wageni wetu wa kutoka Bunge la Uganda wametangazwa na Mheshimiwa Naibu Spika na unasema Bunge letu limeanza tabia ya ubaguzi, sijaelewa ni kitu gani, lakini umesema kwamba Waheshimiwa Wabunge wanaotokana na Chama cha Mapinduzi hawakushangilia hasa makofi yakipigwa kwenye *Hansard* siwezi nikajua yametoka kulia au kushoto, lakini naamini hawa Viongozi wetu, wageni wetu, wameshangiliwa kwa heshima kama ilivyo ada na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Basi naomba tusilete maneno ya uchokozi uchokozi Mheshimiwa Sophia, tusifanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mnyika, tunaongozwa na *order paper* na niunganishe tu na ya Mheshimiwa Mnadhimu wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni Mheshimiwa Jenista; Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ulivyoisoma lazima pia uisome na Sheria nyingine na Sheria moja ambayo inatuongoza na wewe kama Mwanasheria unafahamu ni Sheria ya tafsiri za maneno yote ambayo yametumika katika Sheria yoyote, Sheria hiyohiyo ya Tafsiri, Sura Na.1 ya nchi yetu ndiyo inatuongoza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa sababu kwanza lenyewe halikutokea humu Bungeni, *order paper* niliyonayo ni ya hapa, hakuna

kitu kama hicho, hati zilizowasilishwa ni hizo. Kwa hiyo nakusihi sana uende ukaisome vizuri Sheria ya Tafsiri tunapo- *define* siku, uende ukaisome vizuri na naamini Serikali haijaenda nje ya utaratibu unaotakiwa na Katiba.

Baada ya kusema hayo sasa tunaendelea, Katibu.

**NDG. ASIA MINJA-KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nina orodha ya wachangiaji wetu kwa siku ya leo. Nitajitahidi tuzingatie orodha hii kama ilivyoletwa mbele yangu na tuanze na Mheshimiwa Alex Gashaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Silanga na Mheshimiwa Gekul ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu na mchango wangu utajikita zaidi katika sekta ya uwekezaji. Kabla sijaanza kutoa mchango wangu, nichukue nafasi hii kwanza kupongeza jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa ajili ya kuwaletea maendeleo Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba nchi yetu imepiga hatua hususani katika sekta hii ya uwekezaji na ndiyo maana hata taarifa mbalimbali zinaonyesha kwamba Tanzania tumepiga hatua. Kwa mfano, *Africa investment Index* inaonyesha jinsi gani ambavyo Tanzania tumepiga hatua na kufikia namba 13 katika nchi 54 za Afrika. Pia ukiangalia hata katika taarifa ya *Where to Investment in Africa* inaonyesha jinsi ambavyo tumepiga hatua hususani katika kuvutia uwekezaji na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna namna ambavyo tunaweza tukapiga hatua na kufikia uchumi wa kati kupitia sekta ya viwanda kama hatutajipanga vizuri na kuona ni namna gani ambavyo tutaweza kwenda katika uwekezaji huu. Kuna kauli inayosema kwamba, *we have to learn from the past for future.* Tutakumbuka kwamba baada ya uhuru chini ya Rsis wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere, baada ya uhuru alijikita kuona ni namna gani ambavyo tunaweza sasa tukakimbizana kuinua uchumi wa Tanzania kupitia sekta hii ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini zipo changamoto nyingi ambazo tumejifunza baada ya kuona baadhi ya viwanda ambavyo tulikuwa navyo wakati huo vilikumbana na changamoto kadhaa wa kadhaa. Awamu hii ya Tano tunapokuja kuwekeza zaidi na kuweka nguvu katika uwekezaji kwenye sekta ya viwanda kama injini ya maendeleo kufikia uchumi wa kati, naamini tumejifunza changamoto ambazo zilitukwamisha wakati ule. Nimpongeze Rais kwa sababu yeye sasa amekuwa ni mbeba maono mapya katika kuwekeza kwenye sekta hii ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tulizokutana nazo baada ya uhuru ni rasilimali watu kwa maana ya wataalam walikuwa wachache, miundombinu ya umeme kwani maeneo yaliyokuwa yameunganishwa kwenye gridi ya Taifa yalikuwa ni machache mno lakini sasa kwa sababu ya maono ambayo anayo Mheshimiwa Rais ndiyo maana tumeanza kujenga msingi ili kuhakikisha kwamba tunapoingia sasa kwenye uwekezaji katika sekta ya viwanda hatukumbani na vikwazo tena. Tunaona jinsi ambavyo amethubutu kuanzisha mradi mkubwa wa umeme *(Stiegler's Gorge)* kwenye Bonde la mto Rufiji, tunaona jinsi ambavyo tunaboresha bandari kwa sababu hizi ni fursa ambazo zitatuwezesha sasa kuweza kuingia kwenye uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna neema kwamba Tanzania kijiografia sehemu kubwa tuko kwenye ufukwe wa bahari ya Hindi na ndiyo maana tukaona ni vyema kuanzisha Maeneo Maalum kwa ajili ya Uwekezaji *(EPZ, SEZ)* na ndiyo njia pekee ambayo inaweza ikatupeleka kuwa na uchumi wa viwanda. Kwa mfano, nchi za China na India, zimepata uhuru kutoka kwa Wakoloni miaka inayofanana, miaka ya 1949. Baada ya kupata uhuru tu ndani ya miongo sita waliangalia ni namna gani sasa ambavyo uhuru wao watautumia kwa ajili ya kuboresha uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hizi zilianza kuwekeza kwenye Maeneo haya Maalum *(EPZ, SEZ)* kwa maana ya *Export Processing Zones* na *Social Economic Zones* kwa lengo la kutaka kuinua uchumi wao. Hiki ndicho ambacho kimeweza kuwafanya waweze kukimbia kwa haraka. Leo China ni nchi ya pili duniani katika uchumi unaokua kwa kasi. Ni ukweli usiopingika kwamba sasa hivi katika sekta ya viwanda, China inaongoza ikiwa ni pamoja na India. Tukiangalia mifano pia hata ya nchi za Bara la Asia (Indonesia, Malaysia na Korea ya Kusini) nao pia kupitia mifumo hii ya uwekezaji wameweza kupiga hatua kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na mapendekezo ya Kamati ya Sheria lakini pia na taarifa za Kamati ambazo zipo katika sekta hii kwamba lazima tuweke nguvu sasa katika kuwekeza na lazima tuangalie ni namna gani ya kuweza kuendelea kupanua maeneo haya ya *EPZ* na *SEZ.* Maeneo yametengwa, najua yapo na ni machache na bado kumekuwepo na changamoto ambazo zinakabili maeneo haya lakini lazima tuangalie ni namna gani sasa tunavyoweza kuendelea kupanua maeneo lakini pia tukiendelea kuboresha na kuondoa vikwazo vya fidia ili kusudi maeneo haya yaweze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapowekeza katika uzalishaji wa viwanda ni lazima tuangalie masoko ya vile tunavyovizalisha. Najua kwamba yapo masoko ya aina mbili, soko la ndani na la nje. Tunapokwenda kwenye ushidani wa

soko la nje lazima tuangalie ni mazingira gani ambayo yanawezesha masoko ya nje kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachoamini, kama tutakuwa tumeweza kuendelea kutengeneza mazingira bora ya uwekezaji, tukaendelea kuita au ku-*attract* wawekezaji wenye tija ambao uwekezaji wao huo utatupa faida kwa maana ya kuongeza mitaji, kuwa na akiba ya fedha za kigeni, kutoa ujuzi kwa maana ya kwamba tuta-*attract* na ujuzi kwa sababu wanatoka kwenye mataifa ambayo yamefanikiwa basi itatuwezesha katika kufanya *exportation* ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi kushindana kwenye soko la nje. Kwa hiyo, lazima yote haya kuyaangalia na kujipanga kuona kwamba sasa ni wawekezaji wa aina gani pia ambao tunawaalika kuwekeza ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa aina yoyote unaoweza kufanyika, uwe uwekezaji kwenye sekta ya viwanda, sekta ya kilimo na sekta ya madini ni lazima tushirikishe idara au sekta mbalimbali. Sekta muhimu katika uwekezaji huu ni pamoja na sekta ya ardhi. Najua kwamba upo mpango wa miaka 20 (2013 - 2033) wa matumizi ya ardhi. Mipango hii inatakiwa iende sambamba kwa sababu kama tutakuwa hatujaweza kutekeleza mpango huu wa matumizi ya ardhi na tukaainisha maeneo ambayo tunahitaji kuwekeza na tuwekeze nini kwa maana ya vipaumbele, tutajikuta tunashindwa kufanikiwa na tunakutana na vikwazo. Ndiyo maana nikasema kwamba lazima tuangalie sasa tunaweka vipaumbele katika uwekezaji upi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine ninukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne kwenye Mkutano wake wa kwanza anahutubia Bunge baada ya uchanguzi wa mwaka 2005. Alijaribu kueleza mafanikio ambayo yamepatikana kutoka na awamu zilizopita. Akasema wakati Awamu ya Pili kulingana na hali ya uchumi ilifikia mahali Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Pili, Mzee wetu Mwinyi ikabidi aanze kuruhusu sasa watu waingize mitumba kulingana na hali ya uchumi tukaingia kwenye biashara ya nje. Kwa hiyo, wakati wa kuruhusu Mzee akaitwa Mzee wa Ruksa, akasema

kwamba hata nzi na mbu waliingia baada ya kufungua madirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sasa naomba niseme kwamba ni vyema tukachukua tahadhari kwa sababu lazima tuwe na vipaumbele kwamba tunataka tuwekeze kwenye nini. Kwa mfano, tunapotaka tusema tuwekeze kwenye viwanda lazima tujue *raw material* zinapatikana kutoka wapi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako, muda wako ndiyo huo umeisha.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa Njalu Silanga atafuatiwa na Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Lucy Owenya ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Nichukue fursa hii kuwapongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa na nzuri sana wanayoifanya katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kutoa pongezi zangu katika Mkoa wetu wa Simiyu hususani Jimbo la Itilima. Serikali ya Awamu ya Tano imeweza kututengea fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya lakini na Hospitali ya Mkoa wa Simiyu. Niwapongeze sana Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, niwapongeze sana Wizara ya Maji kwa kututengea fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi mkubwa wa maji unaotoka Busega kuja Wilayani Bariadi pamoja na Itilima na Meatu kwa ujumla. Shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zingine ni katika suala zima la ujenzi wa kiwanda cha vifaa tiba. Kiwanda hiki kinajengwa katika Mkoa wetu wa Simiyu, Dutwa ambako ndiko kwenye Jimbo lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwashauri watu wa Serikali; pamoja na kwamba sisi Mkoa wa Simiyu na Shinyanga ni wazalishaji wakubwa wa pamba lakini tunaozalisha pamba nyingi nchini ni Mkoa wetu wa Simiyu. Katika kiwanda hiki cha vifaatiba teknolojia iendane sambamba na viwanda vilivyopo sasa kuliko kuwa na teknolojia ndogo matokeo yake haiwezi ikakidhi mahitaji ya wakulima wa Kanda ya Ziwa. Kwa hiyo, Serikali ilitazame jambo hili kwa mapana zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine, tunavyo viwanda vya nguo lakini ukitazama uzalishaji wake na uhitaji wa zao la pamba haufanani. Asilimia 80 tunasafirisha, asilimia 20 ndiyo inayobaki hapa nchini lakini hata hiyo asilimia 20 inayobaki ukikaa na hawa watu wa viwanda wana changamoto zao. Naiomba Serikali, badala sasa ya kuwa na mipango mingi, sera nzuri na kadhalika ni vyema Serikali ikutane na hawa watu na ichukue changamoto walizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Shinyanga kuna kiwanda cha Serikali ya China kiliwekeza kwa ajili ya kutengeneza nguo lakini leo kiwanda kile kinatengeneza nyuzi, kinapeleka nje halafu ndiyo inarudi malighafi. Kwa hiyo, ni suala kujiuliza kama Serikali kwa nini hawa wawekezaji wetu wanaokuja hapa nchini wanatumia gharama ya kuwekeza viwanda hivi na malighafi iko hapa, kila siku tunasema malighafi tunayo ya kutosha lakini kwa nini iende nje na gharama za uzalishaji zinakuwa kubwa katika maeneo yao, unakuta katika uzalishaji mzima hatupati bei nzuri katika mazao yetu. Jambo hili kama Serikali wakilitazama na kujua changamoto zilizoko naamini kabisa Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Uwekezaji ikikutana na hawa watu wanaweza wakapata majibu mazuri na ni kwa nini mazao yetu hayapandi lakini sasa hivi asilimia kubwa utakutana na changamoto hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine; Serikali imekuwa ikiendelea kuweka sera zake nzuri. Tulikuwa na viwanda vya ngozi lakini ngozi wakati ilikuwa ikienda nje kwa maana ya Kenya na sehemu zingine bei zilikuwa kubwa na nzuri sana lakini mkaweka sera ya kwamba viwanda vyetu tuvilinde leo ngozi bei zake ni za kutupa hazieleweki. Kwa hiyo, ni mambo ambayo lazima utafiti wetu ufanyike kwa uhakika zaidi na kufahamu kwa nini tunapoweka hiki bei zinashuka. Katika uwekezaji wetu tunaozungumzia lazima tuangalie mambo muhimu hususani kwenye suala la pamba na viwanda vya ngozi na alizeti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, utakubaliana nami kwamba asilimia kubwa ya wawekezaji wetu wanatoka nje na wawekezaji wetu hawa wanatarajia kupata wataalam kutoka nje lakini sera zilizopo zinawabana kuwa na wataalam wa kuwafundisha vijana wetu hapa nchini kwa sababu *bureaucracy* ni kubwa. Kwa hiyo, hilo nalo wakiliangalia tutatoka kwenye asilimia 20 tutakwenda mpaka kwenye asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini duniani kote, Mheshimiwa mama Kilango wiki iliyopita alitoa mchango wake mzuri sana akatoa mfano wa Bangladesh. Ni-*declare interest* mimi ni mwekezaji na bahati nzuri mwaka 2008 tulikwenda kutembelea Bangladesh, karibu asilimia 70 ya watu wa India wanaishi kwa ajili ya viwanda lakini sisi Tanzania tunavyo viwanda na malighafi kwa nini hatuendelei? Ni swali kwa Serikali kwa nini viwanda hivi haviendelei? Kwa hiyo, lazima wafanye utafiti wa kujua kwa nini viwanda vinavyoanzishwa hapa nchini havi-*perform* kwa sababu zipi na nini kifanyike? Watuletee tutoe ushauri ambao unawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiko kiwanda pale Arusha, Mheshimiwa Jambo alishafunga tangu mwaka 2007 hakijafanya kazi. Ukimuuliza sababu za msingi anazokutana nazo anasema gharama ni kubwa. Kwa hiyo, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara wakutane na hawa wadau wawaulize wala siyo kutuma *Email* au kupiga simu wawaulize

kwa nini viwanda vyetu hivi havi-*perform* na kwa nini bei zake zinakuwa ndogo? Utashangaa bei iliyoko soko la dunia inalingana na mtu anayenunua pamba Shinyanga, Morogoro, Dar es salaam tena la kwake linakuwa chini ukimuuliza anasema gharama ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo moja Waheshimiwa Wabunge wanasema kilo moja ya pamba inazalisha masharti matatu, kilo tatu za pamba ndiyo kilo moja ya mahindi. Kwa hiyo, tunapozungumzia kilo moja ya pamba ina maana ni kilo tatu za mahindi lakini siyo pamba tu hiyo hiyo, kuna malighafi ambayo inatarajiwa kutoka nje ili sasa kuunganisha ili vipatikane hivyo vitu ambavyo vinatajwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni suala la umeme. Tunashukuru Serikali imekuwa na mipango mizuri, sasa mipango hii isiendelee kubaki kwenye makaratasi iteremke kwa wahusika kule ili gharama zipungue ili watu hawa waweze kupata *profit* kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa, narudia kusema na mwaka jana nilitoa mchango wangu, ukiwasha kiwanda bili yako kama ni ya shilingi milioni 30 au 50 utalipa kwa miezi mitatu mfululizo hata kama umezima kiwanda, kwa hiyo, jambo hili ni la kutazama sana. Siamini wenzangu Mheshimiwa Mawaziri kama walishafanya *analysis* hizo. Ukiwasha kiwanda leo ukaendesha ndani ya mwezi mmoja utalipa mfululizo miezi mitatu *KVA.* Mambo kama haya yanatengeneza mazingira watu kuona kwaba uwekezaji hauna faida lakini naamini kabisa kama nchi tunazalisha mazao ya kutosha yote haya tukiyachukua kwa pamoja tunaweza tukafanikiwa na tukapiga hatua kubwa katika suala zima la uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano imejipambanua kwa mambo mazuri makubwa sana hususani kwa wananchi wangu wa Itilima na Mkoa mzima wa Simiyu mambo yaliyofanyika ni makubwa. Naiomba Serikali sasa iongeze *speed* katika ujenzi

wa kiwanda cha vifaatiba pale Dutwa ili mazao yetu yaendelee kupata bei kubwa na nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Gekul atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Gimbi Masaba ajiande.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweke mawazo yangu machache katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu anayetupa nafasi hii ya kusema kwa sababu siyo kwa nguvu zetu wenyewe lakini ni kwa neema zake. Pia tunapochangia, tunachangia yale ambayo tunayaona kwa macho yetu ambayo yamekuwa yakifanyika kwa nia njema tu ya kusaidia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilivyokuwa Ukanda wa Gaza nilisema yafuatayo: “Ni nchi gani hii isiyokuwa hata na ndege ya kuazima, isiyokuwa na nia njema ya kuona kwamba Tanzania tunahitaji kuwa na uchukuzi wetu wenyewe lakini pia tukawa na ndege zetu wenyewe”, bajeti iliyopita nilikuwa mkali sana. Miaka mitano iliyopita nilivyokuwa Mbunge wa Viti Maalum na nilivyokuwa Mbunge wa Jimbo miaka kadhaa nyuma, nimekuwa nikichangia sana suala zima la Tanzania sisi wenyewe kuwa na ndege zetu. Leo nitazungumza tofauti na ile kauli niliyokuwa nikiongea wakati niko Ukanda wa Gaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kwa kunukuu, nukuu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo alimnukuu Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli. Ukurasa wa saba katika hotuba yake, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameandika haya yafuatayo akimnukuu Mheshimiwa Rais, amesema: “Tumekuwa wakimya na hatuelezi kwa kina

masuala tunayofanya. Niwaombe basi viongozi wenzangu wa Serikali, kila tunapopata nafasi tuseme mambo tunayofanya…tusipofanya hivyo yanayosemwa yataonekana kuwa ya kweli". Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hii na nukuu hii inatukumbusha kwamba lazima tuseme mambo ambayo yamekuwa yakifanyika katika nchi yetu ambayo hayajawahi kufanyika. Ni dhahiri kuna mahali tulikuwa tumekwama kama nchi, haiwezekani nchi kubwa tumejaliwa kila kitu lakini hatuna uchukuzi, hatuna ndege zetu na vitu kama hivyo. Kazi kubwa inayofanywa na Serikali hii, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu, wasiposema wengine, tutasema sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze sana hili la Serikali yetu, Mheshimiwa Rais kuhakikisha nchi yetu tunapata ndege zetu wenyewe, imetujengea heshima kubwa sana kama Taifa. Watu hawasemi lakini kipato kinaongezeka na watalii wanaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili niliseme kwa sababu nilisema sana nikiwa upande ule, nikiishangaa nchi hii, ni lini tutakuwa na ndege zetu wenyewe? Leo wametekeleza, hatutaki kupongeza. Naomba nipongeze na hizi jitihada ziendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili, uzalendo huu wa Mheshimiwa Rais Magufuli hata ajuzi tumeona anabadilisha ndege iliyokuwa inatumika kwa ajili ya kubeba viongozi, anaipeleka ibebe Watanzania. Inabadilishwa rangi ili iendelee kuongeza nguvu katika uchukuzi huu. Haya lazima tuyaseme. Naomba tusonge mbele, Mheshimiwa Rais asikate tamaa, amefanya mambo ambayo yalikuwa hayafanyiki na aendelee kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuwe wakweli tu, suala la barabara katika nchi zetu, hakuna mahali barabara na madaraja hayajajengwa. Nimekuwa nikiongea kwamba tuna barabara za lami kila mkoa umeunganishwa

na mkoa mwingine, nimekuwa nikisifia ya Dodoma - Babati lakini juzi tumefika Kilombero tumekutana na daraja la Magufuli kule, wakati siku zote wale watu walikuwa wanahangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuache Kilombero, twende Arusha; Mji mzima barabara zinajengwa kwa fedha hizi ambazo leo tunapitisha bajeti. Vile vile twendeni Dar es Salaam, Wabunge wa Dar es Salaam wanafahamu; mimi nimefika Dar es Salaam juzi, nimeshangaa sana; njia nne kwenda, njia nne kurudi, haijwahi kutokea. Haya mambo tusipoyasema tunamkosea hata Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwenye Bunge lililopita jamani eeh, hebu tusimsifie sana Mheshimiwa Rais, tuangalie, tukosoe kwa upendo. Nilikuwa nasema nikiwa najikaza tu, lakini ukweli unajulikana. Leo niseme kwamba hivi vitu vinaonekana, sisi ni Watanzania, tuache siasa, tuweke ukweli mbele, vitu vinavyofanyika Dar es Salaam kumaliza ile foleni, kumaliza msongamano wa magari barabarani njia nne hizo, upande mmoja mwingine nne, haijawahi kutokea na magari yako *site* na watu wanafanya kazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema ya Jimboni kwangu naweza nikawa najipendelea, lakini kwa sababu ni bajeti ya nchi nzima, ni bora Watanzania tukaongea kazi anayofanya Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana tunabeza; wengi wanabeza, lakini sijawahi kuona ni Mbunge wa awamu ya pili sasa zinatolewa fedha nchi hii kwenda kukamilisha maboma ya sekondari ili watoto wetu wasome vizuri. Ndani ya miaka mitatu hii ya Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kazi ya maendeleo aliyoifanya haielezeki. Hospitali zaidi ya 67 za Wilaya zimejengwa. Kwenye elimu hawaishii hapo, sasa hivi wanamalizia sekondari, ujenzi unaendelea, wanawaza kwenda kukamilisha maboma ya Shule za Msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo Watanzania wanajua. Hata kama kuna watu watasimama watayapinga kwenye Majimbo yao, wanafahamu mioyoni mwao kwamba maendeleo yanafanyika, isipokuwa tu hawawezi kutamka hadharani kama ambavyo mimi nilikuwa siwezi kutamka hadharani nilivyokuwa ukanda wa gaza. *(Kicheko/ Vigelegele/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo maendeleo yanafanyika, hawaangalii, hawabagui, fedha za maendeleo zinatoka. Nenda *SGR,* zaidi ya shilingi trilioni 7.1 fedha za ndani. *Collections* zetu kwa mwaka siyo zaidi ya shilingi trilioni 14, lakini Mheshimiwa Rais huyu ambaye wengi wanasimama wanambeza, wanaibeza Serikali ana-*commit* zaidi ya shilingi trilioni 7.1 kwa ajili ya *SGR* tu. Hajasema mengine ambayo yanafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama le niseme, ingekuwa ni maamuzi yangu tu ningesema hatuna sababu ya kupoteza muda, tuwapitishie bajeti yao Serikali waendelee kufanya kazi, maendeleo yanaonekana. Kuna mtu hapa juzi alisimama akawa anazungumza hoja moja, mioyo ya Watanzania kwa maendeleo haya ambayo yanaendelea, tunatamani Mheshimiwa Rais huyu aendelee kuongoza nchi hii tupate maendeleo. Ninafahamu siyo kauli ya wote inaweza ikawa inakwaza kila mmoja, lakini kwa maendeleo haya yanayofanyika, kila mmoja anaweza akawa ana *feelings* zake moyoni kwamba hivi tunahangaika na uchaguzi kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifika Dar es Salaam nikasema, kwa kazi hii, barabara hizi, kazi zinafanyika *site,* tunakwenda kwenye uchaguzi kumchagua Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli awe Rais, kwa kitu gani tunachotafuta tena? Ni kumwambia endelea, chapa kazi ili Watanzania tupate maendeleo. Tunachotaka ni maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ungeniuliza leo mimi Pauline fedha za uchaguzi kwa nini tunakwenda; labda tuchague huko kwenye Serikali za Mitaa na maeneo mengine. Kwa

Mheshimiwa Rais tunaenda kuchagua kitu gani? Sawa ni Katiba, tunaenda kuchagua kitu gani? Kwa sababu ambayo yamefanyika hayajawahi kufanyika na yanaendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilirusha kwenye mitandao, Mji wetu wa Babati. Siyo fedha tu za barabara tunawekewa, jana nimerusha mpaka taa za barabarani tunawekewa sasa, Mji umewaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie hotuba hii kwa kusema Serikali yetu chapeni kazi, Waheshimiwa Mawaziri chapeni kazi, Mheshimiwa Waziri Mkuu chapa kazi, Mheshimiwa Rais usiwasikilize, kwa sababu hata wanaokutukana, kwenye Majimbo yao hawajatekeleza ahadi zao. Wewe umetekeleza nyingi. Chapa kazi, fedha ni hizi sisi tunakupitishia hizi fedha, wananchi wanataka maendeleo, hawataki maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi/ vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako, umeitendea haki Serikali kwa kazi nzuri inayofanya. Mwenye macho haambiwi tazama.

Tunaendelea, Mheshimiwa Lucy Owenya, atafuatiwa na Mheshimiwa Gimbi na Mheshimiwa William Ngeleja ajiandae.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi niweze kusimama katika Bunge lako Tukufu na kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba niipongeze hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, iwapo hakuisoma lakini naamini kwamba Serikali imesoma na mmeona imefanyiwa utafiti wa kutosha, imesheheni ushauri wa kutosha, nategemea mtaifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie barabara ambayo nimekuwa nikiizungumzia kila leo, barabara iliyopo Moshi Vijijini kutokea Kibororoni kwenda Kikarara hadi Tuduni. Kweli kwa sasa hivi Serikali imetenga fedha, imetengeneza kwa kiasi fulani, lakini haifiki hata kilomita moja. Tunajua sasa hivi kule Moshi masika inaenda kuanza, kwa hiyo, ni mategemeo yangu barabara ile watatengeneza mitaro na ninaomba bajeti ya mwaka huu basi zile kilomita 10 zilizobaki Serikali itenge fedha iweze kuimaliza kwa sababu nimeshaelezea umuhimu wa barabara ile ni barabara ambayo ni ya kitalii na *KINAPA* imeitenga ile barabara kwa ajili ya watu mashuhuri ambao watakuwa wanapanda mlima kwa kupitia barabara ya *Old* Moshi. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu sasa bajeti ya mwaka huu barabara ile itatengewa fedha za kutosha ili iweze kumalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie TEMESA. Serikali imekuwa ikinunua magari ya kifahari kila mwaka na TEMESA zilijengwa kila mkoa kwa lengo la kuhakikisha kwamba gari zote za Serikali zinatengenezwa kwenye karakana za TEMESA. Mashine zilizoko kule TEMESA kwa sasa hivi zimepitwa na wakati, hazifanyi kazi na magari ya kisasa sasa hivi hayawezi kutambulika na zile mashine zilizoko TEMESA kwa sababu teknolojia sasa hivi ni mambo ya kompyuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nategemea sasa Serikali ili kupunguza matumizi itengeneze zile karakana zilizoko kwenye kila mkoa na kuhakikisha kwamba wanaweka vifaa vya kisasa ili kupunguza matumizi, maana yake sasa hivi unakuta Serikali inatengeneza gari inapeleka gari TEMESA, TEMESA wanachukua wanapeleka kwenye *private garage* ambazo ni za Wachina, wao wanaenda kupeleka bili inakuwa mara tatu ya bili ambayo ingetengenezwa na TEMESA. Kwa hiyo, naishauri Serikali ipeleke mafundi wetu waende wakasomee jinsi ya kutengeneza haya magari na mlete sasa teknolojia mpya ambazo zitaweza kutumika katika hizo *garage* ili tuweze kupunguza matumizi kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaenda sambamba na karakana iliyoko Kilimanjaro. Kweli tumenunua ndege nyingi na tunahitaji hizo ndege, lakini tukitengeneza ile karakana iliyoko pale *KIA* ina maana ndege zetu zitaweza kutengenezwa pale pale *KIA.* Badala ya kupeleka ndege Canada mnaweza mkawaambia wale mafundi kutoka Canada wakaja wakatengeneza ndege pale *KIA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni jambo ambalo tumekuwa tukilizungumzia mara nyingi sana, tunarudia na kurudia lakini bado Serikali haijaona umuhimu wa kutengeneza ile karakana. Nataka sasa Mheshimiwa Waziri akija atueleze, kwa jinsi gani mmejipanga kuhakikisha kwamba mnaitengeneza ile karakarana kwa sababu sasa hivi kama nchi tumeanza kuwa na ndege zetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni pamoja na uwanja wa *Moshi Airport*. Uwanja wa *Moshi Airport idea* ilikuwa ni kufanya ule uwanja uwe kwa ajili ya mafunzo ya ma-*pilot.* Sasa hivi na sisi tunasema tuna ndege nyingi, ule uwanja sasa umesahaulika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawahi kuzungumza kipindi kilichopita na ninarudia tena, ule uwanja watu wengi sasa hivi wanalima maharage kule na karanga. Ni aibu. Uwanja ni mzuri kabisa, ulikuwa unatumika, lakini sasa hivi una *potholes* haufahi kabisa, hata ndege ndogo sidhani kama zinaweza kushuka pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hapa atuelezee sasa wana mikakati gani ya kuhakikisha kwamba Moshi *Airport* inatengenezwa na iwe kwa ajili ya mafunzo ya ma-*pilot? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kilimanjaro tuna zile mbio za Kilimanjaro *Marathon.* Mbio hizi zimekuwa zikikua mwaka hadi mwaka. Mfano, mwaka 2014 walikuwa wakimbiaji karibu 4,000; mwaka 2015 wakapanda zaidi

wakafika 7,000; mwaka 2018 wamefika 9,000; na mwaka huu 2019 wako zaidi ya 12,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbio hizi zinafanyika katika uwanja wa Ushirika na uwanja huu unalemewa kwa sababu watu ni wengi. Pale Moshi tuna ule uwanja wa *Kim Memorial.* Uwanja ule una michezo zaidi ya saba, lakini pale kuna soko la mitumba. Sijakataa watu wa mitumba wawe pale, wanaweza wakawepo pale mkawatengea sehemu lakini bado ile sehemu kubwa iliyobaki ikatumika kwa ajili ya michezo. Kama tunavyosema michezo ni afya, lakini watu wa Kilimanjaro hatuna mahali pa kufanya michezo na tunajua magonjwa ya kuambukiza sasa hivi yamekuwa ni mengi na magonjwa ya kuambukiza tunaweza tukajikinga nayo kwa kufanya mazoezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni mategemeo yangu sasa Serikali itatusaidia watu wa Kilimanjaro ule uwanja uweze kutumika sasa maana mwaka unaokuja sasa 2020 ina maana hizi mbio kwa sababu zimezidi kujitangaza watu wanaweza wakafika hata 15,000 na wakifika hivyo, siyo kwamba wanakuja kukimbia tu, wanaleta biashara Moshi, hoteli zinajaa mpaka Arusha na wakija siyo kwamba wanakimbia tu, wanapanda mlima, wanaenda safari, kwa hiyo, inaongeza pato la Taifa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusu uwekezaji. Kiongozi wa Kambi ya Upinzani katika katika hotuba yake ukurasa wa 30 amezungumzia vizuri sana kuhusu uwekezaji. Sasa hivi imekuwa ni kero kwa mtu kuja kuwekeza Tanzania. Kodi ni nyingi sana. Ameainisha hapa kodi zote ambazo zinatakiwa mtu alipe akija kufanya biashara Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ku-*declare,* mimi pia ni mfanyabiashara. Wafanyabiashara wengi wanafunga biashara kwa sasa hivi, kisa tu kodi. Hawakatai kulipa kodi, lakini zile kodi basi ziwe rafiki. Unakuta mfano, *OSHA*; *OSHA* yenyewe unakuta inampa mtu bili ya shilingi zaidi ya shilingi 2,400,000, hujaenda *TBS*; hujalipa *withholding tax;* hujalipa

*income tax;* kodi ni nyingi mno. Hebu jaribuni kufanya hizi kodi ziwe rafiki na mtapata kodi nyingi zaidi na Serikali itapata mapato zaidi. Kwa namna hii, ukienda kuangalia ni wafanyabiashara wangapi wamefunga biashara, ni wengi sana. Kwa hiyo, nafikiri kuna haja ya kuja kuleta sheria hapa na kubadilisha sheria zetu za kodi ndiyo *solution* pekee ambayo tunaweza tukabadilisha mfumo wetu wa kodi hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusu kilimo. Tunasema kilimo ni uti wa mgongo, maneno mengi tu yamekuja. Tunajua kwamba asilimia zaidi ya 80 ya Watanzania ni wakulima, lakini katika hotuba ya Kambi ya Upinzani tumeeleza wazi kabisa 2016/2018 Serikali ilitakiwa itenge shilingi 150,253,000,000/= kwa ajili ya fedha za maendeleo, lakini hadi Machi, 2018 zimetoka tu shilingi bilioni 16.5 sawa na asilimia 11. Hivyo zaidi ya asilimia 89 ya fedha za maendeleo kwa ajili ya kilimo hazikutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama kweli tunataka kuendeleza wakulima wetu, tunasema tunataka Tanzania ya Viwanda, bila kilimo hivyo viwanda tutavitoa wapi? Unakuta tunahitaji watafiti, tunahitaji mbegu ambazo ni za kisasa. Kwa fedha hizi ambazo Serikali imetoa, sioni ni jinsi gani ambayo tunaweza tukaendeleza kilimo hiki. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucy. Mheshimiwa Gimbi Masaba, Mheshimiwa Ngeleja atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru nami kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba nianze kwa kumpongeza Mwenyekiti wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa kazi anayoifanya, lakini pia nimpe pole kwa changamoto anazopitia. Sisi kama Wabunge wa Chama cha Demokrasia

na Maendeleo (CHADEMA) bado tunaendelea kumtia moyo na tunamshukuru kwa kuijenga CHADEMA kama taasisi. Hata kipindi anachopitia changamoto taasisi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na changamoto ambayo naona nisipoisema kidogo nitapata shida sana. Nianze na Mkoa wa Simiyu kabla sijaingia kwenye mambo mengine. Mkoa wa Simiyu umekumbwa na changamoto kwenye Halmashauri zake kwenye suala la uchumi. Halmashauri za Mkoa wa Simiyu zinakabiliwa na uhaba wa fedha, hususan Wilaya ya Itilima. Wilaya ya Itilima ni Wilaya ambayo imeshindwa kujiendesha kutokana na kwamba Wilaya ile ni mpya na haina mapato yoyote ya kuendelea kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Serikali ianze kuchukua mapato kutoka kwenye Halmashauri zetu kumekuwepo na changamoto nyingi sana. Madiwani wanakopwa, hawalipwi posho zao, magari ya Halmashauri hayana *service* hakuna fedha, Wakurugenzi wanashindwa kusafiri kutoka sehemu nyingine kwenda sehemu nyingine kwa sababu hakuna fedha. Historia inaongea ni namna gani Serikali Kuu imeshindwa kukusanya mapato vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017/2018 tulikusanya shilingi bilioni 11.172 na katika mwaka wa fedha 2018/2019 tumekusanya shilingi bilioni 8.434, sawa na upungufu wa *negative* 44.5. Hapa tutaona ni namna gani ambavyo tumeshindwa kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema haya kwa masikitiko makubwa sana kwa sababu, wakati mapato yanakusanywa na Halmashauri zenyewe zilikuwa zina uwezo wa kujiendesha, lakini leo zimeshindwa kujiendesha kwa sababu kwanza wao wenyewe wameingiza hasara kwenye ukusanyaji wa napato takribani bilioni 6.8. Haya kwa nini tunayahitaji kuyaingiza kwenye Taifa letu? Nasisitiza na kuomba sana Serikali warudishe makusanyo kwenye Halmashauri zetu ili ziweze kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba nizungumzie kuhusu bajeti ya maji. Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumza kwenye kitabu chake katika ukurasa wa 55, amesema upatikanaji wa maji umefanikiwa kwa asilimia 85. Historia inaongea, kwenye bajeti ya maji, Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge naomba tuipongeze Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Serikali ya Awamu ya Nne, nimechukua mfano mdogo tu. Bajeti ya mwaka 2012/2013, zilitengwa shilingi bilioni 466, zikatolewa shilingi bilioni 303, sawa na asilimia 65, hii sio mbaya ndio maana nimesema tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne. Mwaka 2013/2014 zilitengwa shilingi bilioni 553, zikapelekwa shilingi bilioni 353 sawa na asilimia 64. Mwaka 2014/2015 zilitengwa bilioni 485, zikatolewa shilingi bilioni 249 sawa na asilimia 50; akaja baba yangu, mwaka 2016/2017, zilitengwa shilingi bilioni 915.1, zikatolewa shilingi bilioni 350.99 tu sawa na asilimia 23. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati kiongozi pale Mheshimiwa John Mnyika ameuliza swali lake akajibiwa kwa kejeli na Serikali ikijinasua kwamba, imetekeleza jukumu la maji kana kwamba, asilimia zote imemaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi takwimu tunazotenga zenye namba nyingi...

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** ...halafu utekelezaji wake unakuwa mdogo, nataka kuuliza ni nani wanayemdanganya? Kwa faida ya nani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gimbi kuna Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe Taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, utekelezaji wa miradi ya maji si kama kilimo cha

matikiti kwamba, mwezi mmoja, mwezi wa tatu unavuna. Utekelezaji unaweza ukawekwa mwaka huu, ukavuka hadi miaka miwili, lakini atambue tu katika Mfuko wa Maji tumetengewa shilingi bilioni 158, mpaka mwezi Februari tumeshapokea zaidi ya shilingi bilioni 93. Pia tuna mitadi mikubwa ambayo inatekelezwa maeneo mbalimbali zaidi ya bilioni 54, milioni 154 zimeshatoka. Kwa hiyo, atambue hilo, nampa taarifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gimbi, Taarifa hiyo.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa siipokei. Kama ana majibu ya kwangu asubiri atanijibu wakati Mawaziri watakapokuwa wana-*wind up*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyasema haya nikisisitiza kwamba, kama Serikali ya nne ilitenga bajeti kidogo, wameona ni namna gani iliweza kutekeleza kwa asilimia ambayo inazungumzika. Hawa wanatenga kwa namba kubwa, matokeo yake utekelezaji ni hakuna, hiyo ndio hoja yangu ya msingi. Sasa nikahoji nani wanamdanganya na ni kwa faida ya nani, kwamba tukiongea namba kubwa, hii itawadanganya wananchi, sasa hali kadhalika hata sisi wenyewe humu Bungeni tunadanganywa. Nawashauri Waheshimiwa Wabunge tusomeni historia ya Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu suala la fedha za maendeleo. Hivyo hivyo historia inazungumza na kabla sijazungumza historia ya Serikali ya Awamu ya Nne nizungumze tu ni kwa mara ya kwanza bajeti ya Serikali ya Awamu ya Tano kutekelezwa kwa asilimia ishirini na... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wetu ndio huo.

Mheshimiwa William Ngeleja, atafuatiwa na Mheshimiwa Chumi na Mheshimiwa Bernadetha Mushashu ajiandae.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimesimama hapa kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kama ambavyo imewasilishwa kwa uzuri. Pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, pia natumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote katika Wizara Kuu inayosimamiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, natumia fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati, Taarifa zilizowasilishwa hapa, zimefanya uchambuzi mzuri unaoturahisishia sisi kuchangia katika hotuba hii. Ni jambo la msingi na kimsingi tumeelezwa hapo kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, utekelezaji ama taarifa yake hii aliyoitoa hapa akiomba fedha za utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika bajeti ijayo itakayoanza mwezi Julai mwaka huu umeongozwa na mambo matatu; moja ni ule Mpango Mkuu wa Miaka Mitano, lakini pia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na ahadi ambazo zimekuwa zikitolewa na viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ujumla wetu hapa ni pamoja na kutoa ushuhuda wa namna ambavyo Serikali imekuwa ikitekeleza yale ambayo tumeyaahidi. Nasimama kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema kuwathibitishia Watanzania wenzangu kwamba, Serikali inatenda inayoahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza hapa, lakini moja kubwa ambalo nataka niwakumbushe Watanzania ambalo linaendelea sasa hivi katika Jimbo la Sengerema na Jimbo la Misungwi ni ule mpango wa ujenzi wa daraja kuu litakalounganisha Wilaya ya Misungwi na Wilaya ya Sengerema na hasa Jimbo la Sengerema. Tenda ilishatangazwa na imeshafunguliwa tayari na sasa wanaendelea na tathmini kumpata mkandarasi atakayefanya ujenzi. Hili ni jambo kubwa sana, linaunganisha sio Tanzania tu wala sio mikoa ya Tanzania, lakini ni pamoja na nchi za jirani zinazotoka upande wa Mashariki Kenya, lakini

pia upande wa Magharibi *DRC,* Burundi, Rwanda na hata majirani zetu wa Uganda. Kwa hivi, jambo hili litaongeza, litasisimua uchumi, lakini pia, litapunguza bughudha na usumbufu ambao tumekuwa tukiupata abiria ama wasafiri tunaounganisha maeneo hayo ya kanda ya ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumesikia ujenzi wa meli katika Ziwa Viktoria, lakini Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Mambo haya ni makubwa ambayo yanakuja kuleta *impact* kubwa katika uchumi wa Taifa. Katika kutekeleza haya na kuhakikisha kwamba, Serikali inatekeleza na kutenda iliyoyaahidi ufuatiliaji wake pia, unafanywa na Mawaziri, Naibu Mawaziri pamoja na Makatibu Wakuu hata Naibu Makatibu Wakuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hapa nikitoa shukrani za dhati kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema kwa ugeni ambao tumeupata hivi karibuni, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Kandege pamoja na Mheshimiwa *Engineer* Nditiye kutoka Wizara ya Ujenzi walifika Sengerema kujionea utekelezaji wa haya ambayo tunayazungumza. Katibu Mkuu Wizara ya Maji pia, Profesa Kitila Mkumbo pamoja na wengine wametutembelea hivi karibuni, yote haya ni kutaka kuonesha kweli Serikali inachokizungumza ndio kile ambacho kinawafikia na wananchi kutendwa kwa ajili ya maslahi na manufaa yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi haya ni mambo makubwa ambayo tusipoyazungumza, kama ambavyo wenzangu wamekuwa wakiyasema, pengine mawe yatakuja yazungumze siku moja, lakini Serikali inafanya kazi kubwa na chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kama mtendaji mkuu tukiongozwa na Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kazi inafanyika. Hii kazi inayofanyika wala haihitaji hata majadiliano kwa sababu ni mambo ya kuyaona moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaitafuta kuifikia nchi ya viwanda Tanzania tunafahamu kwamba, tuna mzigo

mkubwa wa miradi viporo. Nimesikia akitajwa hapa Mheshimiwa Chumi hapa na Mheshimiwa Chumi ni mwanzilishi wa hoja ya miradi viporo hapa kwa kadiri ambavyo tumeizungumza miaka miwili iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena kutoa chagizo kwa Serikali. Najua sasa hivi fedha za miradi hasa ya sekondari zimeshaanza kutoka, lakini tuna miradi mingi inayohusu elimu ya msingi, miundombinu, nyumba za Walimu wa shule za msingi, lakini sekta ya afya kwa mfano, zahanati na baadhi hata ya maeneo ya vituo vya afya na ujenzi wa nyumba za Serikali za Vijiji pamoja na baadhi ya majengo katika ngazi ya kata. Naiomba Serikali kwa kadiri ambavyo iliahidi na hasa mwaka jana, tuliahidiwa hapa na Serikali kwamba, ilikuwa inakwenda kutimiza ahadi yake ya kupeleka fedha katika miradi yote ambayo imeanzishwa miaka iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii miradi viporo natoa msisitizo tena kuiomba Serikali, *speed* iliyoanzanayo sasa iendelee ili tuikamilishe hii miradi ili wananchi wetu waone thamani ya nguvu ambavyo tayari wameshakwisha kuitumia kwa sababu, tunafahamu mpango wetu wananchi wanajenga maboma Serikali inakuja kumalizia. Sasa kadiri tunavyochelewa tunawavunja nguvu wananchi, lakini pia tunaanza tena moja kwa majengo ambayo yatapata kuharibika hasa wakati huu wa mvua. Kwa hivi naiomba sana Serikali iikamilishe ahadi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanasengerema tuna jambo la kuishukuru Serikali, tumepata fedha za kuanza ujenzi wa hospitali itakamilikiwa na Serikali kwa ngazi ya wilaya. Tunasema ahsante sana Wizara ya Afya, ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kulisimamia hili. Tunafahamu sasa hivi kwamba, kuna programu ya ujenzi wa hospitali 67, lakini Sengerema pia, tumepewa taarifa kwamba, milioni 500 zimetengwa na zitafika Sengerema hivi karibuni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hospitali ya wilaya. Sisi tunasema ahsante sana kwa sababu, hatuwezi kuifikia nchi ya viwanda kama tuna wananchi dhaifu na ambao hawapati huduma nzuri za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa inaunganika pia na huduma za afya zinavyoimarishwa ngazi ya Kitaifa. Ni jambo jema, sasa hivi tumeona fedha ambazo zinaokolewa badala ya kwenda kutibiwa watu nje kwa maana kwamba, fursa ya kwenda kutibiwa ipo, lakini kwa sasa kwa kweli, kwa sababu, na kutibiwa nje kwa mara nyingi pia zimekuwa ni bajeti za watu binafsi, tunaona kabisa kwamba, ujenzi na uimarishaji wa sekta hizi unatupa afueni sana kama Taifa kuhusu uimarishaji wa huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linanipa msisimko na kuiunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni hili suala la kusisitiza sekta binafsi, limejitokeza sana na wazungumzaji waliozungumza kabla yangu wamelizunguza kwa kina kwamba, tunahitaji kuipa sekta binafsi nguvu na heshima inayostahili. Tunajua tumekuwa katika kipindi cha mpito na ndio maana ukiangalia kwa mfano katika aya ya 143, Ukurasa wa 67 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukiangalia takwimu za ajira kwa hotuba hii tunavyozungumza, kiasi kikubwa kimetoka kwenye sekta ya umma aslimia 66 na asilimia 34 inatoka kwenye sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu inatokana na miradi mikubwa inayofanyika sasa hivi ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa, lakini sasa tunakwenda pia kwenye *Stiegler's Gorge,* lakini pia, tuna miradi mingi mikubwa inayofanywa na Serikali. Hili ni jambo jema sana, lakini kwa asili tunafahamu kwamba, miradi ya umma mara nyingi ina vipindi vyake, itakapokwisha sekta ambayo itakwenda kututoa na kusisimua ajira kwa Watanzania walio wengi ni sekta binafsi. Ndio maana naungana na wenzangu wote na msisitizo aliotoa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, Serikali inajielekeza sasa kwenda kusisimua ushiriki wa sekta binafsi katika ujenzi wa uchumi wa Taifa letu. Ni jambo la heri, ni jambo jema, ni muhimu sana kuiunga mkono Serikali katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote tunaweza kuyafanya, lakini tumejiwekea utaratibu kuendesha nchi yetu kwa misingi ya kisheria, nazungumzia utungwaji bora wa

sheria. Kama unavyofahamu wewe ni Mwenyekiti wetu kwenye Kamati ya Sheria Ndogo, tumekuwa tukitunga sheria bora, sheria mama, lakini sote tunafahamu miongozo inayoongoza utekelezwaji wa sheria nyingi nchini ni sheria ndogo. Nataka kuelezea msingi na umuhimu wa kuimarisha utungwaji wa sheria ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfumo tulionao sisi kama Taifa, sheria ndogo hizi zinatungwa kwanza na Serikali, halafu ndio zinakuja katika Bunge kuzifanyia kazi kupitia Kamati ya Sheria Ndogo, lakini tuna ushahidi na ilifikia wakati fulani hali ilikuwa mbaya sana tulivyoanza Bunge hili. Hata hivyo, kwa kadri ambavyo taarifa zilikuwa zinaletwa kwenye Kamati yetu ilifikia mpaka asilimia 75 ya sheria ndogo zilizokuwa zinaletwa kwenye kamati yetu zina hitilafu, zina kasoro ambazo bila jicho la Bunge hili Tukufu kupitia Kamati yake ya Sheria Ndogo unayoiongoza wewe Mheshimiwa Mtemi Chenge wananchi wengi wangeumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natoa rai kwa Serikali kuendelea kuboresha utungwaji wa sheria ndogo. Ndio maana na ushahidi upo, juzi tulikuwa na mshikemshike wa suala la kanuni za kikokotoo, wote tunafahamu, Taifa lilisimama... ambazo hazikuwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa...

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na kwa hatua hii naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngeleja. Mheshimiwa Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mushashu na Mheshimiwa Livingstone Lusinde ajiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na nilikuwa nateta hapa na

dada yangu Mheshimiwa Rita, tukasema kwamba, kuna siri katika mafanikio ya hii ofisi. Siri yenyewe nimeona katika watendaji wakuu wa hii ofisi wako hapa saba na ndugu yangu Mheshimiwa Mavunde, lakini katika hawa saba watano ni akinamama, kwa hiyo, kweli, akinamama wanaweza. Mimi ni mtoto wa mama, nalelewa na sasa hivi na mke wangu ni mama, kwa hiyo, akinamama wanaweza. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Umeona, una mabinti wangapi?

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina binti mmoja na yeye najua atanilea wakati ukifika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, kwa haraka kabisa kwanza napenda kupongeza jambo moja kubwa ambalo Serikali na Mheshimiwa Rais amelifanya, nalo ni kutupa Waziri ambaye maalum kabisa atahusika na masuala mazima ya uwekezaji. Pia, napongeza hatua za Serikali kuamua chombo kinachohusika na uwekezaji kwa maana ya *TIC* kukiweka chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nadhani hii itarahisisha utekelezaji wa mipango mbalimbali ambayo Serikali imejiwekea katika kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hivyo tu, naona pia jitihada nyingi ambazo Serikali inazifanya ikiwa ni pamoja na kutengeneza miundombinu wezeshi. Tunaona kuna mradi mkubwa utakaokuja wa umeme, yote hii ni kuhakikisha kwamba, uchumi wa viwanda kwa sababu, uchumi wa viwanda bila kuwa na nishati ya uhakika hatuwezi kuufikia. Kwa hiyo, jitihada hizi bila shaka kila mmoja anayo sababu ya kuzipongeza, tunasema kwamba, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Naamini kabisa kwa Serikali kuamua kuwa na Waziri maalum ambaye atahusika na mambo ya uwekezaji, changamoto nyingi ambazo wawekezaji wale ambao tunawavutia wanakutana nazo, lakini pia na wawekezaji wa ndani, zitaenda kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ninao ushauri kwa Serikali; suala la kwanza nashauri kwamba, pia

tuweze kuangalia magumu gani au vitu gani ambavyo ni changamoto katika ku-*slow down* masuala mazima ya uwekezaji. Kwa mfano, naona kabisa tunayo hii Wizara na tunaye Waziri na tunacho hiki chombo cha *TIC,* lakini kuna maeneo chombo hiki hakina mamlaka ya kufanya maamuzi. Kwa hiyo, niiombe na kuishauri Serikali tuamue kwa wakati, tumekuwa na shida ya kuamua kwa wakati na hata Mheshimiwa Rais mara kadhaa amesema ni afadhali uamue ukosee ufanye marekebisho mbele ya safari kuliko kutoamua kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano; kule kwetu Mafinga tuna kampuni ambayo imekusudia kuajiri vijana 1,000 kwa ajili ya kuvuna gundi kwenye Msitu wa *Sao Hill.* Pengine watu mnaweza mkashangaa kwamba, watu wengi wanadhani kwamba, miti ni kwa ajili tu ya mbao, lakini katika miti pia unaweza ukavuna gundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni hii inavuna gundi ma-*container* kwa ma-*container* na inasafisirisha kupeleka China, lakini sasa wanataka wajenge kiwanda ili ile *processing* iweze kufanyikia pale Mafinga. Maana yake ni kwamba, ajira zitaongezeka, lakini ninapozungumza sasa hivi kuna kitu kinaitwa *National Land Allocation Committee,* ni miezi nane wale wawekezaji bado hawajapata hati ili kuwawezesha kuanza kufanya kazi. Huu natoa ni mfano mmoja tu, lakini unaweza kuona kuna mambo mengi ambayo jitihada hizi zote ambazo zinafanywa na Serikali, kama vyombo mbalimbali ambavyo kwa namna moja au nyingine vina-*cut across* kwenye suala la uwekezaji, hatuwezi kupiga hatua mbele. Maana yake ni kwamba, Mheshimiwa Mama Angella Kairuki na vyombo vyake watabaki tu kuratibu, lakini kama vyombo vingine havifanyi maamuzi kwa wakati hatuwezi kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa pengine ningependa kabisa kuzungumza kuhusu taasisi mbalimbali ambazo zinafanya kazi ya udhibiti, yaani hizi *regulatory authorities.* Nitatoa tu mfano vyombo kama *OSHA, NEMC, TBS, WMA* nikiwa na maana wale Wakala wa Vipimo, *SUMATRA* na

kadhalika. Ningeshauri vyombo hivi ifike wakati vijielekeze katika kufanya kazi ya ku-*facilitate* kuliko ku-*ambush* wawekezaji. Vijielekeze katika kutoa elimu kabla ya kufanya *ambush* na kufanya masuala ya kupiga ma-*penalt.* Kwa kufanya hivyo maana yake ni kwamba tutakuwa kweli yale mazingira bora ya uwekezaji ambayo yanaendana na uwekezaji katika miundombinu kama umeme, barabara na kadhalika yataweza kufanya wawekezaji kweli waje na wawe wenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo maana yake ni kwamba tutakuwa kweli yale mazingira bora ya uwekezaji ambayo yanaendana na uwekezaji katika miundombinu kama umeme, barabara na kadhalika yataweza kufanya wawekezaji kweli waje na wawe wenye tija. Kama hiyo haitoshi, niombe na kushauri pia wakati tuna-*focus* kuvutia wawekezaji kutoka nje tuangalie pia na wale ambao tayari wameshawekeza wanakutana na changamoto gani wanakutana nazo ambazo pengine tukiweza kuwaondolea zitawasaidia wao kupiga hatua na hivyo kuongeza ajira lakini kuongeza pato la uchumi katika taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, natoa rai kwa Serikali na hasa kwa wenzetu wa Kazi na Ajira, uwekezaji huu lazima uendane na ku-*reflect welfare* ya wafanyakazi katika maeneo yale ambayo wanafanya kazi. Hapa nazungumzia kulipwa kwao, masuala mazima ya hifadhi ya jamii na bima za afya. Nitatoa mfano na hili nimelisema mara nyingi, pale Mafinga tuna wawekezaji hasa wa kigeni hawajali na ku-*observe* na ku-*comply* kwenye sheria za kazi. Hawaruhusu vyama vya wafanyakazi, hawalipi bima za afya na hawatoi michango ya wafanyakazi katika mifuko ya hifadhi ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naendelea kutoa rai kwa Mheshimiwa Mavunde naomba ufanye ziara katika Mji wa Mafinga ambako viwanda vipo kwa wingi sana uweze kujionea hali halisi. Pamoja na Mheshimiwa *DC* na *RC* kufanya ziara lakini bado nashauri wewe pia ufanye ziara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kutoka mwisho ni chakula. Natoa ushauri, kutokana na bei ya mahindi kushuka sana, wakulima wa maeneo ambayo chakula kinalimwa kwa wingi kidogo walikata tamaa, hawajalima kama inavyotakiwa na tunaona una hali kidogo ya ukame katika baadhi ya maeneo. Kwa hiyo, nishauri Serikali kupitia Hifadhi ya Chakula inunue chakula cha kutosha iweze kuhifadhi ambapo baadaye itakuja kuuza kwa bei nafuu kwenye maeneo ambayo yatakuwa hayana chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki kama sitazungumzia barabara. Tuna chombo tumeanzisha kinaitwa *TARURA*, Waheshimiwa Wabunge na Serikali kwa ujumla, kama hatutaiwezesha *TARURA* kuwa na fedha za kutosha, nilisema mwaka jana tunaweza tukawa na *TARURA* hata 100, bila fedha za kutosha katika chombo hiki barabara hazitajengwa kama tulivyokusudia. Kweli Serikali imejielekeza katika barabara za kuunganisha mikoa na imefanya kazi nzuri sana lakini sasa nashauri wakati umefika tujielekeze kwenye hizi barabara ambazo zinabeba mazao kutoka vijijini na kuleta kwenye barabara kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mimi pale Mafinga kwa kweli barabara wakati huu wa mvua yaani ni changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, naona suluhisho pekee ni *TARURA* kuwezeshwa kuwa na fedha za kutosha ili kuweza kutengeneza barabara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, napongeza kwa Tanzania ku-*qualify* kwenda *AFCON.* Nimesema mara kadhaa, michezo ni biashara, uchumi na ni ajira. Tutumie fursa hii tunapokwenda Egypt lakini pia tutumie fursa na Waziri Mkuu amesema ya *U-17,* wenzetu wa *TFF* na Baraza la Michezo watusaidie kuratibu katika namna ambayo kufanyika kwa mashindano hayo hapa nchini kutakuwa ni neema kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwe na *management* nzuri ya namna ya kuingia pale uwanjani hasa Uwanja wa

Taifa kwa sababu hamasa ni kubwa, watu wanajitolea kwa wingi kuja uwanjani lakini mtu anafika uwanjani anapoteza saa nzima anaingia uwanjani bado dakika kumi. Ni suala tu la ku-*manage* ili kusudi watu wanapokuja uwanjani viingilio vinapatikana lakini pia hamasa inakuwa kubwa na wananchi wananufaika. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Benardetha Mshashu.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa na mimi nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa na nzuri ambayo inafanywa katika Taifa hili na hasa ukizingatia kwamba yeye ndiyo msimamizi wa kazi na shughuli zote za Serikali ndani ya Taifa hili chini ya uongozi thabiti wa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Nawashukuru sana kwa sababu tumeyaona mambo makubwa yaliyofanyika na mafanikio makubwa ambayo tumeyapata kwenye elimu, afya, madini, nishati na kadhalika. Vilevile nawapongeza Mawaziri, Naibu Mawaziri, Katibu Wakuu na watendaji wote ambao wanafanya kazi chini ya Wizara hii kwa uandishi mzuri wa hotuba hii na utekelezaji uliotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye hotuba hii ukurasa wa 60, Serikali imefanya jambo moja kubwa zuri ambapo imewatambua wazee wetu kwa kuwapatia vitambulisho ili waweze kutibiwa bure. Wazee wetu hawa ndiyo wamejenga Taifa letu, wakiwa vijana wametumia nguvu zao na rasilimali zao kulijenga Taifa hili. Sasa hivi wamezeeka, wameishiwa nguvu, magonjwa yanawaandama kila kukicha, hawana tena mishahara, hawana nguvu za kuweza kutengeneza au kufanya kazi za kuzalisha mali kwa hiyo hawana hela ya kujitibia. Kwa hiyo,

huu mpango mzuri wa Serikali wa kuwatambua wazee na kuwapa vitambulisho watibiwe bure ni mzuri na naupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 60 wanasema hadi sasa wazee ambao wameshapewa vitambulisho ni 1, 042,329. Naomba Serikali iongeze kasi kuwatambua wazee ili ifikapo mwisho wa mwaka huu basi wazee wote wawe wameshatambuliwa na waweze kupewa vitambulisho watibiwe bure katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu, wote tunatambua kwamba katika Tanzania kwa miaka mingi ijayo sekta ya kilimo itaendelea kutoa ajira kwa watu wengi zaidi kuliko sekta nyingine yoyote ile lakini sasa hivi tunaandaa viwanda ambavyo vinategemea kupata malighafi kutoka kwenye sekta hii. Vilevile tunamuona Waziri Mkuu anavyojitahidi kuboresha na kuongeza tija katika mazao ya kimkakati ikiwemo kahawa, pamba, tumbaku, chai pamoja na korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli uzalishaji umeongezeka lakini pamoja na kazi nzuri ambayo imefanyika, tatizo tunalolipata ni masoko. Wote tunakumbuka mwaka juzi tuliona kilichotokea kwenye mbaazi, tatizo lilikuwa ni masoko. Wote tumeona kilichotokea mwaka jana kwenye kahawa na korosho tatizo ni soko na kwenye mahindi kuna wakati yalizalishwa yakakosa soko bei ikawa ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaangalia haya mazao ya kimkakati mengi yanauzwa nje, kwa hiyo, bei ya dunia ikishuka kidogo tu, huku inakuwa ni kiama kwa sababu bei kwa mkulima inaporomoka sana, mkulima anapata hasara.

Kwa hiyo, napendekeza kwa Serikali kwa kuwa haya mazao ya kimkakati yanategemea bei kutoka nje, basi Serikali ianzishe mfuko ambao unaitwa *Crops Price Stabilization Fund* wa kumfidia mkulima kusudi hata kama bei ya dunia ikianguka, mkulima asipate hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili siliongelei mara ya kwanza, ni mara kadhaa nikiwa nachangia nalizungumza, wenzetu nchi za nje kama mkulima kukitokea *natural disasters* bei ikateremka kunakuwa na ruzuku anapewa kusudi asipate hasara. Nasi tuweke mfuko, mwaka huu korosho wamesaidiwa na Rais lakini tukiwa na mfuko unaoeleweka utasaidia kwenye kila zao ambalo bei zitakuwa zimeporomoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa Botswana nilizungumza na mtaalam mmoja nikitaka kujua wao wanawezaje, wao ni wafugaji kama sisi lakini nyama wanauza nje na wanapata hela za kigeni nyingi sana kutokana na mauzo ya nyama. Wakaniambia kwamba siyo kazi rahisi, hawakurupuki tu kwenda kuuza nje, wanaandaa tangu ndama wamemlishaje, wametumia viuatilifu na vyakula gani mpaka wanapokwenda kuuza wanakuwa na masoko tayari, wanazalisha kufuatana na hitaji la soko. Tujiulize tunavyopata matatizo katika kuuza mazao yetu, je, sisi tunapokuwa tunazalisha kahawa, pamba na korosho kuna soko tunalo-*target*, tumejiandaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali kwa kutumia idara ambazo zinahusika na masoko waende huko nje watafute masoko. Watafute nchi marafiki zetu, waingie mikataba nao, watafute mashirika makubwa waingie mikataba nao kusudi tujue kwamba korosho au kahawa ya mtanzania tukishaizalisha tutaenda kuiuza wapi. Vilevile tuandae wakulima waanze kuandaa mazao yao kufuatana na mahitaji ya soko, tusiwaache wakalima vyovyote vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano wa Mkoa wa Kagera. Tunao watu ambao wanauza kahawa nje lakini unakuta wanawalea wale wakulima tangu zao linapoanza, ule mbuni wanalea kwa mwaka mzima, mbolea gani utumie na mbolea gani usitumie, viuatilifu *(insecticides)* gani utumie na vipi usitumie, kusudi unapokuwa umezalisha ile kahawa iwe inakubalika kwenye soko lile ulilolilenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza kwamba sasa tuanze kuwalea wakulima kwa maana ya uzalishaji, tuwezeshe zile taasisi zinazofanya tafiti tuwape fedha kusudi waweze kufanya utafiti wazalishe mbegu bora, wakulima wazipande, tuweke mbolea ya kutosha kwa sababu Tanzania hatutumii mbolea ya kutosha, tuzalishe mazao bora kusudi mwisho wa siku mkulima aweze kupata bei inayofaa kwa sababu tutakuwa tumepata mazao bora. Nasisitiza ni kazi ya Serikali kuwahakikisha kwamba wanatafuta masoko kwa ajili ya mazao ya mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya msimu wa kahawa kwa Mkoa wa Kagera utaanza mwezi ujao wa Mei. Tunaomba Serikali ile mikakati ambayo sasa inapangwa iweze kupelekwa kwa wadau waielewe mapema kusudi tusije tukapata matatizo kama tuliyoyapata kwenye msimu uliopita. Vilevile *direct export* inaruhusiwa, hawa ni wanunuzi binafsi lakini Serikali isitoe kabisa mkono wake, ihakikishe kwamba inaweka bei elekezi kusudi hawa wanunuzi binafsi wasije wakawanyonya wakulima wakawapa bei ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa namalizia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mshashu.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Livingstone Lusinde atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Ngwali na Mheshimiwa Grace Tendega ajiandae.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mungu kwa kunipa nafasi ya kuchangia leo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kunipa

afya na kutuwezesha sisi Wabunge kuweza kukutana mahali hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamempongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na watendaji wote wanaofanya kazi kwenye ofisi yake na mimi nichukue fursa hii kukubaliana nao. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anazozifanya za kiutendaji lakini tumeona yeye na watendaji wake wakuu wote wakitembea na kuzunguka taifa zima ili kuchagiza maendeleo kwenye nchi yetu, tunasema hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za pekee zimuendee Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya kuiongoza Serikali hii ya Awamu ya Tano ambayo imejielekeza kabisa kwenye kuondoa changamoto zilizokuwa zikiwakabili wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi punde kuna Mbunge ametoka kuchangia hapa akiisifu Serikali ya Awamu ya Nne kwa kazi kubwa ilizofanya. Nina hakika Wabunge wengine watakuja kuisifu Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri inazofanya kwa sababu siyo wote tutaona mara moja, wengine wataona baadaye. Kwa hiyo, nina uhakika hata haya yanayofanyika sasa hivi baadaye watakuja kuyaona na kuyapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nisimame kama shuhuda kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtera kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano imefanya kazi kubwa kutuletea pesa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mpwayungu. Wametuletea Sh.1,500,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya pale Mlowa Barabarani njia ya kwenda Iringa. Vilevile upande wa maji wamefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Prof. Kitilya Mkumbo akitembea hata yeye kuangalia miradi kadhaa ya

maji na kuikamilisha pamoja na Waziri na Naibu Waziri wamefanya kazi kubwa sana kuhakikisha Watanzania wanaondokana na dhiki ya maji. Kwa hiyo, mimi kama Mbunge ninayeongoza wananchi ambao wamechanganyika maskini wengi kuliko pengine matajiri, nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kuomba mjielekeze zaidi kwenye kumaliza miradi ya maji ambayo haijakamilika. Vilevile kuanzisha visima vipya na kuna maeneo mengine visima vya zamani vimekauka tuweze kuvifufua ili akina mama wasipate adha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo niliamua wakati napewa nafasi hii kwamba nataka kusema na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla. Tumekuwa tukipokea misaada mingi sana, mingine kutoka nje lakini sisi wenyewe pengine Bunge hili lilishawahi lenyewe kujinyima fursa halafu likachukua pesa zake za Bunge tukaenda kununua madawati. Napongeza sana Bunge kwa uamuzi ule ambao tulijinyima tukasema tuchukue hizi pesa twende tukanunue madawati ya watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema maneno haya? Nasema maneno haya kwa sababu tumepata misaada mingi sana ya kusaidia jamii yetu lakini sasa naomba Taifa hili hebu na sisi tujinyime jambo moja ili tuweze kutoa msaada mkubwa sana kwa nchi yetu. Jambo lenyewe ni hili, ukisoma kwenye ukurasa wa 7 utaona kuna mafanikio lakini ukienda kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 17 kuna habari za Tume ya Taifa ya Uchaguzi inategemea kuongeza vituo 858, hivi vituo vinavyoongezeka bado tunaongeza gharama kubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini nachotaka kushauri? Tumeona uchaguzi mwingine tunaoufanya na wenzetu wamelalamika sana kwamba wakati mwingine tunaingia gharama kubwa bila sababu, naomba Waheshimiwa

Wabunge na Watanzania wote hivi kwa nini mwakani tusifanye uchaguzi wa Diwani na Mbunge tu Rais tukaacha apite bila kupingwa? Kwa nini tusifanye hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tutakuwa tumeokoa fedha nyingi wakati Rais anaapishwa tumkabidhi *cheque* ambayo Taifa hili limeokoa ili Rais aende akatumie hizo fedha kuondoa matatizo ya maji na barabara vijijini. Kuna faida gani kwenda kupoteza pesa chungu zima kwa uchaguzi wa Rais, Rais ambaye hana mpinzani? Hii ni kwa sababu tumeona hata mshindi wa pili aliyepata kura 6,000 ameunganishwa na 8,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu nataka niwashauri, naomba mitandao yote na wanazuoni wote hoja hii naiweka mezani tuangalie faida ambayo tunaipata na hasara zake tupime. Jamani sisi ni Wabunge tuliotokana na familia maskini, tusijisahau tunaongoza watu maskini; watu maskini wakati mwingine huwa wanajadili katika milo mitatu ambayo ni haki yake anaamua kukata milo miwili anakula mlo mmoja, sisi kwa nini tusile mlo mmoja? Tule mlo wa Udiwani na Ubunge, kwenye Urais tumuache Mzee Magufuli apite bila kupingwa. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi aliyoifanya Rais ni kubwa, Taifa hili sasa na lenyewe lijinyime kwenye upande huo badala ya kupoteza pesa bila faida tumkabidhi Mheshimiwa Rais pesa ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya uchaguzi wake tumwambie Rais kamata *cheque* hii ondoa shida ya maji kwa Watanzania. Mshindi namba mbili Ulipo Tupo tayari tayari yupo kule kule na Walipo Tupo wamemfuata huko huko, hivi kweli kuna chama nchi hii kinaweza kutengeneza mgombea Urais kwa miezi tisa (9) akamshinda Magufuli jamani? Ukweli tuuseme, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, badala ya kupoteza muda mimi nawakaribisha tuje tushindane kwenye Ubunge na Udiwani, kwenye nafasi ya Urais tumpe heshima huyu mtu amefanya kazi kubwa. Ameonyesha kwamba yupo

tayari kuondoa changamoto za Watanzania, kusimamia pesa za Watanzania na kuhakikisha mambo yanakwenda.

**WABUNGE FULANI:** Katiba.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Hiyo Katiba ni ya kwetu sasa tuangalie faida ya Katiba na umaskini wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kuna Wabunge wengine humu wanapiga kelele Katiba, kwa sababu Majimbo wanayoongoza hayana watu maskini lakini sisi ambao tunaongoza watu maskini ukiwauliza, ndiyo maana nimesema tujadiliane, naomba tujadiliane hasara na faida ya kufanya huo uchaguzi kwa sababu kwa vyovyote vile hakuna mtu atakayeweza kusimama 2020. Mimi naweka wosia kwenye Bunge hili siyo tu akamshinda, akamtikisa Mzee Magufuli, hayupo! *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu hiyo hatuna sababu ya kutumia mabilioni ya pesa kwenda kupoteza muda na kitu ambacho tuna uhakika. Katiba ni yetu, matatizo na changamoto ni zetu, tupime kama Watanzania. Ndiyo maana nimesema naruhusu mjadala huu na naomba Wabunge mtulie nasema makubwa sana hapa, mnaweza mkapata matatizo wengine hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza na nchi, tuangalie kwa namna nchi yetu ilivyo, ufadhili tunaopokea, na sisi tutoe ufadhili kwa nchi yetu. Tutakumbukwa kwa kitendo hicho kuliko kwenda kupoteza pesa bila sababu yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini nilikuwa nataka kuweka hoja hii mezani Watanzania waijadili waone faida na hasara zake

halafu waamue kuniunga mkono au wasiunge mkono. Naunga mkono hoja hii asilimia mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Toa hoja.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Mheshimiwa Ahmed Ngwali, Mheshimiwa Tendega na Mheshimiwa Boniphace Getere wajiandae.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze hoja yangu na Kituo cha Uwekezaji cha *TIC.* Kituo cha Uwekezaji cha *TIC* kilianzishwa kwa malengo maalum ya kuisaidia nchi katika uwekezaji; kuratibu, kusimamia lakini kuishauri Serikali katika maeneo mbalimbali ili nchi hii katika uwekezaji iende mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba leo wawekezaji wamekuwa wapo katika taabu sana. Utamkuta Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, *OSHA,* Afisa wa *TBS* na Afisa wa *TFDA,* wote hao wana mamlaka ya kumkamata mwekezaji wakaita vyombo vya habari wakamwonesha hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji yule ameleta pesa zake nchini, amewekeza, ameajiri Watanzania; hebu Serikali mtuambie, ninyi mnaona fahari gani? Mnaona sifa gani? Serikali inapata faida gani kumwonesha mwekezaji kama jambazi au mtu ambaye hana maana yoyote? Mtu huyu ameajiri watu chungu nzima na Serikali ipo na watu hawa wanaendelea kufanya mambo mabaya kama hivyo na wanaachiwa tu, hakuna hatua yoyote inayochukuliwa. Hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba Serikali kwenye jambo hili mlikomeshe, likome kabisa, kwa sababu hali ya wawekezaji nchini; hebu niwaeleweshe kwamba wawekezaji ni jamii moja. Mnapomfanyia mmoja tu, dunia nzima inapata taarifa na wanaambiana. Ushindani

wa kibiashara uliokuwepo sasa hivi katika nchi jirani, ninyi mnaujua. Kwa hiyo, siyo jambo jema, ni jambo la aibu kwa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni Kituo cha *TIC.* Kile kituo cha *TIC* cha huduma kwa pamoja *(One Stop Center)* kimewekwa pale kwa ajili ya kusaidia wawekezaji, lakini kile kituo Maafisa waliopelekwa katika eneo lile kwenye kile kituo, hawana mamlaka ya kumaliza hayo matatizo ya wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukitazama Sheria hii ya *Tanzania Investment Act* ya mwaka 1997 kifungu Na. 24 kinawapa mamlaka *TIC* kwa mradi uliosajiliwa pale, watano waruhusiwe waingie kufanya kazi katika hiyo kampuni. Wao wana hiyo sheria, lakini Sheria ya Kazi, *The Non-Citizen Development Regulation Act,* hii inasema sasa yule anaruhusiwa watu watano *automatically,* tena kwa mradi fulani, siyo kampuni. Sasa huyu Kamishna wa Kazi kumpatia hicho kibali sasa cha kufanya kazi inachukua miezi sita, miezi saba, jambo ambalo hizo sheria zina-*contradict.* Kwa nini ikiwa *TIC* sheria imeruhusu, halafu huyu mpaka sasa kuomba kwake anapata shida na mara nyingi zinakuwa *rejection* na *TIC* ndiyo wanaosimamia hiyo shughuli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye Kituo cha Uwekezaji, Sheria ya *Immigration Act* ya mwaka 1995, naye Kamishna wa *Immigration* lazima atoe kibali cha *resident permit.* Mwekezaji lazima awe na vibali viwili, lakini hao *TIC* wenyewe, ukienda kwenye kile kituo cha huduma kwa pamoja huwakuti wala hawana mamlaka. Hivyo nini maana ya kuwepo hicho kituo cha pamoja? Maana yake ni nini? Suala la vibali, tuseme ukweli, nanyi Serikali mnajua vibali vya kazi imekuwa tatizo, shida kubwa sana katika nchi hii. Kama wawekezaji ni wezi, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, Serikali inawachukulia wawekezaji, yaani mwekezaji anaonekana kama kaja katika nchi kuchukua mali za nchi. Mwekezaji siyo hivyo ilivyo jamani. Mheshimiwa Mavunde sasa hivi Kamishna

wa Kazi amekuwa mungu mtu kabisa, imekuwa tatizo kubwa. Sawa, hilo tuliache, lakini katika uwekezaji tuna tatizo lingine ambalo lazima tulioneshe hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mabadiliko ya mara kwa mara ya vivutio vya uwekezaji. Wizara ya Fedha kama Wizara ya Fedha wanajua wanafanya nini kwa wawekezaji. Kwa mfano, ukipitia bajeti ya mwaka 2009/2010 Serikali ilifuta ile *capital goods* ikapelekea idadi ya miradi kushuka kutoka miradi 871 mwaka 2008 mpaka kufika miradi 500 mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha katika bajeti ya mwaka 2012/2013 ilipunguza kiasi cha Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 100 hadi asilimia 90 na pia ikapunguza *VAT* kutoka asilimia 100 mpaka 45. Katika bajeti 2013/2014 Serikali ilipunguza kiasi cha msamaha wa Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 90 mpaka 75. Mambo hayo yote Wizara ya Fedha, vivutio vile vikiwa haviwekwi kwa mpangilio vikawa vya kudumu, mnawasumbua wawekezaji. Wawekezaji wanasumbuka sana. Mwekezaji anakuja kuwekeza leo katika nchi katika vivutio hivi, baada ya mwaka mmoja mnaondoa, hiyo siyo sahihi. Mnafanya vitu vya ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipendekeze kitu kimoja. Mheshimiwa Waziri alete sheria hapa Bungeni, ile *TIC* iwe mamlaka. Ikiwa *authority,* inaweza kutusaidia. Mnapoleta sheria, Maafisa wa *TIC* wakawa ni Maafisa wenye kuweza kuamua, ndiyo tutakapokuwa na maana, lakini ikiwa mtaendelea na utaratibu ambao upo sasa, hakuna chochote mtakachokifanya kikawa. Hakuna uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema ikiwa sheria hizi zitaendelea kuwa kama zilivyokaa kwa namna hii, kama hamjaleta sheria hapa Bungeni tukaibadilisha kuwa mamlaka kama ilivyokuwa Rwanda, Burundi na Kenya, haiwezekani. Maana yake hata tukifika hapa kuja kuzungumza haya maneno, inakuwa mambo yametufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanyaji biashara na sijui msaada gani hasa Kituo cha Uwekezaji kinatoa kwa

wawekezaji wa ndani. Serikali, kwa mfano Wizara ya Maji, inazuia watu wanaosafirisha mchanga kwa ajili ya kuuza wasifanye kazi usiku lakini kuingiza *material* mchana mjini, foleni yake unaijua. Mkandarasi anahitaji *cubic meters 2,000* kwa siku, *local investor* ana uwezo kutokana na hali ya Dar es Salaam ilivyo na sehemu nyingine kupeleka *cubic meters* 100. Kuna nchi gani watu wanazuiwa kupeleka *material* usiku, kufanya kazi usiku jamani? Sisi tunaiga wapi ufanyaji wa biashara? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngwali. Mheshimiwa Grace Tendega, Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Justin Monko na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni ajiandae.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe kwa kazi kubwa yenye changamoto anayoifanya na sisi tuko nyuma yake tutaendelea kufanya kazi naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanzia katika sehemu ya lishe, nazungumzia suala la udumavu. Tanzania ni nchi ya tatu Afrika inayoongoza kwa udumavu na ni nchi ya kumi duniani inayoongoza kwa udumavu wa kiakili na kimwili na vilevile zaidi ya asilimia 42 ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano wana udumavu wa kiakili na kimwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninazungumzia hili? Ninazungumzia hili kwa sababu tunataka tujenge Taifa lenye

watu ambao hawana udumavu, tunataka tujenge Taifa ambalo watu wake watakuwa na maamuzi sahihi, tunataka tujenge Taifa ambalo tutaendeleza kizazi na kizazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahatma Gandhi alisema; *"Ishi kama utakufa kesho na fikiri kama utaishi milele."* Hii ina maana gani? Tunayoyatenga hapa katika bajeti yetu, tunayoyapitisha katika bajeti yetu, basi yaende yakafanye kazi kubwa ya kuweza kuendeleza vizazi na vizazi na siyo ya kuangalia miaka mitano mitano, tuangalie nini mwisho wa kizazi cha Tanzania hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, udumavu huu ninaozungumza unaendana na changamoto nyingi za kukosa elimu hasa kwa hawa watu walioko vijijini na hata wa mijini. Utaona hata sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge tupo tunavyoenda kula pale *canteen* tunakosa kujua ni vipi tule vitakavyokuwa na uimara katika miili yetu na katika afya zetu. Sasa je, wale walioko vijijini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia bajeti inayotengwa, kwa mfano, Sekta ya Maendeleo ya Jamii ambao ndio wanaotakiwa kuelimisha watu katika maeneo ya vijijini, hawaajiriwi. Wanatakiwa waajiriwe Maafisa Maendeleo ya Jamii 4,000 sasa hivi wako 1,700, tuna upungufu wa takribani Maafisa Maendeleo ya Jamii asilimia 57.5. Sasa hii kuonesha kwamba tutaendelea kuwa na kizazi chenye matatizo ya udumavu. Mikoa mingi ambayo ina udumavu wa kimwili na kiakili ni watu ambao pia wana vyakula, ni mikoa ambayo inazalisha chakula, lakini wanakosa upangaji mzuri wa vyakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maziwa yamekuwa ni anasa katika familia zetu, mayai ni anasa katika familia zetu, mtu anaweza akawa na maziwa hanywi maziwa. Wenzetu nchi ya Kenya wanapanga kabisa mtu yeyote lazima anywe lita kadhaa kwa wiki. Sisi Serikali yetu mmejipangaje kuhakikisha hawa wananchi wanapata hiyo elimu? *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli itakuwa ni vigumu sana kwa Serikali yetu hii kufikia malengo tunayohitaji ya milenia yale tunayosema kama hatuwekezi mkakati mzuri wa kutokomeza hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda katika suala lingine, kuna ahadi ya Waziri wa TAMISEMI ambayo aliitoa mwezi Juni, 2018 wakati wa matokeo ya Kidato cha Tano yalivyokuwa yanatoka. Alisema atapeleka shilingi bilioni 29 kujenga madarasa 478 na mabweni 269 kwa watoto waliofaulu kwa Kidato cha Tano. Napenda kujua, wamefikia wapi katika utekelezaji? Tuambiwe tujue wamefikia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya mabweni mnaiona, watoto wa kike, walemavu na wengine wote, mnawaona. Nimekwenda kwenye shule moja unakuta walemavu wanapata changamoto, hakuna uzio kwenye hizo shule, kwa sababu kuna elimu jumuishi. Wale watoto kuna wengine ni *Albino*, wanataka kuibiwa, Serikali mnajipangaje kuhakikisha hiyo elimu jumuishi, hawa watoto wanasoma na wenzao, hawawezi kuibiwa? Hilo ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho ni vizuri wakatuambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni taulo za kike. Mwaka 2018 Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa alitutamkia na tukafurahi kwamba wanafunzi wa kike taulo zitaondolewa *VAT.* Imekuwa ni changamoto, hatujauona mkakati mzuri unawekwa watu wakajua ni zipi ambazo mmeamua zipi salama, zipi siyo salama na wapi na kiasi gani? Hakuna utaratibu unaojilikana. Kama inashindikana, basi tupelekwe kwenye *capitation grants* ili tujue kwamba kule watapata shuleni, maana hilo ndiyo lilikuwa lengo kubwa la *TWPG* na wote ambao tulikuwa tunashiriki katika hilo. Tunaomba ufafanuzi wa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni hili la vitambulisho vya ujasiriamali. Napenda kuuliza, hivi mlifanya utafiti kwamba hawa wajasiriamali shida yao kubwa ni

vitambulisho? Mlifanya utafiti kweli! Kwa sababu akina mama na vijana wanaofanya biashara ndogo ndogo, amebeba ungo ameweka maembe, ameweka mchicha na kila kitu, anatakiwa atozwe hicho kitambulisho atoe shilingi 20,000/=. Sasa mnasema hivi, mliahidi shilingi milioni 50 kila kijiji. Hizo shilingi milioni 50 ziko wapi? Hamjapeleka, leo mnakuja na vitambulisho. Huyu mama anaishia kukimbia. Anavyofanya vile, anataka ajikimu kimaisha, akauze mchicha ili akalishe watoto, akauze mchicha ili aweze kusomesha watoto. Ninyi mnakwenda kuwadai hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata kauli ya Serikali, mlifanya utafiti? Utafiti ulisema wapate vitambulisho? Kama siyo, utekelezaji huo, ni kweli? Kama ni kweli unafanyika hivyo, ndivyo mlivyodhamiria kuwakomboa hao wananchi wanyonge kama mnavyojinasibu? Hao wananchi wanyonge kweli watakomboka hapo? Maana tunakwenda tunaona wanazidi kudidimia kwa umasikini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema udumavu ni tatizo, tukiwa watatu Afrika ni shida, tunapaswa tufikiri zaidi, tuone kwamba ni biashara gani, ni mambo gani ya muhimu ambayo tunatakiwa tuyafanye kuleta maslahi mapana ya Serikali, lakini siyo kwenda kukamata hawa wajasiriamali wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwekezaji. Mnazungumzia uwekezaji lakini changamoto kubwa ya uwekezaji katika nchi hii, mazingira ni magumu mno na ni mabovu mno na yanasababisha watu kushindwa kufanya biashara na kuwekeza katika nchi. Kumekuwa na kauli za viongozi za kukatisha tama. Wawekezaji wengine wanaonekana ni kama wanakuja kuchukua mali na kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri lazima aangalie hili. Wawekezaji ndio watakaosaidia Sekta ya Ajira ipatikane. Kama mtawawekea mlolongo mkubwa wa kodi, mtawawekea mazingira magumu ya kuweza kufanya kazi zao… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Justin Monko na Mheshimiwa Dkt. Chegeni.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia kwenye hotuba hii ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kusema kwamba suala la kum-*support* na kumpa nguvu za kutosha Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, Dkt. John Pombe Magufuli sio la majadiliano tena, ni suala la kumuunga mkono kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kila kitu. Na yale anayoyafanya hayawezi kutufaidisha sisi tuliopo, yatawafaidisha wanaokuja na huku mbele kama wenzetu wa upande wa pili wa Gaza kama watakuja kupata nafasi watafaidi haya matunda ambayo Rais anayafanya kwa sasa, kwenye miaka milioni 200 inayokuja huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze mambo matatu leo, la kwanza nataka nizungumze habari ya *TANAPA.* Shirika hili linatunza hifadhi 16 lakini hifadhi zenye faida ni tano tu, na juzi tumeongeza hifadhi nyingine za BBK, Burigi, Kimisi na hifadhi nyingine zimeongezeka nyingi, hifadhi tano ndiyo zenye faida. Na sasa shirika hili lina michango na kodi ambayo inalipwa kodi ndani ya kodi, likitoa mchango wa kujenga Kituo cha Afya Hunyari, Bunda kodi inakatwa, likilipa *cooperative tax* ndani ya kadi inakatwa, na tumezungumza sana na Kamati ya Bajeti nadhani imepewa hiyo taarifa. Ninafikiri Serikali ione namna gani ya kulipunguzia hili shirika hizi kodi ndani ya kodi ili liweze kujiendesha lenyewe kwa sababu lina mzigo mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani kote mashirika kama haya huwa yanapewa ruzuku lakini *TANAPA* inajitegemea, kwa hiyo naomba waipe nafasi ili iweze kuleta namna ya kujenga miundombinu kwenye maeneo mbalimbali ili tuvutie

wawekezaji na kuleta watalii wengi kama inavyoonesha kwenye hotuba ya Waziri Mkuu kwamba wameongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimeangalia kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 67 fursa za ajira, lakini nikasoma Mpango wa Maendeleo wa Taifa ukurasa wa 23 unasema; upatikanaji wa pembejeo, hatua iliyofikiwa ni kununuliwa kwa lita elfu mbili mia mbili sitini na tisa elfu na kilo elfu tatu vya viatilifu zenye thamani ya shilingi bilioni tisa na hivyo viatilifu vya bilioni tisa vinaua panya, nzige, wadudu viwavijeshi, sasa mimi leo nataka nizungumze fursa ya viwavijeshi na fursa ya vipepeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dunia ya leo kuna soko la mende, kuna soko la panya, kuna soko la mbwa, kuna soko la kwerea kwerea ambalo tunatumia bilioni tisa kuwaua, kuna soko la senene, kuna soko la kila kitu. Nchi yetu tumegawana katika maeneo mawili, eneo moja lina asilimia 36 ambayo ina mambo ya mapori haya, Mapori ya Akiba, *TANAPA*, maeneo tengefu na maeneo yote yaliyoko hapa. Eneo 64 ni letu sisi tunaotumia Watanzania, sasa kama tunalitumia tuna vitu vinaitwa mende, nyoka, mbwa, vinatakiwa kupata masoko ya nje, tutafute namna ya kufungua masoko hayo vinginevyo tunaua ajira, wamezungumza hapa ukurasa wa 67 fursa ya ajira tunatafuta fursa ya ajira katika mende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mende leo ni zao kubwa sana Brazil, ukifuga mende wewe ni bilionea, kwa mfano mkate mmoja Brazili ni laki moja ambayo ni dola 44,000.4 ya Brazil ambayo ni sawasawa na laki moja na watu wanafuga mende sasa hivi wameanza kufuga Njombe. Leo tunapozungumza nyoka tunazungumza soko kubwa sana na viwanda vikubwa sana China. Kwa hiyo, tunafikiri kwamba kuanza leo watu wafuge nyoka kupeleka huko. Tunapozungumza kipepeo leo ni nafasi kubwa sana Malaysia na maeneo mengine.

Kwa hiyo tunapozungumza Kwelea kwelea, mmoja ni dola mia mbili hamsini ambayo ni pesa nyingi sana. Sisi

tunasema tunatumia bilioni tisa kuua wadudu na kibaiologia na mimi ni mtu wa *environment,* unavyotumia ndege kuua wale wadudu maana yake unaua vyura vinavyohitajika, unaua nyoka wanaohitajika kule chini, unaua nzige wanaohitajika huko juu. Kwa hiyo, tunataka kujua ni namna gani eneo la uwekezaji litatumia viumbe hai hivi vilivyopo hapa kutengeneza njia kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wakenya wanashirika la *KWS* ambao wanatumia vibali hivi, kwa hiyo wenzetu wanatumia leo wanyama wetu hai, wanatumia mbwa, nyoka na membe kufunga katika maboksi kwenda nje. Kwa hiyo, tunaomba sasa Serikali najua Mheshimiwa Rais aliwahi kusema katika mambo, wakati huo tunafanya mambo ya ovyo, nasema yalikuwa mambo ya ovyo kupeleka twiga nje na wanyama wengine, lakini mzee alivyokuwa anakemea nchi sasa nchi imetulia, arudi aangalie ni fursa gani sasa ipo ambayo watu wanaweza kuitumia bila kuangalia mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumza hilo ili ieleweke kwamba kuna kuna soko kubwa sana la Afrika la wanyama hao. Pia kuna kitu kinaitwa konokono, Ghana ni chakula kibwa sana konokono na konokono kama mnavyomjua tunaita ni *double entry* anajizalisha mwenyewe*, female and male* yaani ukimfuga konokono mmoja akila majani mazuri hahitaji mume wala mke anajizalisha mwenyewe, anapata soko na ni dola elfu 25. Kwa hiyo ukienda Ghana ni soko kubwa sana kwenye maeneo hayo. Hivyo, naomba hili tatizo tusiogope kutafuta fursa ya mambo ambayo yapo wazi, tulizungumze wazi na vijana wapate ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia habari ya jimboni kwangu. Sisi kule jimboni tumejenga maboma tisa ya maabara za sekondari hayajamalizika kwa sababu nguvu za wananchi zimekuwa kubwa kwenye maeneo haya, tunaomba sasa maeneo yanayohusika waweze ku-*support* wananchi wa Jimbo la Bunda kwenye mambo ya maabara waweze kupata nafasi ya watoto wao kusoma sayansi

ambapo kwa sasa sayansi inakuwa ngumu sana kuisoma kwa sababu maabara hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo la barabara, ambapo barabara ya kutoka Nyamswa kwenda Bunda haijatangazwa na ni muda mrefu sasa tumekuwa tukisema barabara hii itatangazwa itapata mkandarasi tunaomba Wizara inayohusika na wamesikia na Rais amekuja pale akasema itatangazwa hivi karibuni, lakini haijatangazwa. Vile vile barabara ya kutoka Sanzati-Mugumu - Nata haijatangazwa na Rais amefika pale akasema itatangazwa hivi karibuni. Kwa hiyo, tunaomba kwa wanaohusika urekebishaji wa mambo hayo uweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja la Silolisimba Mgeta limekatika na Meneja wa *TARURA* Bunda amelifunga na sasa ni wiki moja. Tunaomba wanaohusika sasa waone namna ya kufungua ile barabara ili wananchi waweze kupeleka ng'ombe zao mnadani na watoto waende shule kwa sababu hali siyo nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nilitaka kusema hayo tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na konokono Mheshimiwa Monko, Dkt, Chegeni na Mheshimiwa Allan Njeza, ajiandae.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nami fursa ya kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Ofisi yake kwa utendaji mahiri wa kusimamia Serikali. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna anavyoiongoza nchi yetu na anavyopambana na rushwa lakini vilevile kufuatilia kwenye miradi ya maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nitazungumzia mambo machache kama matatu, manne hivi. La kwanza kabisa ni suala la kilimo,

katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelezea sana suala la kilimo na vilevile ameelezea suala la Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo - *ASDP II* ambao pia umekuwa na vipaumbele vingi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba vipaumbele vyote hivyo vitaweza kuwaondolea wananchi umaskini, kuongeza tija, lakini vile vile kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika moja ya mpango mkakati ambalo nataka niongelee mimi ni suala la mafuta ya kula. Katika mpango wa *ASDP II* umewekwa mpango mkakati wa kuongeza zao la mchikichi hapa nchini ili kukabiliana na tatizo la mafuta ya kula na sisi wote ni mashahidi hata bajeti iliyopita nchi yetu inatumia zaidi ya bilioni mia nne kumi na sita kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja, zao hili la mchikichi kama ulivyoona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu linafanyiwa kazi katika mpango ambao umewekwa katika mpango wa miaka mine. Hata hivyo, tunayo mazao mengine ambayo yenyewe yanaweza yakatoa matokeo ya haraka. Moja ya zao ambayo yanaweza matokeo ya haraka ni zao letu la alizeti ambalo linalimwa kwenye mikoa mingi hususani mkoa wetu wa Singida. Kwa bahati mbaya sana sioni mkakati wowote wa kuweza kuhakikisha kwamba zao hili la alizeti, linawekewa mkakati wa kuhakikisha kwamba tunakamua na kupata mafuta ya kutosheleza. Pengine hatuhitaji hata kuwa na bajeti ya ziada tunachohitaji ni kupunguza bajeti ya kununua mafuta kutoka nje ya nchi na kuhakikisha kwamba tunakamua alizeti tuliyonayo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza wakulima wetu wanateseka sana kwa soko la alizeti yakiwemo na mazao mengine, sisi kwa Singida tuna zao la vitunguu kwa mfano, hali ni mbaya sana. Pamoja na mkakati mkubwa wa Serikali wa kujenga viwanda na kwa Mkoa wetu wa Singida kwa taarifa zilizopo tumevuka hata lengo la kuwa na viwanda mia moja, ni zaidi ya viwanda mia mbili, lakini bado tunalo tatizo la soko la vitunguu na soko kubwa sana

la alizeti. Mpaka sasa wananchi wanahangaika kuuza alizeti yao, wanahangaika kukamua kidogo kidogo na kuweka kwenye madumu, kusimama barabarani na kupoteza muda mwingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niiombe sana Serikali, ili tuweze kupata matokeo ya haraka katika kuendelea kupoteza fedha nyingi za kigeni kuagiza mafuta, ni vyema Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja, tuone mkakati, mahususi kwa ajili ya hili zao la alizeti ili kusudi tuweze kuwasaidia wananchi hawa, kwa sababu hili ni zao ambalo ndani ya mwaka mmoja alihitaji kusubiri kama ulivyo mchikichi. Kwa hiyo, wakati tutakapokuwa tunaendelea kusubiri zao la mchikichi ni vema tukajikita kwenye zao la alizeti na mazao mengine ambayo yanaweza kutoa mafuta na matokeo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika sekta ya maji, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sekta ya maji hasa vijijini imekuwa kutoka asilimia 58.7 na kufikia asilimia 64.8. Kasi hii naiona bado ni ndogo na wananchi wengi bado hawajapata maji. Kwa mkoa wetu wa Singida sisi tumefikia asilimia 49 peke yake kwa upande wa vijijini. Hali hii ni mbaya sana, sasa niiombe Serikali tumebakiwa na mwaka mmoja wa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inatutaka tufikie asilimia 85 kwa vijijini na asilimia 95 kwa mijini, tuiombe sana Wizara ya Maji ambayo sasa hivi imechukua jukumu badala ya Halmashauri, watoe vibali kwa ajili ya miradi ya maji iliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019, ili miradi hiyo itangazwe. Hatutaweza kufikia malengo kama Bunge limetenga fedha, halafu Wizara bado haijaweza kutoa vibali na miradi mingi ya mwaka huu wa fedha unaoendelea haijaweza kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la uwezeshaji, nilikuwa najaribu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, wamefanya kazi, lakini kwa kweli bado kuna changamoto nyingi. Ukiangalia kwenye takwimu ambazo zipo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukienda kwenye ukurasa kwa mfano wa 28 kupitia *TADB* zimetolewa shilingi bilioni 107

ambazo zimewanufaisha wananchi kama milioni moja hivi. Ukijaribu kuangalia maana yake ni kwamba ni sawasawa na mwananchi moja kwa wastani amepata shilingi laki moja na mia saba. Ukienda ukurasa wa 34 kupitia *SIDO* zimetolewa shilingi bilioni 1.74 ambazo zimenufaisha vikundi au wananchi elfu moja na kumi na tatu kwa wastani wa shilingi milioni moja na laki saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukienda kwenye ukurasa wa 66 kwenye upande wa mafunzo hasa kwa vijana ambao ndiyo tatizo kubwa la nchi yetu, tunasema vijana hapa ni asilimia sitini, lakini vijana ambao tumewapa mafunzo nchi nzima ni vijana elfu thelathini na mbili mia tano na sitini na tatu, hapa tunahitaji kuongeza juhudi. Naomba sana Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye inashughulika na masuala ya vijana, tunaendelea kwa kweli kukuza tatizo hili kama tukienda kwa kasi ya kushughulika na vijana elfu thelathini na mbili peke yake ambayo haifikii hata asilimia 0.1. Kwa hiyo, niombe sana, suala hili lirekebishwe na kuhakikisha vijana hawa wanasaidiwa mitaji, wananchi wetu wanaweza wakakopeshwa kwa wingi, siyo kwa kiwango hiki cha nchi nzima, viwango hivi vingeweza kufaa kuzungumza kama viwango vya mkoa na si viwango vya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la mwisho nisemehe kwa upande wa umeme. Naipongeza sana Serikali kwa juhudi kubwa, Serikali ya Awamu ya Tano ambayo imeanza sana kupeleka umeme vijijini, lakini niombe sana juhudi hizi ziongezwe, kwa sababu kwa mujibu wa takwimu bado tuko asilimia 47 pekee kwa nchi nzima. Niseme tu kwa Jimbo langu la Singida Kaskazini mimi ni vijiji 19 peke yake kati ya vijiji 53 ambavyo viko kwenye mradi. Ukichukua kwenye vijiji vyote 84 maana yake sisi ni asilimia 22.6, kwa hiyo, kama wastani wa nchi ni asilimia 47 sisi bado tupo chini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Monko.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu wote ambao wameweza kutoa pongezi na hasa katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuandaa bajeti hii vizuri na naomba tumpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nina sababu kuu mbili za kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu; katika Mawaziri Wakuu ambao wameshapita katika nchi hii, huyu namwona Waziri Mkuu wa kipekee kwa sababu kwanza anazunguka, kuifahamu nchi na kuwatumikia Watanzania vizuri zaidi, lakini pia anafuatilia vizuri sana utekelezaji wa miradi ya Serikali na shughuli za Serikali kwa ujumla. Tunatakiwa tumpongeze kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa huyu ndio kiongozi wa shughuli za Serikali hapa Bungeni, niunge mkono vilevile, kwamba hotuba yake hii ya bajeti ya bilioni mia moja na arobaini na nane tumpatie bila hata kupunguza hata shilingi moja, kwa sababu anahitaji hizi fedha ili kwatumikia Watanzania. Serikali ya Awamu ya Tano imejipambanua kwa mambo mengi sana, wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, hivi ni wapi ambapo leo hii katika nchi hii hutaona shughuli zinaendelea? Iwe za miundombinu, za maji, za elimu, za afya na kadha wa kadha. Hii imesaidia sasa kuwafungua Watanzania na ndiyo maana kuna siku hapa Mheshimiwa Mbunge Profesa Tibaijuka alisema kwamba, unapopanua huduma ndiyo watu wanahitaji zaidi. Kwa hiyo, Watanzania sasa tunahitaji zaidi maendeleo, kwa sababu tumeanza kuona maendeleo yanakuja. Awamu zote zilifanya kazi vizuri sana, lakini Awamu ya Tano kwa muda wa miaka mine, nadhani kila mmoja anaona na kama anaona, basi kuna kila sababu ya kupongeza shughuli za zinazofanywa na Serikali yetu ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia katika miradi mingi kwa mfano ya miundombinu, tumeona barabara nyingi zinajengwa, miradi ya umeme tumeona, mradi wa *REA* sasa hivi katika nchi hii, tunalalamika kwamba baadhi ya vijiji havijafikiwa, lakini karibu kila kijiji miradi hii imeshaanza kutekelezwa. Hii ni hatua moja muhimu sana na naomba tupongeze sana kwamba Serikali inafanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika yote haya nataka niseme kwamba tunahitaji kuifungua nchi vizuri tuwe na *priorities* za kimkakati ili tuweze kuendelea tunahitaji kufungua nchi vizuri zaidi, maeneo ambayo ni ya kimkakati tuyaendeleze zaidi. Mheshimiwa Rais alikuwa kule Mtwara, amezungumza vizuri sana namna ya kufungua korido ya Kusini; kuna korido ya Mbeya, uwanja wa ndege wa Songwe, naomba sana sana hicho ni kitega uchumi cha muhimu sana katika nchi yetu hii. Kwa hiyo, lazima ukamilishwe kwa wakati na uweze kutoa huduma, uwanja wa ndege wa Mwanza ukamilishwe vizuri ili uweze kutoa huduma vizuri zaidi, kwa sababu umechukua sehemu kubwa ya mahitaji na watu ambao wanahitaji kuutumia na kwa kiuchumi uko kimkakati zaidi. Pia uwanja wa ndege wa Mtwara na viwanja vingine ambavyo vimetajwa ikiwepo Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia sana kufungua nchi yetu, lakini tukiangalia Serikali hii ya Awamu ya Tano tumeweza kuwapata wawekezaji wa umma na wa sekta binafsi, uwekezaji wa umma hadi sasa hivi Serikali imewekeza zaidi ya trilioni 54.8 na mwaka jana kwa mara ya kwanza tumepata gawio la shilingi bilioni 830. Tunapaswa tupongeze sana Serikali hii kwa sababu kuna baadhi ya makampuni na mashirika yalikuwa hayawezi kutoa gawio kwa Serikali, lakini yameweza kutambua umuhimu huu, sasa yanachangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Hii ni jitihada muhimu sana kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ambazo zipo na Waheshimiwa Wabunge nadhani wamezungumza na wengine pia tuzungumze, kuhusu ukamilishaji wa miradi,

najua kuna vipaumbele vingi lakini vile vile tunapoanzisha miradi tuikamilishe. Kwa mfano, majengo ya halmashauri hizi mpya za wilaya, kwa mfano Wilaya yangu ya Busega tumejenga jengo huu ni mwaka wa nne halijakamilika. Ukiangalia gharama zinaongezeka.

Kwa hiyo ningeomba kwamba Serikali iweke utaratibu majengo ambayo kwa wilaya ambazo hazijawahi kujengewa majengo mapya basi zijengewe majengo hayo yakamilike ndani ya muda ili kusudi tuepuke kuongezeka kwa gharama za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maboma ya Zahanati, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza hapa na madarasa, wananchi wamechangia nguvu ningeomba sana Serikali kupitia bajeti hii tuelekeze nguvu zetu kuhakikisha maboma haya ya zahanati pamoja na maboma ya madarasa yanakamilishwa ili kusudi tupange kingine zaidi. Mnapoanza kitu msipokamilisha mnaanza kingine, inakuwa ni tatizo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji; mimi na wewe nadhani tupongeze sana Serikali hii kwa sababu tuna mradi mkubwa sana wa maji kutoka Ziwa Victoria. Chanzo cha maji kinaanzia pale Busega, mradi huu ni wa kitaifa na utahudumia vijiji vingi na mikoa mbalimbali. Naomba miradi huu utekelezwe kwa wakati, kwa sababu mradi huu fedha zake zinatoka kwenye *Climate Fund,* basi ukamilishwe kwa wakati. Naomba taratibu zote za ujenzi zifanyike na uweze kukamilika

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi ambayo bado najiuliza sana ni *TARURA. TARURA* Waheshimiwa Wabunge nadhani mtaniunga mkono, wanahitaji kusimamiwa vizuri. *TARURA* tumewapa majukumu lakini hata na Halmashauri hawako pamoja, hawaingii kwenye vikao inavyotakiwa. Pili, wanafanya miradi hata Madiwani hawajui miradi inavyotekelezwa. Naomba sana kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, suala la *TARURA* liangaliwe vizuri zaidi ili kusudi liweze kuwa na tija katika kutekeleza miradi yetu ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunahitaji maisha bora, tunayapataje, ni lazima tuwekeze na sekta binafsi lazima iangaliwe. Nashukuru sana Mheshimiwa Rais ameunda Wizara ya Uwekezaji na wamepata Waziri mahiri, naamini Waziri huyu akipewa ushirikiano atafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tumeona wawekezaji wengi wanakuja hapa Tanzania halafu wanaondoka bila kuwekeza kwa sababu ya ukiritimba. Pia bado kuna vitu ambavyo vinakinzana kati ya vitu ambavyo vinampa mwekezaji *incentives* au vivutio vya uwekezaji ambavyo ukienda *TRA* kwa Mamlaka ya Kodi vinakuwa vinakinzana, matokeo yake mwekezaji anasumbuliwa. Bado kuna vitu vingine ambavyo vinafanya mwekezaji ili aweze kuwekeza vizuri anapata shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la vibali vya ufanyaji kazi. Mheshimiwa Jenista Mhagama analifahamu hili, tunaomba sana kuwe na *coordination* nzuri. Kwa sababu huyu Waziri wa Uwekezaji kama Waziri ameshaomba vibali vya wawekezaji lazima mshirikiane, msomane vizuri zaidi kwa sababu tuta-*frustrate* wawekezaji ambao ni *genuine* kwa sababu ya vibali, kumbe masikini hamjapata taarifa sahihi tu. Huyu atajitahidi kutafuta wawekezaji wanakuja hapa nchini, anaongea nao vizuri zaidi, ana wa-*assure* kwamba Serikali itawapa kila aina ya msaada inapokuja suala la vibali, kunatokea sintofahamu ya hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama nchi tusafiri pamoja, kama Serikali msafiri pamoja ili kusudi tusi-*frustrate* wawekezaji. Ukishampoteza mmoja umepoteza karibu 100. Hii kwetu sisi inatu-*cost* sasa hivi, unakwenda kwenye nchi ambayo haina chochote wala lolote wanasema eti uwekezaji ni mzuri zaidi kuliko kwetu sisi. Naomba tuondokane na dhana hii na naomba sana Mheshimiwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Chegeni, muda wako umeisha.

Tunaendelea na Mheshimiwa Oran Njeza na kama muda utaruhusu Mheshimiwa Ally Saleh (Alberto).

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa hii fursa nami nichangie katika bajeti muhimu Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kasi kubwa anayoifanya kuhakikisha kuwa Serikali yetu inaendeshwa na kuleta ufanisi katika maeneo yote ili uwepo ufanisi katika kuwaletea wananchi maendeleo ya kiuchumi na pia ya kijamii. Napenda pia kuwapongeza Mawaziri wote na watendaji wote wa Wizara hii na bila kusahau kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuleta *transformation* (mageuzi) makubwa kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda labda napenda niorodheshe machache tu aliyofanya nikianzia kwenye Jimbo langu. Kwenye suala la umeme tulikuwa na vijiji 10 tu mwaka 2015 lakini leo tuna asilimia karibu 80 ya vijiji vinavyokaribia 200. Angalia ni mafanikio ya aina gani ambayo yamepatikana katika kipindi hiki kifupi. Pia tunategemea hizi kata mbili zilizobaki nazo zitakamilishwa ndani ya miaka hii miwili. Tunashukuru sana kwa utendaji wa Wizara na Mheshimiwa Rais kwa maagizo yake yeye mwenyewe ambayo yametufanya Mbeya Vijiji tukafanya vizuri kwenye nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la afya. Katika Wilaya yetu ya Mbeya tulikuwa hatuna Hospitali ya Wilaya na katika Miji mikubwa kama Mbalizi tulikuwa hatuna hata kituo cha afya lakini katika kipindi hiki cha miaka mitatu tumeweza kufanikiwa kujenga vituo vya kisasa vitatu katika Kata za Ilembo, Ikukwa na Santilia. Kwa kuongezea, tumepata na pesa kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Wilaya.

Tunaishukuru sana Serikali, kwa kweli hayo ni mageuzi makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo tuishukuru vilevile Serikali kwa kuweza kuifikiria Mbeya Vijijini kutuletea Chuo Kikuu cha Afya. Chuo hiki kitakuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Muhimbili ambacho nategemea katika mikakati kitaanza kufanya kazi hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu nalo tumefanya vizuri sana, imeirudisha Mbeya katika zile nafasi zake muhimu. Kwa mwaka huu Mbeya iko kwenye nafasi 10 bora na kitaaluma maeneo yote tumefanya vizuri mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jimbo langu tumeweza kuongeza shule tatu za sekondari na shule moja ya *high school.* Katika hizo shule tatu, tuna shule ya wasichana ya bweni ambayo imejengwa na wananchi lakini tumepata msaada kidogo wa Serikali. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwa hilo na tunategemea waendelee tena kuipa msukumo elimu kwa vile ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miundombinu Serikali imetufanyia mengi mazuri ikiwemo barabara lakini bado tuna changamoto kubwa kwenye barabara zetu za Mbeya Vijijini. Kama alivyosema mwenzangu aliyotangulia tuna tatizo la *TARURA*. *TARURA* wanafanya kazi vizuri lakini bajeti yao ni ndogo. Bajeti ya matengenezo ya dharura hakuna, sasa kwa maeneo ya mvua nyingi kama Mbeya Vijijini wanatengeneza barabara leo, madaraja yote unakuta yameondolewa na mafuriko, hawana namna ya kutusaidia. Tunaiomba Serikali iangalie namna gani itaboresha bajeti ya *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la maji, Wizara ya Maji pamoja na Serikali kwa ujumla wamefanya kazi kubwa kwa Halmashauri yetu ya Wilaya ya Mbeya. Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wamekuja

wao na wameweza kusukuma na tumekamilisha miradi ya vijiji karibu zaidi ya 10. Tumekamilisha miradi ya Mbawi, Jojo, Haporoto na Idimi na sasa hivi tunakamilisha vijiji kwenye Kata za Igale na Izumbwe lakini bado tunahitaji maboresho kwenye Mji Mdogo wa Mbalizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la kilimo ambacho ndiyo msingi wa kila kitu, kwa kweli pamoja na juhudi za wananchi lakini bado tuna changamoto kubwa za masoko. Naiomba Serikali ijaribu kuangalia ni namna gani itaboreshe masoko ya mazao yetu. Kwenye kahawa, pareto na hata mahindi hatufanyi vizuri. Pamoja na matumizi ya mbolea napo hatuko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie namna gani tutumie malighafi tulizonazo hapa nchi kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya pembejeo. Chokaa inazalishwa sana hapa nchini lakini ni muhimu sana kama sehemu ya pembejeo. Chokaa inasaidia kutibu ardhi kwa vile ina *calcium* na *magnesium* ambayo inasaidia ardhi yetu iliyochoka ili mbolea iweze kutumika vizuri. Ukiweza kufanya *application* ya chokaa udongo utakuwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la kahawa, juzi tulikuwa na Mkutano wa Wadau wa Kahawa na niishukuru sana Bodi ya Kahawa iliandaa mkutano mzuri sana, tukaangalia changamoto nyingi sana. Kitu ambacho nimekipenda ni mkakati wa kuboresha soko la kahawa ambalo napenda msisitizo uwe kwenye *direct export,* wananchi waweze kuuza kahawa yao moja kwa moja nje ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile na uanzishwaji wa hiki chombo kipya kinaitwa *Tanzania Commodity Exchange Market (TMX)* inaweza kutusaidia kutuokoa katika janga kubwa ambapo kahawa yetu ni nzuri lakini bei yake ni ndogo ukilinganisha na wenzetu wa jirani. Kwa mfano tu, kahawa ya Kenya arabica wenzetu katika kipindi hiki wanauza mpaka dola 200 kwa kilo 50 sisi ni chini ya dola 100 pamoja na kahawa yetu kuwa nzuri kuliko yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna pareto, nashangaa ni kwa nini haijaingizwa katika mazao muhimu ya kimkakati. Tanzania sisi tunaongoza Afrika kwa kulima pareto na ni wa pili duniani. Sasa zao kama hili la kimkakati ni kwa nini limesahauliwa na fursa bado zipo za kuweza kuzalisha pareto nyingi, mahitaji ni zaidi ya tani 20,000 na uzalishaji duniani ni chini ya tani 10,000. Tanzania pamoja na kuwa wa pili na wa kwanza Afrika tunazalisha tani 1,000 tu. Katika zao hili nalo naomba suala la masoko liweze kutiliwa maanani ili wananchi waweze kupata faida ya uzalishaji wa pareto.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Njeza, muda wetu hauko rafiki.

**MHE. ORAN M. NJEZA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Ally Saleh (Alberto), hayupo, Mheshimiwa Kiswaga Boniventura.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nilikuwa mbali sana nikiamini kwamba nitachangia mchana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa namna inavyoendesha nchi na kuwahudumia wananchi wake. Pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri na Makatibu Wakuu na wote ambao wanaomsaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa imefanyika kwa nchi hii ambayo wengi hawakuitarajia lakini ndani ya miaka minne tumeshuhudia mengi na nchi imepiga hatua hasa katika huduma za kijamii. Sina sababu ya kuzitaja kwa sababu kila mmoja wetu anafahamu jambo hili. Naomba niishukuru

Serikali hapa karibuni imetoa fedha za kuezeka madarasa na kukamilisha madarasa yetu ya shule za sekondari lakini bado tunauhitaji wa maboma yale ya zahanati zetu pamoja na shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nizungumzie sehemu ndogo sana lakini ni kubwa kwa nchi hii hasa kwenye suala la wastaafu. Watumishi wetu wa Serikali wa kada mbalimbali; walimu, madaktari, wataalam wa ugani na kadhalika, wanaitumikia nchi hii kwa uadilifu mkubwa sana. Hakuna hata mmoja wetu hapa ambaye hajapita kwa mwalimu, daktari na manesi, hata kama hujatibiwa lakini mama yako alipita *labour*, hata kama hakwenda *labour* alihudhuria kliniki, kwa hiyo, watumishi hawa wanafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunasema kwamba walimu ni wito lakini hawa walimu wanaifanya kazi ya Yesu mwenyewe ya kufundisha wanadamu ili waweze kuelewa mambo yote hapa duniani. Huyu daktari na nesi tunasema hiyo kazi ni ya wito lakini hawa nao wanafanya kazi ya Mungu mwenyewe ya kurudisha uhai wa mwanadamu, kazi hizi ni nzito sana. Inapofika sasa wakati wa kustaafu, mafao yao hayaandaliwi kwa wakati. Wako watumishi wamestaafu wamemaliza zaidi ya miezi sita bila kulipwa mafao. Pia wakati huo wakiwa wanasubiri mafao hawalipwi nusu mshahara wao kwa miezi hiyo, tunawatesa sana watumishi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe na kuishauri Wizara kwa sababu taarifa za mtumishi huwa zinafika Wizarani kabla ya miezi sita kustaafu, kwa nini mtumishi huyu asiandaliwe mafao yake kwa uharaka? Tunamfanya mtumishi huyu akiwa anasubiri mafao kwenda kukopa mikopo ambapo anaingia mikopo ya riba kubwa ya asilimia 100, anapokuja kupata mafao yake yanaishia kwenye riba, hatumtendei haki mtumishi huyu.

Naishauri Wizara hii iweze kuandaa mapema iwezekanavyo mafao ya watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtumishi huyu anapotumika miaka 35 anafikisha miaka 60 ya kustaafu kimsingi amechoka anahitaji kupata mafao yake kwa uharaka zaidi. Wakati akisubiri mafao yake, wakati mwingine anapokuja kulipwa yale malimbikizo yake ya nusu mshahara hayapati kwa wakati pia. Niiombe Serikali ya Awamu ya Tano kama ambavyo Mheshimiwa Rais alipoangalia Kikokotoo na kuwahurumia watumishi maskini wa nchi hii akarudisha asilimia zote zilizokuwepo na mafao yao yaendane na muda. Tunaimani mifuko hii wanakochangia watumishi orodha ipo tayari ni uvivu tu wa Wizara kupeleka majina yao ili waweze kupata mafao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii watumishi tunawategemea na watumishi hawa anapokwenda kupumzika anayo mengi ya kufanya. Kama hatutamtendea haki mtumishi mstaafu hatutakuwa tumewatendea haki Watanzania. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Hukubaliani na suala la wastaafu?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni taarifa nampa Mheshimiwa Kiswaga.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Kiswaga na ikiwezekana arekebishe kauli tu yake kuhusiana na Kikokotoo, siyo Mheshimiwa Rais aliyewaonea huruma ni Mheshimiwa Ester Bulaya ndiye aliyepiga kelele sana kama Waziri Kivuli wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei taarifa hiyo kwa sababu haina kichwa wala miguu. Nataka niseme kwamba mwenye maamuzi na jambo lolote kwenye nchi hii ni Mheshimiwa Rais, ndiye aliyefanya uamuzi. Unaweza ukapiga kelele na kelele yako isisikilizwe kama hatuna kiongozi mwenye huruma. Mheshimiwa John Pombe Magufuli ni kiongozi mwenye huruma anayehurumia wananchi wake. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengi ambayo yanafanywa na Serikali. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kumuweka Waziri anayeshughulikia Uwekezaji kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. Hata hivyo, yako manung'uniko mengi ya wawekezaji hasa mtu anapotaka kuwekeza kiwanda, iko mifumo mbalimbali ambayo sisi Wabunge ama nchi tumeiweka mwekezaji apitie hatua hizo ili akafikie uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Uwekezaji ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu angalia mifumo yote ambayo haileti tija, inamkwamisha mwekezaji ulete mapendekezo hapa tuweze kuweka utaratibu mzuri ambao utawasababisha wawekezaji wawekeze kwa urahisi zaidi la sivyo tutakuwa tunasema kwamba wawekezaji wanakwenda kuwekeza nchi nyingine. Tunayo mifano mingi hatuna sababu ya kutaja majina yao lakini watu wamekuja kutafuta uwekezaji hapa nchini lakini kwa *bureaucracy* za taasisi hizo wamekwenda kuwekeza nchi nyingine, Watanzania tunakosa ajira, fedha na kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana tuiangalie *NEMC* kwani haina watumishi wa kutosha kufika kila eneo ambalo mwekezaji anaomba kuwekeza kiwanda chake...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nilistahili nipate dakika 15 nilikuwa na mengi ya kuchangia lakini basi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu ndiyo huo umeisha. Nina tangazo moja hapa la Mheshimiwa Cosato Chumi, alikuwa na mgeni wake Mheshimiwa Mussa Kawambo ambaye ni Mtangazaji na Mzalishaji wa Vipindi vya Michezo wa Azam TV na Uhai FM Redio. Nadhani jina lake lilirukwa lakini acha likae kwenye *record* zetu kwamba alikuwepo.

Waheshimiwa Wabunge, watakaoanza mchana ni Mheshimiwa Ally Saleh, Mheshimiwa Oscar Mkasa na Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda na wengine watafuata baada ya hapo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sina la ziada, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge niliwataja wachangiaji wetu tutakaoanza nao jioni hii, Mheshimiwa Ally Saleh atafuatiwa na Mheshimiwa Oscar Mukasa na Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda ajiandae.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa leo nitachangia hoja moja tu na nitaanza kwa kusoma shairi ambalo nimeliita jina la "Dhima", linasema hivi: *"Dhima ipuuzwapo, dhahiri ikawa, husuda ikaongoza, hutia nyoo doa, awaye yeyote kuwa, ajipaye mno madaraka, izara jadidi itamkuta, iwe leo ama kesho. Fundo za majigambo, fitna kwa jamii zitamrudi. Ubinadamu ni ukosefu, ujue sijibereuze."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kuanza na shairi hili kwa sababu naamini, au kwa kiasi kikubwa nitazungumzia juu ya dhima katika lengo la utawala au katika lengo la Taifa. Neno "dhima" nitalielezea huko mbele, lakini linaanzia na kupewa ridhaa ya kuongoza nchi au kukamata dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi Vyama vya Siasa hufikiri kwamba wakipewa ridhaa maana yake ndiyo mwisho wa kila kitu, kwa maana wanaona uchanguzi ndio unamaliza kila kitu. Uchaguzi au kushinda uchaguzi au kupewa kushika dola ni sehemu ndogo sana ya wajibu wa chama ambacho kipo maradakani. Siyo *free hander* kama wanaweza kufanya chochote, kile lazima kuna maeneo ambayo wanatakiwa wayatazame katika hali nzuri. Huanza kwa kujenga dhana ya kuongoza na siyo kutawala. Kwa ninavyoona mimi, hapa nchini kwetu CCM inatawala na siyo kuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatawala kwa sababu namna wanavyoendesha nchi haikisi *human face*, haikishi kufungua *public space*. Nitaelezea huko mbele namna wanavyobana *public space.* Kwa hiyo, kutawala na kuongoza ni mbingu na ardhi, lakini Kwa CCM tunaona inatawala na siyo kuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunaambiwa kuna maendeleo yanafanywa *in fact* kila mtu anakubali maendeleo ni jambo nzuri; iwe *Stiegler's, Standard gauge*, ndege, barabara, madaraja, *flyovers* na madubwasha mengine yoyote mengine ambayo tunaletewa kama maendeleo. Sehemu ya binadamu ina mbili, ina vitu vya kukamata na ina vitu vipo rohoni. Sasa huwezi kumjazia mtu ukamwambia kwamba kwa kuwa nakuletea ndege, nakujenga daraja, kwa hiyo umnyime haki zake zile ambazo kama binadamu angetaka awe nazo; ku-*enjoy public space,* lakini pia ku-*enjoy* vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *studies* nyingi zimeonyesha kwamba maendeleo ya vitu siyo maendeleo ya binadamu, lazima kuwa na uhuru wa wananchi kwenye

kujikusanya, kwenye maoni, kwenye kujieleza na maeneo mengine. Kwa hiyo, maendeleo bila vitu hivyo, siyo maendeleo kitu. Sasa ili kupewa ridhaa, lazima kuwa na dhima kama chama ambacho kinataka kutawala katika Taifa. Ridhaa ni jambo muhimu sana kwa sababu ndilo ambalo linasimamia vitu vingi. Ni kwamba ukipewa dhima maana yake uendeshe nchi kwa usawa, haki, imani na uadilifu. Bila vitu hivyo basi unakuwa unatawala na huongozi na CCM inatawala, haiongozi, kwa sababu inakosa vitu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuongoza nchi siyo utashi, siyo utakavyo, siyo upendevyo, siyo vyovyote vile, lazima uendeshe nchi kisheria na kikatiba. Hilo kusema kweli linaonekana lina doa katika utawala wa CCM ambao tunakwenda nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, raia wote wanatakiwa wawe na haki sawa wasibaguliwe kidini, kisiasa na kila kitu. Katika hilo tunaliona, raia wa Tanzania hawakuwekwa katika hali sawa. Sasa Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inatakiwa iakisi uendeshaji wa Serikali. Ningetamani Ofisi ya Waziri Mkuu katika bajeti kama hii au katika uendeshaji wa nchi tungeona ina-*reflect* kwamba inagomba, inakataza, inasimamia kwa wivu kabisa juu ya suala la haki, usawa, imani na uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa CCM inatawala, haingozi, hayo hayaonekani. Nataka nim-*quote* msanii Idrisa Sultan, aliandika juzi katika *twitter,* ilikuwa ni suala hili la kutaka suala la *CAG*, akasema yeye anasaini katika watu 15,000 waliosaini juu suala la *CAG* kwamba Bunge libatilishe maamuzi yake kwamba akasema nasaini kwa sababu nina wivu na kesho, nataka nione Tanzania ya kesho inatengenezwa. Kwa hiyo, Bunge hili pia au Wizara hii ilipaswa ione kesho yetu sisi kama binadamu, ione kesho ya watoto wetu, ione kesho ya wajukuu zetu na ione kesho ya vitukuu vyetu.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimwa anayechangia akitaja sana CCM, lakini nilitaka nimwulize kama anapochangia hapo anasimama kama *CUF* au *ACT?* Pili, kama ni *CUF,* anajua kwamba Maalim Seif amekuwa kiongozi Mkuu wa *CUF* kwa miaka mingapi? Kwa sababu mimi nakumbuka alianza sijui ni enzi ya Mheshimiwa Mwinyi, Mheshimiwa Mkapa, Mheshimiwa Dkt. Kikwete na sasa Mheshimiwa Dkt. Magufuli yupo, sasa anamanisha nini anapozungumzia uongozi na utawala? Ni wapi kuna utawala? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naendelea tu. Nimesema CCM inatawala na haiongozi kwa sababu nina *reasons;* na *reasons* zangu siyo za leo, zimekuja kwa muda mwingi sasa. Nitataja mfano, kwa jambo moja tu. CCM katika ilani yake imesema kwamba itakuza vijana ambao wamepata mimba wakati wakiwa shule. Kinyume na Ilani na Sera yake, CCM imebadilika, kwa sababu haina *culture* ya kuongoza, *culture* yake ni ya kutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita tu, chama cha CCM kimefanya mkutano wa ndani Sikonge, tumeona mamia ya watu wamekaa, wamefanya mkutano lakini Serikali hiyo haijawazuia kufanya mkutano. Chama hicho cha CCM kimefanya mkutano *NIT,* wiki hii iliyopita lakini hatuona kuzuiwa. Vyama vingine, iwe CHADEMA, iwe *ACT* au *CUF* wakifanya vitu kama hivyo wanazuiliwa. Kwa hiyo, mimi najiuliza, hii Ofisi ya Waziri Mkuu inafanya kitu gani katika kutazama masuala ya kila siku ambapo uhuru wa siasa unaminywa kila siku? Ambapo kila siku uhuru wa kujieleza unazidi kupungua? Ambapo kila siku watu wanapotea, watu

wanatekwa, lakini hatukuona uongozi wowote kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukiukwaji wa haki za binadamu umekuwa mkubwa nchi hii mpaka juzi Rais Mheshimiwa Dkt. Magufuli akaingilia, mtu ambaye amebambikiziwa makosa na alikuwa ameshakaa kifungoni kwa muda mrefu. Polisi wanazuia vyama vingine kufanya mikutano, tunafika hata maandamano ya amani tunayaogopa. Hivi sasa katika mtandao kuna kikundi kesho kinataka kuandamana kwa ajili ya kueleza hisia zao juu ya kukiukwa Katiba au tishio la kukiuka Katiba uhusiana na *CAG*, lakini wamezuiliwa wasifanye. Hata maandano ya amani yanakataliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Wapinzani kuporwa Wabunge wao. Pia tunaona kwamba hata suala la Tanzania katika nyanja ya Kimataifa kwenye mikataba ya Kimataifa ya haki za kibidamu ya utawala bora inajitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Bunge haliruhusiwi kuonekana wananchi. Sasa ningetamani Ofisi ya Waziri iakisi katika kuisaidia Serikali kuendesha nchi hii kwa hali ya *good faith* na *public space* ili wananchi...

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa. Mheshimiwa Ally Saleh unapewa taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Ally Saleh kwamba jana Tarime Mjini, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa John Heche walikuwa na Mkutano wa Hadhara. Kwa hiyo, unaposema mikutano inazuiwa, mimi sikuelewi, maana jana walikuwa na mkutano wao na hawazuiliwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Asubuhi Mheshimiwa Gekul alizungumza kwamba alikuwa upande Gaza, naona bado ana Gaza *syndrome* ndani ya kichwa chake. Hatuzungumzii *individual cases* na hao ambao wamefanya mkutano baada ya msukosuko. Kwa nini iwe msukosuko wakati ni haki ya kikatiba? Kwa mfano, kufanya mkutano ni haki ya kikatiba, kwa nini uzuiliwe? *That is the question,* siyo kwamba amepewa mtu mmoja ameonjeshwa ndiyo tuseme kwamba ndiyo *general rule,* tunataka tuhakikishe...

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kumpa taarifa mzungumzaji, hivi ninavyoongea sasa hivi, viongozi wa Tarime Jimbo CHADEMA na Mkoa wameshikiliwa na Polisi na wanahojiwa kwa nini walienda kumsindikiza Mbunge wa Chama chao kufanya mkutano jana Tarime? Kwa hiyo, nakupa taarifa. *(Makofi)*

**MHE. ALLY S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa inapokelewa kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kusema kwamba *we need to change* kama Taifa. Sote...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa kaka yangu Mheshimiwa

Ally Saleh kwamba watu wanazuiliwa mikutano na maandamano kwa kutokuwa na nidhamu. Kwa mfano, jana mkkutano wanaozungumza wapo watu ambao wamemsindikiza Mheshimwa Esther Matiko ambao kimsingi sio Wabunge lakini walikuwa wakimtukana Mheshimiwa Rais kwenye mkutano ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Esther Matiko mwenyewe kwenye mkutano wake alikuwa anamtuhumu Hakimu aliyeshughulikia kesi kule Mahakamani akamweka ndani na kwamba amepewa dhamana. Sasa katika mazungumzo kama hayo sheria inakataza. Ni lazima Serikali ingalie utaratibu ulivyo. Ukizuiliwa maana yake hukwenda vizuri. Ukiomba mkutano, ukazungumza mambo yanayopaswa, hakuna ugomvi na Serikali wala vyombo vya dola. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE.ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba mambo yanayopaswa siyo mambo ambayo Serikali inayataka, ni yale ambayo kwa uhuru tulionao chini ya Katiba na chini ya Sheria tuna haki ya kusema. Huwezi kumzuia mtu kusema. Kama unamwona ana makosa, mpeleke Mahakamani, siyo umzuilie kusema, siyo utumie utaratibu wa intelijensia kwa vyama vingine lakini vyama vingine unakuwa una madudu kichwani. Lazima tuhakikishe kwamba kama intelejinsia inaonyesha kwamba watu watafanya fujo, basi jukumu la Polisi ni kuwakamata hao ambao wanataka kufanya fujo na siyo kuwazuia wale ambao wana haki ya kukutana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda na Mheshimiwa Hassan wajiandae.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana. Awali ya yote namshukuru Mwenyenzi Mungu

kwa kuturuhusu kufanya hii shughuli leo, lakini nitumie fursa hii kuendelea kuwashukuru wananchi wa Biharamulo kwa kuendelea kunipa imani na kunivumilia kwenye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka niipongeze Serikali, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayofanya, lakini kwa maana ya bajeti hii, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi anayoifanya, Mheshimiwa Jenister, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Manaibu wao; Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Ikupa, hongereni sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia mambo mawili; Sekta ya Afya kama iliyoelezwa kwenye kitabu cha hotuba ukurasa 56 mpaka 62, lakini nitagusia kidogo suala la UKIMWI na mwishoni nitaja mambo mawili matatu yanayohusu Biharamulo mahususi ambayo mengine ni dharura na mengine ambayo yamekuwa yanatusumbua kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 56 mpaka 62 wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu, kinaongelea Sekta ya Afya na kuna mahali kinasema vizuri kabisa kuhusu mafanikio ambayo nimeyapongeza na ninaendelea kuyapongeza. Kwa mfano, miundombinu ya huduma za afya kumeongeza vituo vya tiba kutoka vituo 7,678 mpaka vituo 8,119. Maana yake ni kwamba tunaendelea kupeleka huduma za afya kwenye maeneo ambayo zinaweza kutolewa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu kwenye hilo, twende mbali zaidi. Ukisoma ukurasa huo wa 56 mpaka 62 ingawa kichwa cha habari kinasema “Afya”, lakini kwa kiwango kikubwa tumejikita kwenye tiba, ambapo tiba tunaihitaji, lakini tunahitaji sana kwenda kwenye afya kwa ujumla. Afya inaanzia kwenye kuzuia/kukinga lakini kuelimisha watu ili hata hayo mahitaji ya Vituo vya Afya na vifaa tiba, hata kama yanaongezeka yasiendelee kuongeza kwa kasi, ifikie mahali sasa tunashughulika na tiba kwa wale ambao wanaumwa, lakini kwa kiwango kikubwa tunazuia watu

wasiugue. Kwa namna hiyo tutakuwa tunatumia zaidi pesa yetu inayozalishwa na sekta nyingine za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia hapa kitabu cha ikama ya Wizara ya Afya wanaita *Staffing Level for Ministry of Health and Social Welfare* kwa 2014 - 2019 ndiyo kinatumika mpaka sasa. Wameweka pale *Staffing Level* kwa ngazi ya zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukiangalia pale, karibu asilimia 80 ya watumishi ambao wamewekwa pale kwenye Kituo cha Afya ni watumishi wa tiba. Mtumishi wa Kinga ni mmoja tu, wanamwita *Community Health Worker or Social Welfair Assistant* ambapo hao wengi wote wa tiba wanaelekezwa kabisa, kwa mfano, *Clinical Officer* anaambiwa kwa siku ataona wangonjwa 40, Mphamasia anaambiwa kwa siku atafanya *prescription* 40 na Nesi anaambiwa kwa siku ataona wagonjwa 30. Huyu mtu, *Community Health Worker* kazi yake anaambiwa *to link person between community and the dispensary.* Hata ile dhana ya kwamba sasa huyu naye anapaswa tumwekee kipimo kwamba kwa siku atatembelea nyumba kadhaa ahakikishe kuna sehemu ya kunawa mikono, kaya zina vyoo na mambo kama hayo ili nguvu yetu iwe kwenye kinga zaidi kuliko tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Afya ili iweze kuleta majibu kwa maana ya afya kwa ujumla, mapendekezo yangu ni kwamba sasa taratibu tuanze kuondoka kwenye kuwekeza tiba peke yake, tuanze kwenye kinga. Nafahamu kwenye upande wa kinga, kwa mfano, upande wa chanjo tunafanya vizuri sana. Tanzania ni moja ya nchi ambazo zimeshafika zaidi ya asilimia 95 kwenye kuchanjwa watoto wetu. Vile vile kuna kinga za magonjwa mengine kama ya kuhara, magonjwa mengine ambayo yanasabishwa na tabia tu za wananchi kule vijijini, hatujawekeza vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ule mzigo wa magonjwa kwenye zahanati zetu, ukiangalia *burden of*

*diseases profile,* utakuta kuna sehemu kubwa ni magonjwa ya kuambukiza ambayo yanazuilika. Malaria ni wazi hilo ni tatizo la Kitaifa, lakini unakuta magonjwa ya kuhara kwenye zahanati yanachukua namba mbili ama namba tatu.

Kwa hiyo, mzigo ni mkubwa sana, ni magonjwa ambayo ukielimisha watu tu kidogo, akanawa mikono kabla kula, akanawa mikono baada ya kula, akahakikisha kuna choo kizuri, ule mzigo utapungua na ile nguvu ya pesa tutaipeleka kwenye maeneo mengine ambayo ni ya uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee UKIMWI. Tuna tatizo mpaka sasa kwamba asilimia 93 ya pesa ya mwitikio wa UKIMWI kwenye nchi hii ni kutoka kwa wafadhili. Tumesikia hivi karibuni, wametanga wenzetu Wamarekani kwamba asilimia 23 ya fedha hiyo inaondoka kwa mwaka huu. Ambapo ukiipeleka kwenye thamani ya fedha Kitanzania ni shilingi bilioni 282. Ni fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vizuri tuendelee kuwa tegemezi, lakini namna nzuri ya kujitoa kwenye utegemezi ni kuanza kuwekeza kwenye mfuko wetu wenyewe, Mfuko wa *AIDs Trust Fund.* Uwezo huo tunao na mifano tunayo, tumefanya hivyo kwenye *REA,* tumefanya hivyo kwenye maeneo mengine, tutafute namna kukanza kusimama...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji kwamba badala ya kuongeza bajeti kwenye UKIMWI ashauri wananchi waache uasherati. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa naiachia kiti, kitaona inaendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mifano kwamba Tanzania kwenye baadhi ya maeneo tumeendelea kusimama wenyewe na jambo hili la UKIMWI ni jambo ambalo linatoa *platform*, ni jambo mtambuka ambalo linasababisha magonjwa mengine yote ikiwemo *TB*, *Hepatitis* hata Kisukari sasa hivi, mtu ambaye ana tatizo la upungufu wa kinga, anakuwa kwenye hatari kubwa zaidi ya kufariki kutokana na magonjwa mengine kwa sababu ya kuwa na upungufu wa kinga. Jambo ambalo linahusu maisha yetu tena kwa upana huo ni vizuri sana na ni muhimu sana Serikali ikafahamu kwamba tuanze sasa kutafuta namna ya kusimama wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo matatu ya Biharamulo; moja jana jioni Askari wa SUMA JKT wamemuua mwananchi mmoja wa Kijiji wa Mavota kwa tuhuma kwamba aliingia kwenye eneo ambalo hapaswi kuingia. Naomba Serikali, Waziri wa Nishati kama yuko hapa, Waziri wa Ulinzi watusaidie kuangalia hali kama hii, kama inaanza kujitokeza tena, ni kweli hatuwaambii wananchi wetu wavunje sharia, lakini taratibu za kuwadhibiti pale ambapo wanaonekana wamevunja sheria zinafahamika. Huko nyuma jambo hili lilikuwa kubwa sana, tukalikabili likawa limeisha, lakini sasa inaonekana linataka kurudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee habari ya ulinzi na usalama Biharamulo; jana na wiki kadhaa zilizopita yameanza kurudi matukio kwa kasi ya majambazi kuvamia maduka, majambazi kuteka magari, jambo ambalo lilikuwa linatuathiri siku za nyuma kwa sababu ya sisi kuwa mpakani na nchi jirani ambazo zina watu wanaoingia bila utaratibu likawa limedhibitiwa kwa kiwango kikubwa hasa kwa kuweka kikosi maalum pale Nyakanazi, lakini kwa wiki chache zilizopita inaonekana ile hali ya zamani ambayo ni mbaya inaanza kurudi kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali waangalie jambo hili kwa sababu wananchi wa Biharamulo sasa hali kama ile inavyojirudia kwa kiwango kikubwa, tunashindwa kufanya shughuli zetu za uchumi, tunaishia nguvu zetu zote kuweka kwenye mambo ya kiusalama. Kuna migogoro ya Jeshi na Vijiji, Kijiji cha Rusabya, Kabukome na Kalebezo, nimesikia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi asubuhi analiongelea kwa ujumla, lakini ujumla huo, umekuwa unachukua muda mrefu sana. Tunaomba Serikali, hizo Wizara zimepewa kazi ya kwenda kutazama, hebu tumalize kazi hiyo, kwa sababu kule wananchi kule wamesimama hawafanyi shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kwa mara nyingine nampongeza Waziri Mkuu na timu yake, kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mukasa kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Masala na Mheshimiwa Zacharia Issaay ajiandae.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi kwanza kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba muhimu sana katika kipindi hiki cha bajeti. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ndiye aliyetuwezesha leo kutupa mazingira haya leo tunachangia hii bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze na pongezi za dhati kabisa, kwa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Dkt. John Pombe Magufuli, jamani kazi inafanya. Pongezi pia kwa Waziri Mkuu na Mawaziri walioko katika Wizara yake, lakini vilevile na Manaibu Waziri, pongezi za dhati vilevile ziwafikie Wakurugenzi, Mkurugenzi wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS)* na Mamlaka ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya. Kamishna Siang'i anafanya kazi ya kujituma sana, mpaka tumefikia hali tulivyo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yangu itakuwa mifupi sana leo, nitazungumzia hotuba hii ya Waziri Mkuu, kipengele cha 87 na 88 kinazungumzia huduma za kiuchumi. Wote tunajua humu tunapozungumzia uchumi, tunazungumzia Watanzania ambao wengi wako vijijini na wanategemea ardhi. Niipongeze Serikali hii kwa mara nyingine tena, katika Wilaya ya Malinyi, Wilaya ya Kilombero na Ulanga, tuna mradi wa urasimishaji wa ardhi ambao unatuwezesha kupima, kupanga namna gani tutatumia ardhi yetu na mwishoni kuwakabidhi wananchi hati za umiliki. Hili limesaidia kwa kiasi kikubwa sana kuondoa migogoro ya ardhi ambayo inatuweka sasa kwa msingi wa ardhi namna gani tunaweza kuwekeza kuunga mkono jitihada za Dkt. John Pombe Magufuli katika suala la uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye ardhi kwenye kipengele cha 89, Serikali imeeleza wanatekeleza agizo la Mheshimiwa Rais, tarehe 15 Januari mwaka huu Mheshimiwa Rais kama alivyo kwa tabia yake mjasiri, anathubutu ni kweli, amethubutu kusimamisha zoezi la kufuta vijiji 364 katika nchi hii. Wananchi hawa, miongoni mwa hivyo vijiji 364, vingine vipo katika Wilaya ya Malinyi, wamejikuta wao ni wahanga wa mabadiliko ya Sheria ya Wanyamapori ya 2009. Sheria ya zamani ilikuwa imenyamaza haikusema lolote hasa katika mapori tengefu na ndio matokeo yake kwamba vijiji vimesajiliwa ndani ya mapori tengefu na wananchi wameruhusiwa shughuli za kawaida za maisha yao, pamoja na kilimo, uvuvi na ufugaji, sasa 2009, tukabadilisha ile Sheria, imekataza, lakini wananchi hao tayari wako ndani ya hifadhi na wako ndani ya yale mapori tengefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa Watendaji wa Serikali hasa hawa wa Wanyamapori wamekuwa *too machinery,* wamekuwa wanafanya kazi kimashine mno, huwezi kuangalia mazingira yale unawaambia wananchi wale watoke vile vijiji 364. Huu msiba kwa kweli ungekuwa mkubwa sana. Bado migogoro inaendelea, pamoja na Rais ametumia busara ameonyesha ujasiri wake, ameunda Tume ya Mawaziri nane, wamezunguka Mawaziri wale watachukua na michango ya wataalamu, rai yangu ya mwisho kwa suala

hili, upande wa kule Malinyi lile Bonde la Kilombero, tuna dhamira ya kweli na tunataka kulilinda, wananchi wale wanachogombania ni kiasi kidogo sana, ile *buffer zone,* eneo lile la Pori Tengefu la Kilombero ni ina *range* kati ya kilomita nane mpaka kilomita 23, wananchi hao wanataka kidogo tu wapewe angalau kilomita tatu ndiyo mashamba yao yamo mle. Ndiyo maana nasisitiza nashauri tena Serikali, hili zoezi wanaloendelea nalo la kurejea mipaka wawaachie mashamba yale wananchi, hayo ndiyo maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uchumi, vilevile linaendana na suala la barabara, Serikali imeonesha dhamira yake na tumeiona barabara inayounganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Ruvuma. Hii barabara inaanzia Mikumi, Ifakara, Lupilo, Malinyi, Kilosa Mpepo, Londo, Lumecha mpaka inaingia Songea. Barabara hii sasa imetoboka toka 2017, lakini ombi langu toka itoboke ile barabara haiwezi kutumika kwa sababu bado ina maeneo korofi katika bajeti hii, sijaona dhamira ya kweli kabisa kurekebisha ile barabara ili yale maeneo korofi angalau ipitike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiikamilisha barabara hii sasa tutakuwa tumekamilisha dhana na Sera ya barabara kwamba iunganishe Mkoa kwa Mkoa, nitachangia zaidi itakapofika kwenye Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo hapa ninachoomba, Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili suala la barabara ya kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Ruvuma ni muhimu sana kwa maendeleo sio tu hii Mikoa miwili, lakini kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kama nilivyosema nitachangia ni suala la Tume ya Udhibiti UKIMWI. Ndugu yangu hapa Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI ameshagusia, lakini naomba nisisitize zaidi, jamani, suala la UKIMWI, takwimu zinatuonesha kwamba linapungua, lakini kihali halisi bado tatizo ni kubwa. Sasa naomba tuungane wote kwa pamoja na ule mkakati ambao unasema 90 kwa 90 kwa 90, nini maana yake 90 kwa 90 kwa 90? Ni kwamba asilimia 90 wanaokadiriwa wanaishi na Virusi vya UKIMWI wao

wamepima na 90 ya pili ni kwamba wale ambao wamegundulika wanaishi na Virusi vya UKIMWI baada ya kupimwa, waingie kwenye matibabu na asilimia 90 yao wanaendelea na matibabu na 90 ya tatu wale ambao wanaendelea na matibabu ya *ARV's* asilimia 90 yao wao wamefubaza Virusi vya UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo mkakati ambao unaweza ukatokomeza suala la UKIMWI, nini maana yake, ile 90 ya mwisho maana yake ni kwamba kama mtu umefubaza Virusi vya UKIMWI unakuwekea mazingira wewe huwezi kumwambukiza mwenza wako unayeshea naye kama yeye hajaambukizwa na halikadhalika na yeye hawezi kuambukizwa na Virusi vya UKIMWI kama yule mwenza anatumia *ARV's.* Sasa changamoto iliyopo Tanzania hatuna rekodi nzuri katika ile 90, 90, 90 na mkakati huu mwisho 2020 ni mwaka kesho. Sasa hii 90 ya kwanza ndio tuko asilimia 61, najiuliza asilimia 61 leo, 2019 mkakati unasema 2020 tuwe tumefikia asilimia 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kuna changamoto, tunaiomba Serikali, Kamati ya UKIMWI wamependekeza mara nyingi, tunaiomba Serikali labda isikie kwamba vitu ambavyo vinachangia navyo hii 90 ya kwanza ni suala la Sheria ya UKIMWI. Sheria ya UKIMWI haimruhusu mtoto chini ya miaka 18 kwenda kupima bila ridhaa ya mzazi au mlezi ambapo hawa watoto wa miaka 18 na takwimu zinaonesha waathirika wengi, *survey* iliyofanywa mwaka 2017 ilionyesha asilimia 40 ya waathirika wa Virusi vya UKIMWI ni vijana wenye umri kuanzia miaka 15 mpaka miaka 24, ndiyo hao tunazungumza wengi wao hawaruhusiwi kwenda kupima kwa hiari yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama mtu ataenda kupima yeye mwenyewe, kwa hiyo tukiongeza idadi ya watu kupima Virusi vya UKIMWI, tunaongeza ile 90 ya kwanza. Sasa hili suala ni la kisheria tumeiomba mara nyingi Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Serikali wamekuwa wana-*dill dull* suala hili hawalileti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako Dkt. Tunaendelea, Mheshimiwa Hassan Masala, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Issaay na Mheshimiwa Vicky Kamata ajiandae.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Niungane na wenzangu waliochangia kwa kutoa pongezi kwa mawasilisho yaliyofanywa, lakini pia kwa upekee kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Wasaidizi wake wote ambao wanamsaidia majukumu ya kutekeleza mambo mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha tunawatumikia Watanzania ambao wametupa ridhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo bado pia naomba nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, takribani siku nne sasa amefanya ziara ndani ya maeneo ya Kanda ya Kusini. Wote mtakuwa mashahidi amefika Mkoa wa Mtwara na kwa muda mrefu sana, sisi wananchi tunaotoka katika ukanda huo tulikuwa na hamu kubwa sana ya kumwona Mheshimiwa Rais anakuja kule. Ujio wake kwetu umekwenda kutupa faraja kubwa sana, yako maelekezo mengi ambayo Mheshimiwa Rais ameyatoa kwa ajili ya kuhakikisha Watanzania wanapata zile huduma zote muhimu, lakini hapa kubwa ambalo ningependa nipongeze ni suala zima linalohusiana na korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara ni sehemu ya uchumi wetu, ni sehemu ya maisha,

lakini ni sehemu ya changamoto ambazo kwa wakati fulani kidogo tulipitia. Hata hivyo, kupitia ziara aliyoifanya ameenda kutuachia faraja kubwa sana na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nachingwea na kwa niaba ya wananchi ambao wanalima korosho tutakuwa watovu wa fadhila kama hatutathamini na kupongeza kile ambacho Mheshimiwa Rais amekielekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu yeye ndiye msaidizi, tunaomba atufikishie salamu hizi kwa Mheshimiwa Rais na Watendaji wake wote wakiwemo Mawaziri wa Kilimo, ambao walichukua mawazo yetu na waliyafanyia kazi yale ambayo sisi tuliyashauri kwa niaba ya wananchi ambao wametupa nafasi ya kuwepo katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ukurasa wa 27 mpaka 30 kwa sehemu kubwa wamezungumzia suala zima linalohusu kilimo. Ningependa nizungumzie zaidi kwenye eneo la kilimo kwenye namna bora ambayo tutakwenda kujipanga wakati tunaelekea kwenye msimu ujao hasa katika zao hili la korosho, ambalo ndilo hasa linalotuletea uchumi na ndilo ambalo hasa linatuletea kipato kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tulizozipitia sehemu kubwa ili tuweze kuzirekebisha yako mambo ambayo ningependa nishauri kupitia hotuba ambayo imetolewa. Jambo la kwanza ni suala zima la kuhakikisha wakati tunajiandaa na msimu mpya wa 2019/2020, tuone namna gani ambavyo tunaweza kwenda kusambaza pembejeo za kutosha hasa *sulfur* pamoja viuatilifu vingine ambavyo tumekuwa tunavitumia katika kufanya uzalishaji. Jambo hili na kupitia Serikali yetu, naamini iko dhamira ya dhati kabisa ambayo tayari imeshaonekana hasa katika msimu uliopita wa 2018/2019, lakini zipo changamoto ambazo tungependa awamu hii wakati tunajiandaa tungeona mabadiliko makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mfumo uliotumika 2017/2018 wa kutoa pembejeo bure au karibu na bure au kuleta pembejeo ya ruzuku, ningependa kushauri watu wanaohusika ili waweze kuona namna sasa tunavyoweza kwenda kupata hizi pembejeo ili wakulima wetu waongeze uzalishaji katika zao hili la korosho ambalo kwa muda kidogo sasa ni kama hatufanyi vizuri sana kwenye uzalishaji. Kwa hiyo pendekezo langu kubwa ambalo ningependa kulitoa ni hilo kwa wale ambao wanahusika na zoezi hili la utoaji wa pembejeo na hasa ukizingatia katika hotuba hii suala la kilimo pia limegusiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado pia tunahitaji tuone maandalizi ya haraka sana, tuone namna ambavyo wadau wanaohusika na zao la korosho wanavyoweza kukutana na kuanza kufanya tathmini ya changamoto ambazo tumezipitia katika msimu. Ziko hoja za masoko, lakini pia ziko hoja zinazohusiana na namna bora ya kuendesha msimu kupitia Vyama vyetu vya Ushirika. Niwaombe watu wanaohusika waweze kupanga ratiba za haraka, lakini pia waweke katika kalenda za vikao tuweze kukutana mapema, tuweze kujadiliana yale yote ambayo mwaka huu yamejitokeza katika huu msimu, basi tuhakikishe msimu ujao wa 2019/2020, mambo haya machache ambayo yamejitokeza hayatojirudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala kubwa ambalo limezungumzwa kwa muda mrefu sana kuhusiana na korosho suala zima la *kangomba, kangomba* ime-*trend* sana, imezungumzwa sana, lakini yako maelezo ambayo sisi tunashukuru kupitia hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu na kupitia Bunge lako, tungependa sasa tushauri ili tuepukane na *kangomba* kwa kadri ya maelekezo yaliyotolewa. Yako mambo ya msingi ambayo yakifanyika tunaamini suala la kangomba msimu ujao, na maelekezo yaliyotolewa halitojirudia na kubwa ni hili la kupeleka pembejeo, kwa sababu *sulfur* zinavyokosekana hili limechochea wakulima wetu kuingia katika majaribu ya kuwapa wafanyabiashara korosho zao ili waweze kuhudumia mikorosho yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ili kuliepuka hili na kuwaepushia wakulima adha walioipata safari hii, basi ni vizuri sana tukaona namna ya kutengeneza hayo mazingira wezeshi ya kupanga vikao, ya kupanga bei, lakini pia ya kutoa pembejeo kwa wakati na kwa gharama nafuu ambazo zitaepusha wakulima kukutana na wafanyabiashara au watu ambao hawana nia nzuri ya kuwasaidia wakulima ambao kwa muda mrefu wamekuwa wanapata changamoto katika uzalishaji wa zao hili la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaishukuru sana Serikali kwa namna na nia njema waliyoonesha katika kuendelea kufungua na kuboresha Viwanda vya Kubangua zao la Korosho. Juzi Mheshimiwa Rais akiwa Newala kule Tandahimba amezindua na kuona Kiwanda kile cha lyuri, lakini bado tuna maeneo mengine ambako kuna Viwanda ambavyo vilikufa na tayari Serikali imeshaonesha nia ya kuvirejesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nachingwea tunacho Kiwanda cha Mamlaka ya Korosho, bado Kiwanda kile kinacho uwezo mkubwa wa kuweza kuzalisha na tayari wapembuzi wameshafanya kazi ya kukikagua ili waweze kuona namna ya kukirejesha, lakini bado Mtama kuna Kiwanda na Lindi Mjini bado kiko Kiwanda ambavyo hivi vyote vikitengenezewa mazingira mazuri azma ya kubangua korosho ndani ya maeneo yetu itakuwa ni kubwa na hivyo tutaenda kuongeza thamani ya zao la korosho na pia tutaenda kuongeza ajira kwa vijana wetu na kuboresha mfumo mzima wa upatikanaji wa korosho katika mazingira yetu. Kwa hiyo, haya niliona niyazungumze kama sehemu ya mapendekezo ambayo ningependa Serikali iyachukue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nizungumzie ni suala zima la zao la mbaazi, bado wakulima wetu sisi ni wazalishaji wakubwa wa zao la mbaazi. Hapa tunapozungumza tuko kwenye msimu wa maandalizi, naomba kupitia Wizara ya Kilimo, ambayo iko chini ya Ofisi pia ya Waziri Mkuu na kwenye hotuba imezungumziwa, waone namna wanavyojipanga katika kuhakikisha

hatuyumbi tena katika upatikanaji wa masoko hasa wa zao hili ambalo kwetu sisi ni muhimu sana na linazalishwa kwa wingi sana. Miaka mitatu iliyopita zao la mbaazi hatujafanya vizuri, kwa hiyo naamini wakati tunaelekea kwenye kuhitimisha hizi bajeti basi, tutapata maelekezo mazuri ya namna ambavyo tunajiandaa kwenda kununua zao la mbaazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba nizungumzie suala zima la miundombinu, Jimbo la Nachingwea, Jimbo la Liwale, Jimbo la Masasi kwa sehemu kubwa ndiyo wazalishaji lakini pia miundombinu yake sio rafiki sana. Naipongeza Serikali kwa sababu imeonesha nia ya dhati ya kujenga barabara ya lami kutoka Masasi kwenda Nachingwea, Nachingwea kwenda Ruangwa, Ruangwa kwenda Nanganga na tayari utaratibu wa kuitangaza hii barabara kwa ajili ya kupata mkandarasi ulishafanyika. Hata hivyo, mpaka sasa hivi ninavyozungumza bado sijaona taratibu zozote ambazo zinaendelea, kwa hiyo wakati tunaendelea kutaka kupitisha bajeti hii, niwaombe sana watu wanaohusika watoe maelekezo ya kina ya namna ambavyo wamejipanga kuanza ujenzi wa barabara hii ambayo ina kilomita karibu mia moja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Masala.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zacharia Issaay atafuatiwa na Mheshimiwa Kamata na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuona siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa iliyofanya nchi nzima ikiwemo Jimbo la Mbulu Mji. Niseme tu kwa ujumla kazi zilizofanywa na Serikali hii ya Awamu ya Tano zipo katika ngazi mbalimbali na kwa nyakati tofauti. Watanzania wa leo wana masikio na macho na wanaona matokeo ambayo yanagusa zaidi maeneo ambayo pengine kwao yalikuwa tatizo kwa namna mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya afya ambayo ni muhimu sana lakini Serikali kwa jitihada mbalimbali imechukua hatua za makusudi kuboresha huduma ya afya kutoka kwenye miundombinu na huduma mbalimbali ikiwemo dawa na vifaa tiba lakini pia katika kila sekta kwa kazi hizi zimefanyika. Kwa namna ya pekee sana, tunampongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake lakini pia Baraza la Mawaziri kwa kuwa kila sekta imejaribu kufanya kazi. Nayazungumza haya kwa sababu yamefanyika katika Jimbo langu la Mbulu Mji na nchi nzima kwa ujumla kadri tulivyoona kwenye Kamati mbalimbali kwa kukagua miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwa uchache na umuhimu sana kuzungumzia eneo la ajira. Hali ni mbaya sana, tunaomba Serikali ifanye utafiti na ichukue hatua za makusudi kuona ni kwa namna gani vijana wote waliomaliza elimu yao katika vyuo mbalimbali wanaweza kutoa mchango wao kwa Taifa letu. Kadri nafsi za ajira zinavyokuwa chache basi sekta hii ambayo tunaiita ni sekta binafsi ina nafasi kubwa ya kuchukua vijana wetu ambao wamehitimu. Tatizo tulilonalo ni kwamba vijana wengi wanakosa nafasi ya kufikiri kwamba sekta binafsi inaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuwapatia Watanzania ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili ili kwa namna mbalimbali tutazame sheria za ajira na upungufu uliopo kwenye sekta binafsi katika suala la ajira kwa vijana. Vijana wengi wanaogopa kuajiriwa na sekta binafsi kutokana na

mtazamo wao uliojijenga kwamba Serikali itawaajiri, kwa hiyo, sekta binafsi inaogopwa. Kwa hivyo, ni jukumu la Serikali kutazama upya suala la ajira pamoja na mazingira ya kustaafu kwani ndiyo yanaifanya jamii na vijana kuona kwamba wakiajiriwa katika sekta binafsi hawatakuwa sawa na wale walioajiriwa katika sekta za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nayasema haya? Kila mtu hapa tulipo anaogopa kustaafu, hata Wabunge tunaogopa kustaafu kwa sababu mazingira ya kustaafu baadaye siyo mazuri, kila mtu ana hofu hatma yangu itakuwaje baadaye nikishastaafu. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia sheria na taratibu za ajira na mafao ya kustaafu katika sekta binafsi kwa sababu akiangalia kama baadaye akistaafu hali yake siyo nzuri, basi lazima kijana aanze kupata hofu na waweze kuogopa kuajiriwa katika sekta binafsi. Pengine haya yanatokana na mishahara midogo lakini pia mazingira ya kufanyia kazi yanakuwa siyo rafiki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali itazame pia shule zetu za sekondari na msingi ni namna gani tunabadilisha na kuingiza mitaala ya sekta za biashara, ajira na mafao baada ya kustaafu ili vijana wetu wasisome kwa dhamira au kwa nia ya kwamba hapo baadaye wataajiriwa na Serikali. Katika shule zetu za msingi lazima tuwe na mitaala ya kilimo na biashara na kufanya mambo haya kuwa rafiki kwa kijana wa Kitanzania. Sasa hivi vijana wana chuki kwetu sisi Wabunge wanaona kwamba hatuzungumzii suala zima la upungufu wa ajira katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uanzishwaji wa viwanda, tusipotafuta utaratibu na mazingira yanayoruhusu vijana waende kwenye ile hali ya kwenda kwenye viwanda, tutakujakuta tumeanzisha viwanda lakini vijana wetu hatukuwaandaa katika ile mitaala ya ajira kwenye sekta ya viwanda. Hii ni kwa sababu utakuta vijana wengi hawana mwamko wa kwenda vyuo vya ufundi, vyuo vya kati na vyuo vya ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapopata ajira kwenye viwanda au tunapoanzisha kiwanda tutajikuta kwamba vijana hawana uwezo na taaluma ya kuweza kujiingiza kwenye zile sekta za viwanda. Nadhani tutumie vizuri nafasi za Maafisa Vijana katika Halmashauri zetu na kuwe na *forum* za majadiliano katika ngazi ya wilaya na baadaye mkoa. Serikali ione utaratibu ambao utawezesha vijana kujadili masuala yao mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapungufu haya yanaweza kufanyiwa kazi na kuleta tija kwa sababu hata sasa sekta ya michezo hatujaitumia vizuri ikaonesha mchango wake katika ajira kwa Taifa letu. Nasema hivi kwa sababu kama ambavyo vijana wanafanya mazoezi ya mashindano ya shule za msingi na sekondari na mwisho mkoa, hakuna utaratibu wa kuwashika mkono kwa vile vipaji vyao vinapoibuliwa na kufika kwenye ngazi ya mkoa. Kwa sababu hiyo basi, tunayo sababu ya kuendeleza fursa zote zinazowagusa vijana ili waweze kujiendesha na kutambuliwa kupitia vile vipaji walivyozaliwa navyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunawaambia vijana waanzishe shughuli binafsi au wajiari, mazingira si rafiki sana kwa sababu kwanza hawana mitaji lakini hata akisema anaanzisha biashara uwezo wa kusimamia biashara hana kwa sababu yeye mwenyewe alitarajia aajiriwe Serikalini ama kwenye sekta fulani wakati anasoma, hakuwa amejiandaa kwa kujiajiri. Kujiajiri ni nafasi pana au namna ya kijana kujiajiri kunahitaji maandalizi toka mwanzo, amefanya mazoezi kama nchi nyingine huko duniani zinavyofanya kwamba anapokuwa na sura fulani basi anakuwa na nafasi ambayo ameifanyia mazoezi na mwisho wa siku akijiajiri ni *nature* aliyokuwa nayo toka mwanzo na hiyo inampeleka kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili pia naomba kuishauri Serikali, kuna taarifa isiyo rasmi inatembea ambayo inasema kauli ile ya Rais ya kubadilisha Kikokotoo siyo waraka wa Serikali. Kama kuna hiyo kauli na kuna watu wanaitumia hiyo *loophole* tunawaomba watambue kauli ya mwenye nchi

ni sheria, ni waraka huwa inatakiwa izingatiwe. Wastaafu wengi wanalalamikia jambo hili kwa maana ya kwamba bado hawajabadilishiwa, kwenye Jimbo langu kuna baadhi wamenipigia simu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Vicky Kamata, atafuatiwa na Mheshimiwa Rwamlaza na Mheshimiwa Zainab Bakar ajiandae.

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mungu kwa kututia nguvu na kutuvusha salama katika kipindi kigumu ambacho kilikuwa ni cha kuuguza na hatimaye kumpumzisha mahali pa milele mama yetu mpendwa Paulina. Nimshukuru pia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa upendo, huruma na utu wema aliotuonesha katika kipindi cha kuuguza na hata mpaka mama alipofariki na hata baada ya kumpumzisha katika nyumba ya milele ameendelea kutupa faraja mimi na kaka yangu kwa kutupa maneno ya imani ambayo yametupa nguvu hata tunaweza kuendelea kustahimili kuishi bila mama yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Rais Mstaafu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya pamoja na mama yetu mpenzi, Mheshimiwa mama Salma. Nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote, Wabunge, Spika, kaka yangu Rashid Shangazi pamoja na Joseph wa Faraja Fund. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana viongozi wote wa dini, madaktari wote wa Muhimbili na Bugando, wananchi wote wa Geita, wananzengo wenzangu wa Mbweni pamoja na Mpigi kwa faraja kubwa ambayo wametupa na Watanzania wote kwa pamoja ambao wameweza kutufariji na sasa tunaendele vizuri, tunamshukuru Mungu. Raha ya milele umpe ee Bwana na mwanga wa milele umwangazie. Apumzike kwa amani.

**WABUNGE FULANI:** Amina.

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu baada ya kuwa nimekipitia kitabu hiki vizuri na kwa kweli niipongeze sana Serikali kwa kuonesha dhamira ya dhati ya kutaka kututoa hapa tulipo na kutupeleka mbele zaidi kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitauanzia kwenye ukurasa wa 53. Ukurasa wa 53 unazungumzia mambo ya elimu bila malipo. Nitasoma kidogo: "Serikali inatekeleza kwa mafanikio makubwa mpango wa Elimumsingi bila malipo. Mpango huo una lengo la kuhakikisha kila mtoto wa Tanzania mwenye umri wa kwenda shule anapata haki ya kupata elimumsingi bila kikwazo cha ada na michango mingine.

Katika kipindi cha miaka mitatu, Serikali imetumia shilingi bilioni 711.22 kutekeleza mpango huu. Katika mwaka 2018/2019, Serikali tayari imetoa shilingi bilioni 166.44 hadi Februari, 2019, kwa ajili ya kutekeleza mpango wa Elimumsingi bila malipo hapa nchini. Utekelezaji wa mpango huo, umeongeza idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika shule za msingi na sekondari".

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kusema, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kubuni jambo hili ambalo ni muhimu na lenye tija kubwa sana kwa nchi yetu kwa ajili ya kizazi chetu cha leo na kijacho. Naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuwa kila jambo jema kubwa la namna hii linapokuwa linaanzwa kwa mara ya kwanza huwa halikosi changamoto mbalimbli na kwa kuwa mimi kama Mbunge kazi yangu ni kuishauri Serikali, napenda nishauri machache kwenye elimu bila malipo. Kwanza kabisa, kwa kanuni iliyowekwa kwamba pesa inayopelekwa shuleni inaenda kulingana na idadi ya wanafunzi katika shule husika. Kwa mfano, Shule ya Msingi Bunge ina watoto 150, nitolee mfano tu, kwa kuwa TAMISEMI inatoa Sh.10,000 kwa kila mtoto na katika Sh.10,000 hiyo, Sh.4,000 inabaki TAMISEMI kwa ajili ya kununua vitabu, Sh.6,000 ndiyo inaenda kule shuleni, sasa Sh.6,000x150 kwa mwezi nadhani inakimbilia kwenye Sh.75,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipiga mahesabu ya matumizi kwa ile shule husika bado kuna changamoto kidogo kwamba inakuwa haitoshelezi. Kila shule kwa ajili ya usalama wa vifaa vilivyoko pale ni lazima kuwa na mlinzi. Mlinzi kwa vyovyote hawezi kulipwa chini ya laki moja, itakuwa ni laki moja na *point*. Shule yoyote ni muhimu na ni lazima kama ikibidi iwe na umeme, kama haina umeme basi lakini iwe na maji maana ni muhimu sana. Kwa hiyo, bili za umeme, bili za maji zitatoka kwenye hiyo hiyo Sh.75,000 kitu ambacho unaona kabisa bado kinakuwa ni kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mkuu wa shule huyu Mwalimu Mkuu kila mwezi anatakiwa aende hata mara mbili au ikibidi hata mara tatu kuhudhuria vikao na Afisa Elimu labda ameitwa au ameitwa na Mkurugenzi kwenye Halmashauri, atategemea ile ile Sh.75,000 ndiyo imsaidie yeye kwenda mpaka kule na wakati mwingine ni mbali inabidi alale, hakuna posho ambayo anaipata ya kwenda kulala au usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo, kuna hii michezo ya UMITASHUMTA ambapo anatakiwa huyu Mwalimu Mkuu achekeche akili yake ahakikishe kwamba watoto wanashiriki michezo kuanzia kata, wilaya, mkoa na mpaka taifa. Kwa taarifa nilizonazo ni kwamba mwaka huu Mtwara ndiyo michezo inafanyika kitaifa. Katika hiyo Sh.75,000

yake, atafanya muujiza gani ili watoto hawa waweze kushiriki vizuri michezo kwenye kata, waende kwenye wilaya, washiriki kwenye mkoa, anunue jezi na mipira, kwa kweli kiuhalisia inakuwa bado ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado huyu huyu Mwalimu Mkuu anatakiwa adurufu *internal exams*, *test,* wakati mwingine hata ku-*print* repoti kwa ajili ya watoto hawa wapeleke kwa wazazi wao, zote zinahitaji pesa ambayo inatoka kwenye ile Sh.75,000. Maelekezo yaliyotoka TAMISEMI pia yanaeleza kwamba pesa hiyo hiyo kama kuna marekebisho madogo madogo Mwalimu Mkuu aitumie hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ijaribu kufanya upya *calculation* ili tupate ile *initial cost* ambayo itasaidia kujua pamoja na kwamba tunaenda na uwiano wa shule, pesa inatolewa kwa ajili ya watoto 100, kuna shule nyingine zina watoto 1,000 tunatoa hiyo lakini lazima tuangalie vitu ambavyo ni vya muhimu. Kwa mfano, *issue* ya mlinzi, Mkuu wa Shule asiwe na hiyo *headache* kwamba nitatoa wapi hela ya kumlipa mlinzi mwisho wa mwezi umefika. Ikija bili za maji, umeme, kuna mpishi wa uji, Mwalimu Mkuu anaumia kichwa, kidogo inasumbua na kwa kweli inakuwa ni *burden* kwenye hizi shule ambazo tumelenga kuzisaidia. Kama tunataka elimu bora na tumeanzisha mpango huu mzuri kabisa wa Elimu bila malipo, basi tupeleke na haya marekebisho madogo madogo viende kwa pamoja ili tuweze kulifikia lengo la kutoa elimu bora, siyo tu elimu bila malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, napenda kuishauri Serikali yangu kupitia upya kuangalia kupandishwa kwa madaraja ya walimu. Ni muda kidogo walimu hawajapandishwa madaraja na *increments* za mishahara na yenyewe inaweza ikapunguza kidogo *morale* ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa lengo letu ni jema, tunataka watoto wetu wapate elimu iliyo bora, basi tujaribu

kuangalia makandokando haya ambayo yanaweza yakakwamisha kutupeleka kwenye ile elimu bora tunayoitaka, tuhakikishe tunarekebisha hizi changamoto ambazo nimezizungumzia. Nina imani kubwa na Serikali ya Awamu ya Tano kwamba ushauri huu nilioutoa utafanyiwa kazi kwa sababu naamini pesa ipo, tutajaribu kurekebisha hayo ili tuweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, mchango wangu ulikuwa ni mdogo, naomba muuzingatie. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vicky Kamata kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Conchesta.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu, bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na meli au usafiri katika Ziwa Viktoria. Waziri Mkuu ametueleza namna walivyoweka mkataba ili kuweza kujenga meli katika Ziwa Viktoria. Tangu meli ya Viktoria iharibike ni karibu miaka saba. Wananchi wa Mkoa wa Kagera wameteseka sana na hasa wanawake ambao walikuwa wanatumia meli ile ili kuweza kusafirisha bidhaa na hasa za kilimo na kufanya biashara kati ya Mkoa wa Kagera au Bukoba na Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli hii sasa imekuwa ni hadithi. Tunaomba Waziri Mkuu atueleze pamoja na kusema kwamba wameweka meli kubwa ambayo itaweza kusafirisha abiria zaidi ya 1,000 na mizigo, je, hii meli itakamilika lini? Wananchi wa Mkoa wa Kagera kwa kweli tumeteseka kiasi cha kutosha kwa sababu bidhaa zote zinazokwenda Mkoa wa Kagera zinasafiri kwa njia ya barabara. Kwa hiyo, wananchi wa Mkoa wa Kagera wanateseka sana na kwa kweli tusingependa kulalamika kwamba labda mkoa wetu haupendwi, mnatutupa sana kutokana na matukio mbalimbali hata yale ya tetemeko majibu tuliyoyapewa,

tunaonekana kwamba sisi ni watu ambao hatustahili sana kupata huduma kutoka katika Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye barabara vijijini. *TARURA* ni wakala ulioanzishwa ili kuona barabara za vijijini zinaweza kutengenezwa. Barabara hizi zilikuwa zinatengenezwa na Halmashauri za Wilaya, ikaonekana kwamba huu Wakala ungeweza kusaidia barabara hizi zikatengenezwa na zikaweza kupitika mwaka mzima. Mimi niseme, *TARURA* wanafanya kazi nzuri tatizo walilonalo ni ukosefu wa fedha. Serikali haitoi fedha za kutosha kwa *TARURA* ili waweze kutengeneza barabara vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mdogo tu. Mimi ninafanya kazi katika Halmashauri ya Bukoba Vijijini, wana mtandao wa barabara kilomita 593 na wanapewa bajeti ambayo ni shilingi milioni 800.09 tu kwa bajeti ya mwaka mzima. Ukigawa hizo hela kwa kilomita 593 kila kilomita inapewa karibu shilingi milioni 1.4*.* Unaweza kuona, je, hiyo pesa inatosha *TARURA* kuweza kutengeneza barabara nzuri? *TARURA* wanaweza kutengeneza barabara kama zile zilizokuwa zinatengenezwa na Halmashauri, wanapitisha magreda na mvua ikinyesha zinarudi kule kule zinakuwa mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuiambie Serikali kwamba pamoja na kutengeneza huu Wakala wa *TARURA*, basi wapewe pesa za kutosha. Mjue kwamba kule vijijini ndiyo kuna mtandano mkubwa sana wa barabara na wananchi wanataka huduma hiyo ili waweze kusafirisha mazao yao na kuweza kuinua kipato na maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee kuhusu Tume ya Uchaguzi. Waziri Mkuu ametuonesha jinsi vituo vilivyoongezeka Tanzania Bara, Tanzania Visiwani kule lakini Tume hii ya Uchaguzi naiona kama ndiyo Taasisi pekee ambayo inaweza kudumisha amani katika nchi yetu; ni Taasisi ambayo kazi yake ni kupanga safu ya uongozi katika nchi hii; ni Taasisi ambayo inasimamia moja ya kigezo cha

demokrasia katika nchi, kwa sababu uchaguzi ndiyo mwisho wake unaleta matatizo katika nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii kwa kuangalia uchaguzi mdogo uliofanyika, wote uliofanyika baada ya uchaguzi wa 2015, wamefanya mambo ya ajabu na ya kushangaza sana. Mimi nina jina langu ambalo ningeweza kuita Tume, lakini naogopa msije mkaniambia futa maneno, kwa sababu hii Tume nimeipima nikasema ni kitu gani hiki? Tumekuwa na Tume miaka nenda rudi lakini siyo Tume hii tuliyonayo sasa hivi. Hawa watu nao wamejitoa ufahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshuhudia chaguzi Wilaya ya Muleba katika Kata ya Buhangaza. Nilimwona Mkurugenzi anakuja na Polisi nikiwepo kwa macho yangu. Polisi sita, bunduki sita, anakuja kubeba boksi kama mwizi. Huyo ni Mkurugenzi ambaye anasimamia uchaguzi, yuko chini ya Tume. Wakurugenzi walio wengi ni makada wa Chama cha Mapinduzi, inawezekana wamepewa maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa tahadhari kwamba Tume inawaona Watanzania kama watu legevu, Watanzania ambao wamelelewa katika misingi ya kutopenda kufanya vurugu, Ninachotaka kuwaambia, Tume isitupeleke Watanzania kwenda kufanya mambo yasiyostahili katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa Monduli, nimeshuhudia kwa macho yangu, nilikuwa Mto wa Mbu, nimeona ni jinsi gani Polisi wameweka magari zaidi ya 15, niliyahesabu, magari ya washawasha, wanatisha wananchi. Hatuwezi kufanya uchaguzi wa vitisho. Unatisha wananchi wanashindwa kutoka nje kwenda kupiga kura halafu unasema umeshinda, umeshinda kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Tume sasa iwe huru na pale ambapo uchaguzi utafanikiwa kwa uhuru na haki, mtu atakubali kwa sababu kwa miaka yote ya nyuma

mbona tulikuwa tunakubali mtu akishinda anamshika mwenzake mkono! Kinachotokea sasa, nami nashangaa Serikali iliyoko madarakani, tazama mlivyo wengi ndani ya Bunge, mnahofia nini? Kama mnajigamba kwamba mnafanya kazi nzuri, mnasema maneno yenu, mmefanya kazi, sasa mna wasiwasi gani? Kizuri chajiuza, kibaya chajitembeza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama wewe unajiamini, unaendaje kwenda kufanya madhara ambayo yanafanywa na Tume? Sasa hivi katika siasa za Tanzania sisi upande wa Upinzani tunashindana na dola, hatushindani na Chama cha Mapinduzi. Nami nimeona kwa *style* hii kumbe ninyi ni wepesi kama hamna Polisi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Tume, Waziri Mkuu atueleze: Je, *BVR* zimenunuliwa katika nchi yetu? Ziko ngapi? Zinatosheleza? Tunaomba kujua wananchi wanajiandikisha lini? Tunaomba kujua ni lini Watanzania wataweza kukagua majina yao katika daftari la wapiga kura? Kwa sababu tangu mwaka 2015 hili daftari la wapiga kura halijawahi kuboreshwa. Sasa kama linaboreshwa, je ni lini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rwamlaza, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tu kupunguza *pressure* kidogo ya suala la daftari kwa Mheshimiwa Mbunge, naomba tu nimpe Taarifa kwamba Serikali hii sikivu ambayo inafanya kazi kwa umakini sana, suala la uboreshaji Daftari la Wapiga Kura kwa mujibu wa sheria na Katiba, kazi hiyo imeshaanza. Sasa hivi Tume iko kwenye hatua ya awali ya kufanya majaribio ya vifaa

vyake na mfumo mzima na kanuni zilizopitishwa na Vyama vya Siasa. Wameshaanza hiyo kazi Wilaya ya Kisarawe na hapo Morogoro. Kwa hiyo, Kata mbili sasa hivi ziko kwenye majaribio na mwezi wa Tano tunaanza uboreshaji wa Daftari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge *pressure* itulie, *BVR* ziko za kumwaga, kila kitu kiko tayari kabisa. Tuko tayari kabisa kwa kuanza kuboresha Daftari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mhesimwa Rwamlaza, taarifa hiyo.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Taarifa hiyo Mheshimiwa Jenista wasifanye siri, uchaguzi siyo siri, uchaguzi siyo msiba bwana kwamba hautakuwa na maandalizi. Semeni basi Watanzania wajue mnachokifanya, mpaka uulizwe hapa? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wakijua, watajua kwamba sasa uchaguzi wetu utafanyika kwa uhuru na haki. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Si umeshasikia lakini sasa!

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kwa mzungumzaji.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumpa Taarifa mzungumzaji kwamba ni kweli daftari la mfano limeshaanza na ukiwemo Mkoa wangu wa Morogoro, mimi kama Mwenyekiti wa Chama, CHADEMA Mkoa wa Morogoro na Mjumbe wa Kamati Kuu, tumeingia kwenye hilo zoezi kwenye Kata moja ya Kihonda. Sisi kama

wadau wakubwa wa Daftari hili tumezuia kabisa na Tume kuhamasisha wananchi waende wakajiandikishe isipokuwa Tume wametangaza siku moja tu na hawakufika kwenye maeneo ya mbali ambayo wananchi walipo. Kwa hiyo, Daftari limeenda kwa kusuasua sana, mpaka limemalizika juzi ni wananchi 6,000 tu ndio waliojiandikisha. Kwa hiyo, ni CCM tupu ndiyo wanaofanya hiyo kampeni. *(Makofi)*

Hiyo nakupa... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rwamlaza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa hiyo, kwa sababu najua lazima mizengwe ifanyike katika uchaguzi huu. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, hakikisha kwamba mambo yanaenda vizuri. Wewe ni mwanamama kwa sababu nchi hii ikiingia kwenye matatizo kuna matatizo kuna siku utakuja kusimama na kuomba samahani kwa wananchi kama Rais wa Algeria alivyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mnapofanya matendo haya msijue kwamba baadaye huko Mungu akikujalia ukafika miaka 90 kwamba hutaweza kulaumiwa na baadaye ukasimama mbele ya watu kuomba msamaha kwa matendo machafu yaliyofanyika. Kama watu wataingizwa katika hali mbaya au katika mapigano au katika malalamiko na mambo mengine ambayo hayastahili kutokea kutokana na uchaguzi mbaya unaotokea katika nchi hii. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Zainab Bakar Mussa.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nashukuru kwa kupata nafasi nami nichangie katika hotuba hii ya Waziri Mkuu. Pili, namshukuru

Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya nzuri baada ya kupata ajali. Nawashukuru Wabunge wote ambao walikuja hospitali na ambao walinifariji kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, namshukuru Mwenyekiti wangu kwa misukosuko aliyoipata, lakini ukiona giza linazidi ujue alfajiri inakaribia. Jambo la tatu, napenda niunge mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia katika mambo machache. Jambo la kwanza nitakalochangia ni mapato ya Serikali na sekta binafsi. Hii ni sekta muhimu sana kwa Taifa letu kwa sababu ni sekta ambayo inakusanya mapato ya Taifa. Sekta hii imekuwa ni kama adhabu kwa wananchi na sekta binafsi, kwa sababu katika sekta hii kuna milolongo mingi ya kodi. Kwa mfano, unapoanzisha biashara ama kampuni, kuna milolongo mingi ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, utatakiwa kusajili biashara yako ama kampuni, inahitaji hela; pili, utatakiwa kodi ya mapato ya *TRA,* ni hela; kulipa kodi la zuio, ni hela; kulipa kodi ya ujuzi, ni hela; na hali kadhalika. Hivi kwa mlolongo huu wa kodi, sekta binafsi ndiyo maana zinafunga kampuni zao na wafanyabiashara wanafunga biashara zao. Kwa nini tusiweke kodi ambazo ni chache na kodi ambayo itakuwa ni rafiki kwa wananchi na sekta binafsi kuliko kuweka mlolongo huu ambao unasababisha biashara kufungwa na sekta binafsi kukimbia katika nchi yetu? Hatuoni kwamba hii ni hasara katika nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoweka kodi ndogo ni kwamba wananchi wote watalipa kodi na Serikali itapata mapato ya kutosha, lakini tunapoweka utitiri huu wa kodi, inasababisha wale ambao tunasema wajiajiri washindwe kujiajiri; na wale ambao wataajiriwa na sekta binafsi, sekta binafsi zisiweze kuajiri kwa sababu hali ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee suala lingine la demokrasia nchini. Hali ya demokrasia nchini ni

mbaya sana. Naomba tujitathmini. Serikali ya CCM ijitathmini, ni demokrasia gani ambayo inaonesha? Ni demokrasia gani ambayo wenzetu wanaotuangalia sisi tunawaonesha? Ni kwamba sasa hivi Serikali ya CCM inazuia vyama vya siasa kufanya kazi za siasa wakati Chama cha Siasa kazi yake ni kufanya siasa. Sasa unapoizuia unataka wafanye kazi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ina-*base* upande mmoja. Tunaona kwamba vyama vya Upinzani wanazuiwa kufanya mikutano, wanazuiwa kufanya kazi yao ya siasa. Tukiangalia Chama Tawala, kinafanya mikutano, kinafanya siasa, kinazunguka nchi nzima bila kubughudiwa, lakini leo vyama vya Upinzani ukitaka kufanya siasa, unaambiwa kuna intelijensia, sijui kuna namna gani, huo ni uoga. Hivyo ndivyo mnakufa kidogo kidogo kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kama hiki kikiendelea, mhakikishe 2020 hapa hamtashika dola, kwa sababu wananchi sio wajinga, wanaona yote mnayoyafanya.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Mlinga.

**T A A R I F A**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nimpe Taarifa mzungumzaji kuwa kufanya siasa siyo kufanya mikutano ya hadhara tu, kufanya siasa hata anayofanya Mheshimiwa Lipumba kuwaondoa wasaliti ndani ya *CUF,* hiyo ni siasa tosha. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Unasemaje na Taarifa hiyo Mheshimiwa?

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siwezi kupokea taarifa hiyo, kwa sababu ninavyojua chama cha siasa, ni kufanya siasa. Leo CCM wanafanya

maandamano, lakini wakifanya Chama cha Upinzani inakuwa ni zogo, Polisi, ni kwamba ninyi mnajidai kutokana na kwamba mnalindwa na dola, lakini iko siku hiyo dola itavua jukumu la kuwalinda ninyi ambao mnawateka wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkiendelea hivyo, niwahakikishie 2020 mtalala kifo cha mende. *(Makofi/ Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Waambie!

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niendelee kuchangia. Nataka nichangie katika maandalizi ya uchaguzi na Tume Huru. Tume Huru ni kilio cha siku nyingi katika nchi hii. Serikali ya CCM inajificha katika kivuli ambacho sijui nikiite kivuli gani kwa sababu hawataki kuleta Tume huru ya uchaguzi kwa sababu wanaona ikiletwa Tume huru ya uchaguzi ndiyo kifo chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia katika Tume hii hasa muundo, Maafisa wote wa Tume ni makada wa CCM, Wakurugenzi wote ni makada wa CCM walioshindwa uchaguzi. Hivi hapa kweli pafanyike uchaguzi upinzani, hata siku moja. Huko ni kujitekenya huku mkijichekesha wenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba Tume ya Uchaguzi ni huru sana na ndiyo maana huyu Mbunge anayezungumza ni Mbunge wa Viti Maalum

baada ya Tume kutangaza Wabunge wa CHADEMA wengi wakapata Viti Maalum. Pia mimi nilitangazwa na Tume hii nikiwa CHADEMA na nimetangazwa tena nikiwa CCM, maana haipendelei kabisa. Hii Tume ni huru, waendelee kuchapa kazi, wanatenda haki na hiyo ndiyo taarifa. *(Makofi/ Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa…

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei taarifa hiyo kwa sababu alitoka huku akaenda huko, wakiweko huko wanakuwa kama wamerogwa fulani wanaropokwa ropokwa tu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama CCM inajiamini, ithubutu leo hii kuleta Tume Huru ya Uchaguzi. Kama CCM inajiamini, ithubutu leo hii kuleta Katiba mpya ya wananchi inayopendekezwa. Nawapa changamoto hiyo, mkiweza, nitajua mnajiamini, lakini mnashindwa kujiamini kutokana na kwamba mkileta Tume Huru ya Uchaguzi au Katiba ya wananchi inayopendekezwa kwa dola mtasahau.

**KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu…

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu kanuni ya ngapi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kanuni ya ngapi, nakuuliza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 64(1) (a). Mheshimiwa Mbunge anayechangia hatatumia ndani ya Bunge taarifa

ambazo hazina ukweli. Mimi sijalogwa. Kwa hiyo, naomba athibitishe au afute hiyo kauli. Kikanuni, naomba athibitishe au afute hiyo kauli, mimi sijalogwa. Nathibitisha niko timamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba afute hiyo kauli au alithibitishie Bunge kwa mujibu wa kanuni hii.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niendelee kuchangia. Wakati watu wanadai Tume Huru ya Uchaguzi ziliundwa Tume zaidi ya tatu; iliundwa Tume ya Jaji Nyalali, Kamati ya Jaji Robert, baadaye ikaja Rasimu ya pili ya Katiba mpya na wananchi wote walitoa maoni yao kwamba wanataka Tume Huru ya Uchaguzi. Ni kwamba Tume iliyopo hapa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar siyo huru.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, muda ndiyo huo. *(Makofi/ Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima zote, sisi hatuamini kwatika mambo ya uchawi.

Tunaendelea, Mheshimiwa Augustine Holle Vuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Rukia Kassim Issa na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ajiandae.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia kwenye bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mchango wangu utajikita sana kwenye shukurani, maombi, pia na ushauri. Nitaanza na la mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kushauri kwanza kwenye suala la vibali vya ajira. Nchi yetu hii tunavyojua ni kwamba ina soko dogo sana la ajira. Ajira ni chache lakini tunao vijana wengi ambao hawana ajira. Kwanza

nimpongeze Mheshimiwa Jenista na Ofisi yake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwenye kudhibiti otoaji holela wa vibali vya ajira. Maana hapo katikati vibali hivi vimekuwa vinatolewa kama njugu, sasa sisi kama Taifa tuna uhitaji mkubwa wa ajita kwa sababu kuna vina wengi ambao wako mtaani. Nashangaa kuna watu ambao wanakuja hapa Bungeni kutetea kwamba Serikali izidi kumwaga vibali vya ajira hii kwa wawekezaji mbalimbali. Jambo la ajabu kabisa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa sababu tuna vijana wengi ambao wako mtaani, Mheshimiwa Jenista na ofisi yake waendelee kuminya. Nimpongeze Kamishna wa Ajira, waendelee kuminya, wasitoe vibali hivi kwa wageni ili wananchi wa Tanzania, vijana wengi ambao wako mtaani ambao hawana ajira, waendelee kupata kazi hizi. Hili ni jambo la kwanza. Niseme, kwa sababu tunajua kuna shida, tatizo kubwa la ajira nchini, mimi nitoe ushauri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwamba iundwe *Task Force,* yaani Kikosi Kazi, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ambacho kitajumuisha wasomi, wajasiriamali na wadau mbalimbali ili kuweza kujadili tatizo hili la ajira nchini na hatimaye waweze kutoa ushauri mzuri kwa Serikali yetu pendwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua, Serikali inaendelea na juhudi zake za kuendelea kutoa ajira kwa maelfu...

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vuma, taarifa.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa msemaji, hoja iliyopo hapa ni ile sheria inayosema kwamba, mwekezaji ana fursa ya kuleta watu watano wa mwanzo, *automatic* bila hata akileta mtu wa aina gani, wale ambao watamlindia mali yake. Kwa hiyo, hawa kwa nini wanasumbuliwa ndiyo hoja, napenda kumpa taarifa hiyo, wakati wameshatajwa kwenye sheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Augustine taarifa hiyo unasemaje?

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei, kwa sababu Kamishna wa Ardhi anaifahamu vizuri kabisa Sera na Sheria yetu, amekuwa anawanyima vibali watu ambao hawana sifa za kupata vibali vya kuajiriwa, kabisa, kwa sababu nina watu ambao nimeshuhudia kwa macho yangu, wenye vigezo, wanapata vibali. Kwa hiyo, wale ambao wananyimwa ni wale ambao hawana vigezo na nashauri Kamishna wa Ardhi aendelee kukaza buti, kwa sababu kuna vijana, kuna wadogo zetu, kuna watoto wengi ambao wako mtaani ambao hawana kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Ofisi ya Mheshimiwa Kairuki, Uwekezaji, kwamba niko Kamati ya *PIC* tuna Mashirika mengi ya Serikali, tuna mashirika mengi ya Serikali ambayo yana fedha nyingi sana. Badala ya mashirika haya kwenda kujikita kuwekeza kwenye ujenzi wa majengo ya nyumba za kuishi, sijui za biashara, nashauri, washauriwe watu hawa waende kuwekeza kwenye sekta ambazo zitawagusa Watanzania walio wengi sana, hususan kwenye kujenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nitoe ushauri mmoja, kwamba katika Awamu hii ya Tano, ambayo tunajua kwamba ni Serikali ya Viwanda, ningeweza kushauri kwamba, Mheshimiwa Waziri akae na Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii, hasa *NSSF, PSSPF,* waweze kukaa pamoja na kutafuta wadau mbalimbali wengine ambao wataunganisha nguvu pamoja, tupate kiwanda kikubwa cha mbolea katika nchi hii ili tuweze kuondokana na tatizo la kuagiza mbolea kila mwaka kutoka nje ya nchi, ushauri huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri kwenye suala pia la *internship*, vijana wengi ambao wanamaliza vyuoni wanakaa mtaani na wakati mwingine wanakosa ajira katika sehemu mbalimbali kwa sababu ya ukosefu wa uzoefu. Sasa nashauri, Serikali iwe na mkakati wa kutoa *internship* kwa vijana ambao wanamaliza vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua huwa tuna utaratibu, tuna mipango kwamba baada ya mwaka mmoja tunaajiri watu kadhaa, baada ya miaka mitano tutaajiri vijana kadhaa. Sasa ushauri wangu ni kwamba, vijana wanapokuwa wamemaliza vyuo vikuu, basi tuwe na utaratibu kabla haujafika wakati wa kuwaajiri, tuwachukue tuwaweke sehemu mbalimbali katika ofisi za Serikali, kwenye mashule, mahospitali na sehemu nyingine, waende wakajifunze kuchapa kazi ili wasiwe tu na elimu bali pia wawe na uzoefu wa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wako tayari kujitolea, kwa sababu wanajua kwamba kwenye kujitolea wanapata uzoefu na hatimaye wanakuwa na nafasi ya kupata kazi hata kwenye sekta binafsi kwa sababu wanakuwa na uzoefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, tumepanga, kwa sababu Makao Makuu ya Halmashauri yako kwenye Halmashauri ya Kasulu Mji, kwa mzee wangu Nsanzugwako pale. Naomba Serikalini, kwamba eneo la kujenga Makao Makuu ya Halmashauri, tunalo tayari, pale Kata ya Nyamnyusi, kwa hiyo, niombe fedha kwa ajili ya ujenzi wa halmashauri ili kwamba tuweze kutoka Kasulu Mjini, twende sehemu yetu kwa maana ya kuwafuata wananchi na kuwapelekea huduma zaidi karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Chuo cha Ufundi cha Nyamidahu, hiki chuo tumejengewa na *World Vision,* wamejenga chuo kizuri kina mabweni, kina madarasa, kina *furnitures*, lakini sasa hakina vyoo, hakina umeme na miundombinu midogomidogo. Kwa hiyo, niombe Serikali kwamba ikichukue chuo hiki, ikimalizie, kwa sababu kina zaidi ya miaka mitatu toka kikamilike ili kiweze kuanza kutumika kuwanufaisha wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine, kwa sababu tunaendelea na miradi ya umeme miwili, kwenye Jimbo la Kasulu Vijijini na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla, tunaendelea na *REA*, lakini na ujio wa Gridi ya Taifa. Najua kwenye gridi ya

Taifa, *evaluation* imefikia asilimia 90, na mwezi wa Sita kwa maelezo niliyonayo, kwamba watakuwa wamemaliza tayari *evaluation*. Wananchi wa Mkoa wa Kigoma wamesubiri kwa muda mrefu sana ujio wa umeme wa gridi ya Taifa, kwa hiyo, niombe chonde chonde *evaluation* itakapokamilika, kwenye bajeti hii ambayo tunaipitisha muda si mrefu, ya mwezi wa Sita, basi wananchi wa Kigoma tuhakikishe kwenye bajeti hii wanapata umeme wa gridi ya Taifa kwa sababu tumesubiri muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipende kuomba pia, tumepata vibali vya miradi ya maji, miradi ya Nyamnyusi, Titye na Lalambe kule, zaidi ya bilioni sita, tumepata vibali vya kutangaza tenda hizi. Niombe tutakapopata mkandarasi kusiwepo na ucheleweshwaji wa fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya mkandarasi huyu ili kuhakikisha kwamba mradi unakamilika kwa wakati na wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Serikali, kuna vitu vingi sana ambavyo imefanya kwenye Jimbo la Kasulu Vijijini. Tumepata milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha Nyamidaho, tumepata milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha Rusesa Uboreshaji, tumepata milioni 500 ujenzi wa kituo cha afya cha Nyakitonto, tumepata bilioni moja na milioni mia tano kwa ajili ya ujenzi ya hospitali mpya ya Wilaya kwenye Kata ya Nyamnyusi. Napenda kuishukuru sana Serikali, kwa kweli kazi kubwa imefanyika, kazi kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu, juzi tumepata fedha milioni mia tatu kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na kupanua Sekondari ya Kasangezi. Tumepata fedha tumemalizia shule ya Asante Nyerere, imeanza tumesajili, tumepata fedha tumemalizia shule ya Sekondari Kitanga imeanza tayari, lakini pia tumepeleka milioni 48 kwenye shule ya msingi Shunga. Kwa kweli kazi kubwa inafanyika, na niwaambieni, mwaka 2020, Magufuli Kasulu yeye aje apunge mkono tu atashinda. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vuma ahsante sana.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Rukia.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nami kuwezakupata nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu. Naanza katika kitabu hiki cha Waziri Mkuu, ukurasa wa 11 unaozungumzia mfumko wa bei. Taarifa za kitabu hiki zinasema kwamba mfumko wa bei umepungua kwa wastan wa asilimia nne kwa mwaka 2018 hadi asilimia tatu kwa mwaka 2019. Jambo ambalo naliona liko tofauti kabisa, hali ya maisha ya mtanzania wa kawaida bado ni ngumu sana na kadri tunavyokwenda mbele maisha yanazidi kuwa magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa kutoa na mifano, mwaka 2018 Juni, Mtanzania wa kawaida alikuwa ananunua sukari kilo moja kwa Sh.2,100/=, leo Mtanzania huyu huyu ananunua sukari kwa Sh.2,400/=. Mwaka huo huo 2018, Mtanzania alikuwa ananunua maharage kilo moja Sh.1,700/=, mwaka huu 2019 ananunua kwa Sh.2,400/=. Mtanzania huyo huyo alikuwa ananunua tambi kilo moja Sh.1,700/=, lakini hivi sasa ananunua tambi Sh.2,500/= kwa kilo moja. Mafuta ya kula Mtanzania alikuwa ananunua lita moja ya mafuta Sh.1,100/=, lakini Mtanzania huyo huyo mwaka huu 2019 ananunua mafuta ya kula Sh.2,000/= kwa lita moja. Tulikuwa tunanunua mafuta ya *petrol*, kwa bei lita moja Sh.1,600/=, lakini hivi sasa ni Sh.2,206/=. Hapa napata ukakasi, naomba nipatiwe ufafanuzi. Je, mfumuko wa bei umepungua au umezidi? Mheshimiwa Waziri naomba awafafanulie Watanzania wajue, je, maisha yamezidi kuwa magumu au yamekuwa mazuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hapo, nataka niende katika kitabu hikihiki cha Waziri Mkuu, ukurasa namba 44, unaozungumzia kupunguza kwa msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Ni kweli msongamano wa magari umepungua, tokea kujengwe lile daraja la juu la

Mfugale. Pia tunategemea hali itazidi kuwa nzuri likimalizika kujengwa daraja la juu lile la makutano ya Ubungo, pamoja na daraja la *Salender Bridge.*Pia naishauri Serikali, Halmashauri ya Jiji sasa, ili na wao wajitahidi katika hili, waweze kutengeneza barabara zile za ndani, za mitaa, zilizoko Kariakoo wazitie lami, barabara za Kariakoo zile za mitaani, barabara za Ilala, za Magomeni ili sasa magari yaweze kupita kiurahisi katika zile barabara za mitaa kuliko kusubiri kupitia katika barabara zile kubwa tu,hapo nahisi kidogo foleni itaweza kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba kutoa ushauri kwa Serikali. Wenzetu wa Senegal nchi yao ni ndogo tu, wana *beaches* nzuri, kama hizi zetu zilizopo Tanzania, Tanzania tumebahatika kuwa na *beaches* nzuri, tuna ufukwe wa bahari ambao ni wa kupendeza, una upepo wa kuvutia, lakini jiji hawajajitayarisha kuutengeneza huu mji wetu wakati huu mji wetu ni kioo cha Tanzania. Wageni wengi wanakuja hapa, hata sisi wenyewe, mji wetu ukijengwa, ukiwa katika mazingira mazuri na sisi pia tutafurahia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali, Halmashari ya Jiji ya Dar es Salaam watengeneze fukwe zile za Oysterbay*,* badala ya kuziacha katika mazingira yale. Sasa hivi watengeneze *public gym*, ambayo watu wetu wataweza kwenda kufanya mazoezi, wataweza kupata afya bora, tutajenga vijana walio na afya bora na tutatengeneza Taifa ambalo lina vijana walio na afya bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, watengeneze sehemu za kupumzikia, kama vile Zanzibar tulivyofanya Forodhani ili watoto wetu waweze kupata sehemu za kwenda kucheza, kupumzika, watu wazima waende pale kupumzika na kupunga upepo wa bahari na pia mji wetu utapendeza na utavutia hata kwa wageni watakaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitakwenda sasa kwenye barabara, kwanza naipongeza Serikali kwa kutekeleza Sera yake ya kuunganisha barabara za mikoa hizi kwa lami, wakiendelea na sera hii tutaweza

kukuza uchumi, kitakuwa ni kichocheo cha kuleta maendeleo ya kiuchumi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawaomba watu wa barabara, yaani watu wa *TANROADS*, wajitahidi kutekeleza ile Sera na Sheria Namba 13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2019, waweze kuweka vigingi katika barabara, waweze kuangalia alama za barabarani, watoe taaluma kwa wananchi wetu, wasiharibu barabara. Kwa sababu watu wengi wanatoa alama za barabarani na hawajui adhabu yake ni nini. Wakiweza kutoa taaluma katika vyombo vya habari na watu wakajua kama unapotoa alama za barabarani kosa lake ni hili, watu wetu wataweza kuogopa na wataheshimu zile alama za barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri watu wa *TANROADS* waweke watu maalumu ambao wataangalia alama zote za barabarani zitakazotolewa pamoja na rangi ambazo zinaweza kuwa zimefutika. Alama za barabarani zinasadia sana kuepusha ajali za mara kwa mara. Nasema hili kwa mfano, unapotoka Dar es Salam jioni ukafika huku Dodoma alfajiri, ukifika maeneo ya Gairo unakumbana na ukungu. Ukungu ule unakuwa huoni mbele yako kama kunakuja gari au haiji, huoni hata zile alama tena na barabara huioni, lakini zile alama za barabarani nyeupe zilizochorwa katikati ya barabara ndiyo alama pekee ambazo zinamwelekeza dereva wapi apite na wapi aelekee, bila alama zile nadhani magari mengi yangelianguka. Kwa hiyo, nashauri watu wa *TANROAD* wajitahidi, kila ambapo alama zile zimefutika wazirudishe na kila ambapo kuna alama za barabarani nyingine zilizotolewa wazirudishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hapo, sasa nataka nijielekeze kwenye Jeshi la Zimamoto, mara kwa mara tunakumbana na maafa ya moto katika maeneo yetu, lakini Jeshi la Zimamoto halijajipanga kutoa taaluma kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, naomba wawe na kitengo maalumu cha kutoa mafunzo, aidha kwenye Luninga, kwenye vyombo vya habari na watoe hata vingine kwa vitendo katika maeneo yetu. Kwa sababu ajali za moto, kuna

mioto ya aina nne, kuna moto unaosababishwa na makaratasi au mbao. Moto huu unakuwa unazima kwa kupitia maji, watu wetu wakishajua pindi inapotokea moto wa namna hii.....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rukia ahsante sana. Tunaendelea Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu atafuatiwa na Mheshimiwa Shaban Shekilindi na Mheshimiwa BahatiAlly Abeid ajiandae.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, maana yake nilishaanza kukata tamaa, maana yake muda unazidi kwenda. Naomba kwa kuanza kabisa niunge mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya Bajeti yake na vilevile naunga kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa umahiri wake, kwa uongozi wake na umakini wake wa kusimamia shughuli za Serikali na unaiona katika hotuba aliyoleta mbele ya Bunge hili. Vilevile nitakuwa mnyimi wa fadhila kwa sababu najua kazi wanayofanya Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Angella Kairuki kwa kuweza kumsaidia na kuonyesha mambo mazuri yanayofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kutumia nafasi hii vizuri, nitajielekeza kwenye uwekezaji na nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kuona mambo kwa upesi kuitoa Wizara hii, Sekta hii kwenye Viwanda na Biashara na kuileta chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa sababu uwekezaji ni suala mtambuka, uwekezaji uko kwenye viwanda, uwekezaji uko kwenye kilimo, uwekezaji uko kwenye elimu na uwekezaji uko kwenye sehemu nyingi. Kwa hiyo, mahali panapofaa ni kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuona hili, kwa sababu kwa kweli, katika uwekezaji ndiyo tutaongeza mapata ya Taifa hili, bila uwekezaji hatutaweza kuongeza

mapato ya Taifa hili. Vilevile, ajira hii inayoliliwa na vijana ambao wako vijijini na ambao wanatoka vyuo vikuu na vyuo vingine itatokana na uwekezaji ambao tutawekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi ya hapo, vilevile uwekezaji ndiyo unatumia teknolojia mbalimbali na kuongeza maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, lakini vilevile kwa ajili ya yeye kusimamia uwekezaji huu kupitia ofisi mbalimbali, Tanzania imekuwa ya saba katika bara la Afrika kuvutia uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, mtaji umeongezeka, uwekezaji umeongezeka kutoka dola 640 mwaka 2005 hapo tulipo mwaka 2016 ilifikia mwaka dola 1,365, ingawa umeteremka kidogo mwaka 2017 kuwa dola milioni 1,180 kwa sababu huu ndiyo mwelekeo wa dunia, siyo wa Tanzania, lakini Tanzania ndiyo iko mahali pazuri na wanaotaka kuja kuwekeza Afrika watataka Tanzania kwanza, kwa ajili ya amani yetu. Vile vile uwekezaji kwenye miundombinu, uwekezaji kwenye maji, uwekezaji kwenye maeneo ambayo yanahitaji kufanya uwekezaji uwe rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo, ningependa kuona kwamba, mwelekeo wa uwekezaji kwa Tanzania pamoja na mazingira mazuri ambayo Serikali imeweka, Tanzania katika nafasi nzuri iendelee kuona kwamba inasahihisha maeneo ambayo yataifanya Tanzania iwe bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo, napenda kuona kwamba mwelekeo wa uwekezaji kwa Tanzania pamoja na mazingira mazuri ambayo Serikali imeweka iendelee kuona kwamba inasahisha maeneo ambayo yataifanya Tanzania iwe bora zaidi.

Naomba tuimarishe *One Stop Center,* kwa sababu bila ya hivyo, kwa mwekezaji kutoka nje au kutoka ndani kwenda *BRELA*, *TRA* na sehemu nyingine itamchukua muda na wakati mwingine anakwamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba tufuate mfano ambao uko Rwanda wa *Rwanda Development Company* au *Center* ambapo mambo yote ya uwekezaji yako mahali pamoja na wale ambao wako pale wana uwezo wa kupitisha na wawekezaji wanaweza wakapitishwa sehemu zote hata kwa siku moja. Kwa hiyo, naomba sana sisi Watanzania tuone umuhimu huu badala ya kuwa na *TIC* peke yake halafu hawana uwezo wa kupitisha kitu cha *BRELA* ambayo iko viwanda, hawana uwezo wa kupitisha mambo ya *TRA* ambayo yuko Wizara ya Fedha, tungepaswa kuwa siyo *TIC* tungekuwa na shirika au taasisi ya uwekezaji ambayo ina watu ambao wanaweza kupitisha kodi kiasi gani na mengine yote yanayohusika kwenye mambo ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali imeimarisha sera, sharia na taasisi. Serikali kwa kuimarisha mazingira ya uwekezaji, kuna *Roadmap* ambayo imewekwa ambayo kama tutaisimamia vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu uwekezaji utakuja kwa nguvu zaidi. Ni muhimu sana Wizara na taasisi za Serikali zinazohusika katika kutekeleza mpango huu ziwe na mikakati madhubuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kusema ni kwamba Ofisi ya Waziri kama mratibu wa uwekezaji ni muhimu pia kuratibu na kusimamia mpango ambao unapitia *Blueprint* ya viwanda kwa sababu wakati huu ni wa kuimarisha viwanda, tuiangalie na mahali ambapo kuna upungufu tuweze kuyaboresha. Ukiunganisha hii *Blueprint* na *Roadmap* nina hakika nchi hii itajielekeza vizuri kwenye uwekezaji, mapato ya Serikali na uwekezaji unaotoka nje tukiimarisha hatutakuwa tunarudi nyuma bali tunaenda mbele na tutapata mapato zaidi kwenda kwenye elimu, afya na sehemu zingine. Ndugu zangu kama nchi haitatilia mkazo kwenye uwekezaji hatutafanya mambo makubwa tutakuwa tunatumia au tunakula bila kuangalia kesho tutapata faida gani. Tusipowekeza hatuwezi kujiendeleza kwenye mahitaji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Angellah mwanangu huyu ambaye alikuwa na mimi wakati nikiwa Waziri wa Katiba na Sheria na nimefurahi sana kwa sababu ni mchapakazi na atamsaidia Mheshimiwa Waziri kuona uwekezaji unaenda vizuri na uchumi wa nchi hii utapanda na uchumi ukipanda huduma za jamii na mambo mengine yatakuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Nakushukuru sana, nilitaka nijielekeze kwenye uwekezaji kwa sababu najua umuhimu wa uwekezaji ambao sasa hivi unatiliwa mkazo kwa kuwekwa chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naunga mkono hotuba na bajeti hii na hii hotuba itafanya hotuba zingine ziende vizuri. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mwenyekiti wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu. Tunaendelea na Mheshimiwa Shaaban Shekilindi, Mheshimiwa Bahati Abeid na Mheshimiwa Augustino Masele wajiandae.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo ndiyo iko mbele yetu. Kwanza kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake, Mheshimiwa Jenista pamoja na Mheshimiwa Mheshimiwa Kairuki kwa kazi kubwa wanayoifanya, hakika mwenye macho haambawi tazama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja niende kwenye suala zima la afya. Kwanza niendelee kuipongeza Serikali yangu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa wanayoifanya kwani hivi karibuni tumeshuhudia karibia Hospitali za Wilaya 67 zimekarabatiwa. Sambamba na hayo, Hospitali yangu ya Wilaya ya Lushoto sijaiona na hospitali ile ni kongwe, ni ya zamani sana. Hospitali ile inachukua karibia Wilaya tatu ambazo zimezunguka pale, naamini inahudumia takribani watu 500,000. Niiombe sasa Serikali yangu Tukufu watakapokuja ku-*windup* basi waingize hospitali hii iweze kukarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kama nilivyokwishasema hospitali hii ni kongwe lakini pamoja na ukongwe wake majengo pia ni ya zamani sana, hayaendi na wakati, inapitwa mpaka na kituo cha afya. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu Tukufu sasa itengee fedha kwa ajili ya Hospitali hii ya Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hospitali hii haina *X-Ray* kwa muda mrefu, sasa hivi ni takribani miezi sita. Hata Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi wakati anakuja Lushoto nilimlalamikia kuhusu *X-Ray* hii. Kwa hiyo, niiombe sasa Serikali yangu Tukufu iweze kupeleka *X-Ray* ile wananchi wangu waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vituo vya afya ambavyo vinaendelea kujengwa. Niishukuru Serikali yangu Tukufu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwani tumepewa Kituo cha Afya kimoja cha Mlola, tumepewa takribani shilingi milioni 700; shilingi milioni 400 kwa ajili ya majengo na shilingi milioni 300 kwa ajili ya vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nguvu za wananchi tumeshajenga vituo vya afya viwili ambavyo viko hatua tofauti tofauti. Kituo cha Afya Gare tayari kina maboma zaidi ya matatu na vyumba zaidi ya 20. Kama ilivyoahidi au kama ilivyo ada wananchi wanapojenga maboma yale basi Serikali inamalizia maboma yale, kwa hiyo, niiombe Serikali yangu Tukufu ipeleke fedha tuweze kumalizia maboma yale na wananchi wa Gare na wa Lushoto kwa ujumla waweze kupata huduma hiyo na kupunguza msongamano ambao upo katika Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Kituo cha Afya Ngwelo tunaanza kukijenga na kiko hatua ya lenta kwenye *OPD*. Kwa hiyo, niiombe pia Serikali yangu Tukufu kwamba ipeleke fedha pale tuweze kukamilisha kituo kile cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna zahanati kama Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inavyosema kwamba kila kijiji kitajengwa zahanati. Wananchi wa Lushoto kwa nguvu zao

wamejenga zaidi ya zahanati 12. Zahanati sita ziko tayari zinahitaji vifaatiba na watumishi, zahanati sita ziko kwenye lenta. Kwa hiyo, niombe Serikali yangu kama ilivyoahidi au kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyosema kwamba mnapofikisha kwenye mitambaa ya panya basi Serikali itachukua. Niombe sasa Serikali iwaunge mkono wananchi wa Jimbo la Lushoto ili waweze kumalizia zahanati zile ambazo zimebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la *TARURA.* Kwa kweli *TARURA* ni watu wazuri sana na wanafanya kazi kubwa sana ambayo kwa kweli inafaa kuigwa lakini haina fedha za kutosha. Kama unavyofahamu Lushoto ni ya wakulima wa mbogamboga na matunda na kahawa lakini wanapata hasara kubwa sana hususan mvua zinaponyesha mazao yao huwa yanaozea shambani kwa sababu ya kukosa miundombinu ya barabara. Niiombe Serikali yangu Tukufu iangalie namna ya kuiwezesha *TARURA* waweze kupata fedha nyingi ili waweze kutengeza barabara zile za Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ambazo ni *critical issue,* mfano barabara ya kutoka Mlalo – Ngwelo – Mlola – Makanya - Milingano – Mashewa. Barabara hii ni ya kiuchumi na kila siku, kila mwaka na kila wakati naisemea lakini mpaka leo haijatengezwa. Kwa hiyo, niombe Serikali yangu Tukufu kwamba barabara ichukuliwe na *TANROADS* kwa sababu inaunganisha wilaya hadi wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lushoto kuna barabara moja kuu tu ambayo inatoka Mombo - Soni – Lushoto, kwa hiyo, Wilaya nzima ya Lushoto barabara ya kuingia Wilayani ni moja tu. Kuna barabara moja ya mchepuko ambayo inatoka Dochi - Ngulwi - Mombo, hii ni barabara muhimu sana na kwa kweli itaenda kutatua kilio cha wananchi wa Lushoto kwa sababu ni njia fupi, ni kilometa 16 tofauti na barabara ya kutoka Mombo - Soni - Lushoto ambayo ni kilometa 32, ni nusu ya barabara hiyo. Niiombe Serikali kutenga fedha ili barabara ile iweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye suala zima la umeme, kwa kweli tumekuwa tunajibu maswali magumu sana ambapo na sisi tunashindwa kuyajibu. Niiombe sasa Serikali yangu Tukufu, dada yangu Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Medard ameshafika Lushoto na ameona hali halisi ilivyo, ameona jinsi wananchi wa Lushoto wanavyopenda umeme na anajua kabisa Lushoto hakuna nyumba ya nyasi hata moja na wananchi wa Lushoto tayari wameshafanya *wiring* kabla hata hawajatangaziwa mambo ya umeme. Kwa hiyo, niiombe sasa Serikali ipeleke umeme kwa wananchi wangu wa Lushoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye suala la kilimo, Lushoto kuna zao moja la kahawa ambalo hata wadau wa mkutano juzi walikaa pale *LAPF* wakasema kahawa ya Lushoto ni bora kuliko kahawa ya sehemu nyingine. Kwa hiyo, niombe sasa Serikali yangu ipeleke pembejeo na miche kwa ajili ya kupanda kahawa katika milima ile ya Usambara ili tuweze kupata kahawa bora tuweze kuimarisha kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kumalizia niongelee uwekezaji. Hebu tuangalie ni namna gani ya kuondoa changamoto zinazowakwaza wawekezaji wetu. Mheshimiwa Kairuki naamini ni jembe, unafanya kazi iliyotukuka, kuna Kiwanda cha Sementi kule Mkinga, mwekezaji yule anaweka shilingi trilioni 7.7 lakini leo hii ni mwaka wa tatu hajafanikiwa. Naomba Mheshimiwa Kairuki kwa sababu Wizara hii umeshakabidhiwa naomba kabisa uanze na hili tuhakikishe mwekezaji anafungua kiwanda kile. Kiwanda kikishashafunguliwa inamaana wananchi watapa ajira, uchumi wa Taifa utakua na mambo mengine yataenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali yangu Tukufu Uwanja wa Ndege Tanga sasa upanuliwe ukizingatia sasa hivi tuna bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda. Tanga sasa inaku,a tunaongeza kina cha bahari, ina maana wawekezaji na wanachi wengi watakuja kwa ajili ya fursa zilizopo Tanga. Kwa hiyo, niombe Serikali yangu Tukufu iweze…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Nyamagana, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Masele na Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Napenda sana kwa nafasi hii nami nichangie walau maeneo machache ambayo nadhani nitayasemea vizuri kwa ajili ya faida na manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba nami sitakuwa nyuma kuungana na wenzangu wote walioipongeza na kuishukuru Serikali kwa utendaji wake mkubwa ambao kwa kweli unaonekana kwa vitendo na si kwa maneno peke yake. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu namna ambavyo amekuwa akishiriki kwa asimilia kubwa kuhakikisha majukumu yote ya Wizara anayoisimamia yanatekelezeka kwa wakati na kwa namna ambavyo yamekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda njikite kwenye mambo ambayo nimepanga kuyazungumzia sana. Moja ni juu ya viwanja vya ndege. Ni ukweli usiofichika kwamba Taifa letu sasa hivi baada ya kuwa lina uwezo wa kumiliki ndege ilizonazo leo hakuna ukweli unaopingika kwamba ni lazima sasa tujikite kwenye kuimarisha viwanja vyetu vya ndege. Tumeanza ujenzi wa viwanja hivi kwa muda mrefu, vingine vilihitaji ukarabati mdogo, vingine vilihitaji ukarabati wa kati na vingine vilihitaji ujenzi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila wakati nimekuwa nikisema juu ya Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Uwanja huu kwa namna ulivyoanza na unavyopangiwa bajeti kila kukicha lakini bajeti hii isipokamilika kama ambavyo imekuwa, leo tuna zaidi ya miaka ya sita tunazungumzia uwanja wa ndege ambao unasafirisha abiria wengi kabisa kwenye nchi hii. Mwaka jana nilisema hapa na hata Mheshimiwa Waziri wa Utalii atakuwa ni shahidi yangu. Ushahidi huu unatoka na ubora na umuhimu wa Uwanja wa ndege wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rekodi tulizokuwa nazo mwaka jana kama tutaendelea hivi tutamaliza miaka hii uwanja huu hautafanikiwa. Tumeshajenga jengo la mizigo, jengo la kuendeshea ndege na tumeshapanua uwanja wa ndege, kila siku nasema huku ni sawa na kuvaa suti na kutembea na kandambili hutaonekana nadhifu kwa sababu ya namna ambavyo unaonekana. Kwa hiyo, nishauri sana Serikali kwa bajeti hii ambayo tumeitenga safari hii, Mheshimiwa Waziri Mkuu Uwanja wa Ndege wa Mwanza uwe ni sehemu ya kipaumbele tukiwa tumeelekeza katika kukuza utalii, lakini tukiwa tumeelekeza katika kuendelea kulipa hadhi Shirika letu la Ndege lakini ubora wa kiwanja chenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nilitaka nizungumzie juu ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA).* Tulipoamua kuikabidhi Mamlaka ya Mapato Tanzania jukumu la ukusanyaji wa mapato kwenye maeneo mbalimbali kutoka Halmashauri kuna mambo ambayo yatatupelekea miaka inayokuja tupoteze kabisa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka kwenye Jiji, pale katikati Mwanza Mjini, leo ushuru wa mabango baada ya kwenda *TRA*, naamini tukiwaweka hapa watupe *record, record* watakazotupa hazitalingana na kile ambacho kilikuwa kinafanywa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaweza kupigwa mkono gari mfano gari ya Pepsi, gari yenye trela ikipigwa mkono inachukuliwa futi inapimwa urefu na upana mtu anatozwa

shilingi 500,000, shilingi 600,000 au shilingi 800,000 kwa gari moja, ana gari 300 huyu mtu, unategemea makampuni ya stahili hii yatafanya nini? Yalichoamua sasa hivi ni kufuta maandishi wanabakisha rangi nyekundu, Pepsi atafuta maandishi ya Pepsi atabakisha rangi ya *blue* na Konyagi watafuta konyagi watabakisha rangi za njano. Matokeo yake ni nini? Mwaka ujao hatutapata hata shilingi 100 ya fedha kidogo ambayo tungeweza kuipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe warudi nyuma ambavyo Halmashauri zilikuwa zinafanya. Mfano upo, Mheshimiwa Rais alipoelekeza kukusanya kodi ya majengo kwa kiwango cha shilingi 10,000 na shilingi 50,000 kwenye nyumba zenye sakafu moja na kuendelea imeleta mafanikio makubwa sana. Kwa nini hawataki kujifunza kufanya kidogo ili upate kingi? Sasa ni sehemu ambayo inatupa tabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu suala la vitambulisho na namshukuru Mheshimiwa Rais amelisema juzi. Yuko mwendesha bodaboda ambaye tayari ameshatambuliwa na Serikali, ndiyo maana leo analipa bima Sh.76,800, leseni ya pikipiki shilingi 56,000, kodi ya Halmashauri ambayo wanagawa *50%* na *SUMATRA* shilingi 22,000, tunapomwambia leo alipe Sh.20,000 tunamkosea na tunamkosea Mheshimiwa Rais kwa sababu siyo sawa. Ni lazima tuwaache hawa watu walipo na tuangalie namna ya kuwapunguzia mzigo na siyo kuendelea kuongeza mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumza juu ya uboreshaji wa bandari. Sisi sote hapa tunafahamiana na sote hapa tunafanya biashara kwa namna moja au nyingine. Bandari ya Da es Salaam pamoja upanuzi mkubwa tunaoufanya leo hatuwezi kufanikiwa kwa sababu ya namna mbovu inavyoshughulikia ukusanyaji mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo haya tusipoyasimamia, mtu ana *bonded warehouse,* huyu ni mtu anauza *brands*

ikifika wakati *brands* zimeisha huyu mtu anaonekana lazima alipe kodi wakati ambao sote tunafahamu namna anavyokwenda. Lazima tukubali tunapoboresha hizi bandari leo tunataka ku-*archive* nini? Kazi ya mtu wa *TPA* ni nini? Kazi ya mtu wa Mapato ni ipi? Ni lazima tukubaliane haya mambo yaende kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimependa sana nizungumze juu ya habari ya Mifuko yetu hii ya Hifadhi ya Jamii. Nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wakurugenzi waliopata nafasi hizi, Mkurugenzi wa *PSSSF,* Ndugu yangu Kashimba na Ndugu yangu Erio wa *NSSF*. Tunaamini baada ya migogoro mingi na wanafanya kazi kubwa sana, huu ni wakati wao sasa wa kuhakikisha ule umuhimu wa Serikali kuyaunganisha unaonekana kwa kutoa huduma bora. Kwa uwezo na sifa zao na kuwa kwenye sekta hii kwa muda mrefu sina shaka watafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mwisho, Limezungumzwa humu, na mimi naomba hili niliseme kwa masikitiko makubwa sana. Wizara hii jukumu lake na Wizara kupitia sekta hii ya Mambo ya Ndani kupitia sekta ya Uhamiaji, kuna mdau mmoja amekuwa anasemwa sana humu ndani na kila akitaka kusemwa sisi tunaguswa. Bahati nzuri Mheshimiwa kila akitaka kuongea anasema najua wako watu humu wataumia.

Mimi ni mmoja watu wanaoumia, naomba nikiri hivyo. Kwa sababu mtu huyu ni mwekezaji, haijalishi ameishi hapa miaka mingapi. Kutaka kupata leo uraia siyo jukumu la Wizara kusema apewe au asipewe. Jukumu la Wizara ni kuhakikisha haki na utaratibu na sheria zimefuatwa. Leo mtu akitaka kuomba uraia kutumia utaratibu anaambiwa amehonga pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nilitegemea sana Mheshimiwa Waziri aombe hapa kama kuna ushahidi unatumika kama huyu mtu ni mhalifu kwanini asishughulikiwe?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Ahsante sana Mheshimiwa Mabula. Mheshimiwa Mabula, muda wetu ndiyo huo.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Augustino Masele.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kukupongeza kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hotuba nzuri ya Waziri wetu Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Hotuba yake inaweka msingi wa bajeti ya Serikali itakayojadiliwa hapa Bungeni kwa kipindi cha miezi mitatu kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea mbele, naomba niunge mkono hoja hotuba ya Waziri wetu Mkuu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu wetu alifanya ziara katika Mkoa wetu wa Geita na alifika pia katika Wilaya yetu ya Mbogwe akikagua miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo imetekelezwa na Serikali yetu ya Awamu ya Tano. Niseme tu kwamba Serikali yetu ya Awamu ya Tano imejipambanua kuwa ni Serikali ya viwanda; na pia inaendena na kauli mbiu ya Chama chetu cha Mapinduzi inayosema ya kwamba, "Tanzania mpya na CCM mpya na CCM mpya ni Tanzania mpya." Kwa sababu mambo mengi ambayo yanatendwa na Serikali hii yanatia moyo na yanaonyesha kwamba kweli tunakokwenda ni Tanzania mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miradi mbalimbali ambayo inatekelezwa na Serikali yetu ya Awamu ya Tano, zipo sekta mbalimbali muhimu ambazo Serikali yetu imezitilia mkazo ikiwemo sekta ya elimu. Sekta ya Elimu ni sekta nyeti na Serikali yetu imeweka msimamo mzuri wa kuweka elimu bila malipo kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne. Hongera sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika Sekta ya Afya, sisi sote ni mashahidi ya kwamba Serikali yetu imejenga Vituo vya Afya vingi katika sehemu mbalimbali za nchi hii ikiwemo katika Wilaya yangu ya Mbogwe. Tumepewa vituo vya Afya viwili; Kituo cha Afya cha Iboya na Kituo cha Afya cha Masumbwe. Vituo hivi vyote kwa pamoja vimepewa jumla ya shilingi milioni 800 na kwa kweli utekelezaji wake kwa kutumia ile *force account,* tumeweza kuyaona manufaa ambayo yamepatikana baada ya kuwa tumepata majengo mazuri. Ukifika kwenye Kituo cha Afya utajua kabisa kwamba kwa kweli mgonjwa akifika hapo hata kama alikuwa na hali mbaya anarejeshewa matumaini ya kuishi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kututengea awamu hi shilingi milioni 500 za kuanza ujenzi wa hospitali yetu ya Wilaya ya Mbogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yanaendelea kufanyika katika Wilaya yetu ya Mbogwe ikiwemo ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri yetu. Tuipongeze kabisa Serikali kwa sababu hatua za ujenzi zinaendela vizuri, miradi mbalimbali ya maji pia inaendelea kufanyika. Upo upanuzi wa mradi wa maji wa Nyakafuru, upo mradi wa Mbogwe, upo mradi wa Uhala katika Kata ya Lugunga. Yote haya wana Mbogwe tunasema ahsante sana kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala zima la ujenzi wa reli ya *standard gauge*. Ujenzi huu ni hatua ya maendeleo ya hali ya juu sana. Nchi yeu tumeshuhudia Serikali ikitekeleza mradi huu kuanzia Dodoma mpaka kule Dar es Salaam, ujenzi unaendelea vizuri. Tunayo matumaini makubwa kwamba ujenzi huu utaendelea mpaka kufika Kigoma na Mwanza na hata ile reli ya kutoka Isaka kwenda Kigali tunaamini Serikali yetu kwa kushirikiana na wenzetu wa Rwanda tutaishuhudia ikitekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi mapana ya kulinda muda, niipongeze sana Serikali kwa ujasiri wake

mkubwa wa kuanza na kuendelea kujenga mradi wa uzalishaji umeme wa maji katika mto Rufiji maarufu kama *Stiegler's gauge.* Sisi sote ni mashahidi ya kwamba hapa zitapatikana *Megawatts* 2100 ambazo aitaingizwa katika gridi ya Taifa. Ninaamini ya kwamba, Tanzania ya viwanda bila ya umeme isingewezekana lakini kwa kufuatana na juhudi mahususi za Serikali jambo hili limetiliwa mkazo na ninaamini ya kwamba itakapofika mwaka 2020 tutakuwa na uwezo mkubwa wa kuweza kui-*supply* Tanzania umeme vijiji vyote na vitongoji vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi wote Waheshimiwa Wabunge mtakuwa ni mashahidi wa namna ambavyo Wakandarasi mbalimbali wameendelea kutekeleza miradi ya usambazaji wa umeme vijijini kupitia Wakala wa Umeme Vijijini *(REA).* Jambo hili linafanyika katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika Wilaya yangu ya Mbogwe. Naiomba tu Wizara ya Nishati iendelee kumsukuma Mkandarasi ili aweze kumaliza mradi huu wa awamu ya tatu ya *REA* ili kwamba Watanzania wengi wa Mbogwe waweze kupata huduma hii muhimu ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika sekta ya barabara. Serikali yetu ya Awamu ya Tano pamoja na Awamu ya Nne wagombea wake waliwahi kuahidi ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika Mji wangu wa Masumbwe, tuliahidiwa kupatiwa lami kilometa tatu. Kwa maana hiyo, naishaurri tu Serikali katika bajeti yake ya mwaka huu ikumbuke kuzitimiza hizi ahadi za viongozi wetu wakuu wa Serikali katika maeneo mbalimbali ambako tunaamini ahadi hizi ziliwekwa na nitilie tu mkazo ujenzi wa barabara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Masele kwa mchango wako.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomnba kuunga hoja mkono kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nami nafasi ya kuweza kuchangia hii hotuba ya Makadirio ya Bajeti kwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kabla sijaanza ili nisije nikasahau, naomba kwanza kuunga mkono hoja ya makadirio katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali kwa miradi mbalimbali ambayo imekuwa ikiendelea hapa nchini. Miradi mingi kwa kweli ambayo hatukutegemea miaka ya nyuma, sasa inakwenda vizuri. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la kilimo. Tunaposema uchumi wa viwanda Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia ni kutilia kwanza mkazo kwenye suala la kilimo. Bila kilimo kwa kweli hata hayo meendeleo ya uchumi wa viwanda itakuwa ni ndoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Waheshimiwa Mawaziri katika sekta hii, lakini kilimo kina changamoto zake. Kwa mfano, ukiangalia sasa hivi kuna miradi hii ambayo iko chini ya Wizara, miradi kama ya *greenhouse* au vitalu nyumba. Tumefanya ziara tumeona baadhi ya hii miradi. Kwa kweli katika kilimo Wizara hii niwapongeze sana Waheshimiwa Waziri, wanafanya vizuri sana. Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Angellah Kairuki pamoja na Naibu Mawaziri wenu, Mheshimiwa Ikupa na Mheshimiwa Mavunde, tumeona hiyo miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli miradi hii inakwenda vizuri na hasa ajira kwa vijana. Vijana wengi sana

wameajiriwa katika miradi hii ya vitalu nyumba na wanafanya vizuri katika kujiingizia kipato. Tatizo linalojitokeza ni kwamba hii miradi hasa ya vitalu nyumba bado ni ghali. Mathalan, kama unataka upate kitalu nyumba cha mita 30 kwa nane unahitajika uwe na shilingi milioni 12 mpaka 15 kitalu nyumba kimoja. Sasa kwa mtu wa kawaida kuwa na uwezo huo ni vigumu. Naiomba Wizara katika eneo hili ione uwezekano wa kupunguza hi gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vingi kwa jinsi tulivyokuwa tunahoji vinatoka Kenya, vichache ndiyo vinatoka hapa Tanzania na hasa zile wavu zake kwa ajili ya kuezekea vitalu nyumba vinatoka nje kwa mujibu wa maelezo ya wataalam. Sasa naiomba Wizara, kama inawezekana, kukawepo na uwezekano wa kuweza kupata hizi malighafi hapa hapa Tanzania ili kila mmoja aweze kumudu kununua au kutengenezewa hivi vitalu nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta hiyo hiyo ya Kilimo naomba nisome eneo dogo kwenye ukurasa wa 27 kwenye kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Linasema: "upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2018/2019 umeendelea kuimarika kutokana na hali nzuri ya mvua katika maeneo mengi ya nchi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashaka yangu hapa, *data* hizi sijui zimetoka wapi? Kwa hawa wataalam wetu, tumetembea kidogo Kamati ambayo mimi nipo ya Katiba na Sheria, maeneo mengi bado hali ya chakula siyo nzuri. Maeneo mengi ambayo tumetembea, mazao mengi yamekufa, hata hapa tu jirani Gairo mahindi mengi ukiangalia na mazao mengi yalifika maeneo yanataka kubeba, lakini sasa yanakufa na maeneo mengi. Sasa hii hali nzuri, sijui, labda kuna Mikoa ambayo mimi sijatembea inawezekana kuna hali nzuri ya mvua. Ila mimi sijaona sehemu nilizotembelea au tulizotembea nikaona kuna ongezeko au kuna mvua ambazo ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la ulinzi kwa wanawake na watoto ambapo katika kitabu hiki

ni ukurasa wa 59. Kuna changamoto kubwa hapa. Juzi juzi tulikuwa Mkoa wa Mara, tuliufanya ziara ya kukagua miradi ya Makahama. Tulipomtembelea Mkuu wa Mkoa, Ndugu Malima alitupa *report* moja ambayo siyo nzuri kabisa kuhusiana na usalama wa wanawake na watoto. Kuna ongezeko kubwa sana la udhalilishwaji wa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, pale Mara, tulikuta kesi ambayo kuna mtoto wa miaka kama minne alibakwa lakini siyo kubakwa tu, akaambukizwa na UKIMWI baada ya kwenda kupimwa. Mama wa mtoto yule baada ya kuona kesi haiko vizuri, akapewa shilingi milioni mbili akawa anakwenda kuomba kwamba kesi isiendelee kwa sababu mtoto wake tayari ameshaharibiwa na hakuna kitakachoweza kubadilika. Hii inaonyesha kabisa kwamba bado wananchi wengi na hasa akina mama hawajapata elimu ya kutosha kuona namna gani wanapaswa kulinda watoto wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhalilishaji huo upo wa watoto lakini hatua zinachukuliwa. Sheria zetu bahati nzuri na wewe ni Mwanasheria; Sheria ya ubakaji haijakaa vizuri. Hii sheria kuna umuhimu wa kuipitia upya, kwa sababu ili idhihirike kwamba mtu alibaka, zile *elements* za kuhakikisha mtu atiwe hatiani kwa kubaka ni ndefu na siyo rahisi kuithibitisha. Nadhani hii haijakaa vizuri, inatakiwa ifanyiwe marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa Mahakama. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria. Tumekagua miradi mingi ya Mahakama, lakini kuna sehemu nyingi sana ambazo bado zinahitaji kuwepo na Mahakama. Sehemu nyingi Mahakama wanapanga, zile ambazo kunakuwa na mashauri mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tulikwenda Mkoa wa Arusha tukaenda mpaka kule Longido. Kuna sehemu tulifika yale maeneo ya mpakani pale, bado wanakodi kwenye sehemu za watu. Ile katika utoaji haki

kunakuwa na tatizo kidogo, kwa sababu kama Hakimu au Mahakama zipo kwenye nyumba za watu, hata utaoji haki unakuwa hauko sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi hiyo ya Mahakama, kuna miradi mingi ambayo sasa inakamilika; na hili nimewahi kulizungumza. Shida inayokuja ni kwamba fedha zile za kuwalipa Wakandarasi sehemu nyingine bado hazijafika. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba Mahakama ambayo inasimamia haki pale itakapotokea kwamba pesa hazijapelekwa kwa wakati, Mahakama hiyo hiyo nayo itashitakiwa. Sasa hili jambo halijakaa sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye hifadhi ya jamii. Mifuko yetu mingi imekuwa ikifanya vizuri, lakini kuna changamoto. Baadhi ya mifuko hii kuna kadi kwa mfano za *NHIF* hospitali nyingine zinakataa kupokea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Keissy

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nipatre kuchangia dakika zangu hizi 10. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja kwanza kwa asilimia mia moja. Namshukuru Waziri Mkuu kwa jitihada anazofanya pamoja na Mawaziri wote. Kusema kweli Mawaziri wanapishana kwenye anga za Wilaya na anga za Majimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais, Wilaya yangu ina miaka 40 lakini ilikuwa haina Hospitali ya Wilaya ila mwaka huu imepata fedha za Hospitali ya Wilaya pamoja na Vituo vya Afya viwili. Tumelalamika miaka na miaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nataka kuchangia kwenye Tume ya Uchaguzi. Wengi wanazungumzia habari Tume ya Uchaguzi, mimi nazungumzia Tume ya Uchaguzi, ipitie upya Majimbo na Kata. Hatulingani Majimbo. Unakuta Mbunge mmoja ana Kata nne, Kata sita, Kata saba mwingine Kata 28 au 29, anapata mafuta yale yale ya Jimbo, pesa ile ile ya Jimbo, mwingine amekaa tu anazunguka na bajaji na pikipiki anamaliza Jimbo lake. Naomba Tume ya Uchaguzi kabla ya uchaguzi wa Serikali za Mita aipitie Kata upya, kabla ya Uchaguzi Mkuu apitie Majimbo upya. Kama Majimbo hayafai, fyekelea mbali. Nadhani tunaelewana hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia habari ya wakulima wa Rukwa. Wakulima wa Rukwa ni wakulima wa mahindi na mahindi yetu hayo ni zao la biashara. Mwaka 2018 wameteseka sana, leo hi nimepata habari *DRC Congo* mahindi gunia ni shilingi 100,000/= lakini kwetu mahindi ni shilingi 30,000/= vikwazo vimekuwa *too much.* Vikwazo vimezidi. Mahindi yanatakwenda Kenya vikwazo, yanataka kwenda *South Sudan*, vikwazo; yanataka kwenda wapi, vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wakulima wetu mahindi ni kama zao la biashara. Kwanza hamwasaidii mbolea, hamwasaidi kupalilia, hamwasaidii kuvuna, wakivuna mnawawekea vikwazo, kwa vipi? Mwaka huu ndugu zangu sehemu nyingi mnasikia mvua hakuna. Kufa kufaana. Tuache tuuze mahindi tunapotaka, kila mtu ajue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wanakalia kucheza bao, kucheza dhumna hawalimi shambani, wanaogopa kwenda kulima, walime wengine mwekewe vikwazo. Vikwazo mwaka huu hatuvitaki Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kila mtu ajue lake, tuuze mahindi tunavyotaka na ondoeni vikwazo kuuza mahindi popote tunapoweza. Nyie chukueni ushuru wenu, mambo yaishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri Ziwa Tanganyika. Tufanye biashara. Ziwa Tanganyika tumezungukwa na nchi

ambayo ni tajiri katika Afrika *DRC Congo. DRC Congo* hawana usafiri. Hivi tukitengeneza meli kubwa iwe inazunguka kutoka Kigoma iende Huvira, Kalemi, Moba, Zambia - Mpulungu, irudie huku kwetu, tutapata na pesa za kigeni. Tusijifungie kati. Congo kama Congo ni nchi tajiri. Tufunguke tufanye biashara *DRC Congo.* Huwezi kufanya biashara na masikini mwenzako, huwezi kuendelea, miaka yote utakuwa masikini. Tuelekeze nguvu zetu Congo. Congo kuna utajiri mkubwa! Tufanye biashara Congo. Tupeleke ujumbe mkubwa wa wafanyabiashara kule Congo watu wafanye biashara zao, tusifanye vikwazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji. Kila mara nazungumza kuhusu maji. Hakuna Waziri anayefanya kazi kwa wakati huu kama Mheshimiwa Profesa Mbarawa, amejitahidi sana kutembea kila sehemu. Naomba aongeze ukali, tunaibiwa sana kwenye miradi ya maji. Bwawa la Fili-Namanyere, nimezungumza kila mara hapa, hata ukienda lile bwawa halizidi shilingi milioni 300, Mkandarasi akapewa shilingi milioni 900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukifanya hesabu za haraka haraka, uchukue *grader* na *excavator* zifanye kazi kwa mwezi mmoja thamani yake ni shilingi milioni 78. Hakuweka *cement,* hajaweka nondo, kachimba tuta; tuta lenyewe mita 100. Kokoto zenyewe hakuweka chochote. Mawe *trip* 100. Nimepiga hesabu lile bwawa kwa hesabu zangu za haraka haraka iko hapa karatasi, haifiki shilingi milioni 110, yeye kachukua shilingi milioni 900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashauri, kuna mabwawa hapa nikikusomea hapa, ni Nchi nzima. Mabwawa yaliyopo katika nchi hii, karibuni yote yana ufisadi ndani yake. Namwomba Mheshimiwa Profesa Mbarawa aunde Tume Maalum afuatilie bwawa moja hadi moja atagundua wizi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anafoka. Siku anakwenda Mheshimiwa Rais ndio anakataa majengo, anakataa mabwawa, miradi ya maji anaikataa. Ndugu

zangu, naomba Mawaziri mumsaidie kabla Mheshimiwa Waziri hajaja muanze kuwatumbua watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakusomea idadi ya mabwawa hapa ya nchi nzima ambayo ukiyapitia yote yana ufisadi wa pesa. Yaani ni mengi, ukiyapitia utapata kujua hata kule kwako labda yapo hayo mabwawa. Ni mengi ajabu, yana ukakasi wa wizi, yana matatizo na kila kitu. Naomba Wizara ya Maji iyapitie kabla Mheshimiwa Rais hajaenda akapata matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mabwawa ya idadi ambayo yameshajengwa Habia, Itimila, Kawa, Nkasi, Matwiga, Chunya, Mwanjoro kule Mkinga, Kilungadunga - Mkinga, Donda - Mkinga, Loliondo, Mafutela, Selewa -Kilindini na mabwawa kadhaa wa kadhaa. Ni hatari. Tunakusanya kodi kwa walala hoi lakini Wakandarasi wanakwenda kuchukua hela ambao siyo halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akija Rais katika Wilaya ya Nkansi, nitamwomba hata kwa dakika tatu akaangalie bwawa ambalo wanapiga kelele la Mfili akalione kama thamani yake kweli ni shilingi milioni 900. Tumesikia wanakwenda Mawaziri kwenye bwawa, tunamwambia asilipwe hela zake shilingi milioni 300 mpaka wataalam waje kilichunguza hili bwawa lakini walimlipa. Kaenda Mheshimiwa Waziri Kakunda kaenda kusema hili bwawa halifiki shilingi milioni 300. Tupo na *RAS* pale, tunazuia asilipwe Mkandarasi lakini analipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji Kirando walithamini shilingi bilioni 7.4 na *cheque* imeandikwa Mkandarasi apewe shilingi milioni 800 juu ya meza tukazuia. Wataalam wamekwenda ku-*check* ule mradi wa mamji utaona ajabu, wamegundua kwamba ni shilingi bilioni 4.6 na Mkandarasi wamempa kwa shilingi bilioni 4.6. Tumekoa shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Mweyekiti, sasa kama Namanyere ni mradi huu mmoja tu tumekuta tofauti ya shilingi bilioni tatu,

miradi mingine ilikuaje katika nchi hii? Mheshimiwa Waziri, msaidieini Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais kila akienda, hotuba zake za Mikoa ya kusini huko nimezifuatilia, zote zina mtatizo ya miradi miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ndege tu kupaka rangi. Wewe mwenyewe usingepaka rangi ndege. Walitaka kulipua shilingi milioni 300. Sasa kama mbele ya macho Jijini Dar es Salaam wanataka kulipua shilingi milioni 300, kule vijijini karibu na Zaire wanatulipua kiasi gani? Tunasema mpaka povu linatoka, lakini wanakaa maofisini wanaandika mikataba, Mawaziri wanasema hawawasikilizi. Mheshimiwa Prof. Mbarawa anasema mpaka povu linamtoka, Mdogo wangu Mheshimiwa Aweso amekuja kule amesema ufisadi umefanyika lakini hawachukuliwi hatua zozote, wamekaa wamestarehe, wanatuchezea akili tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu zangu, tuonyeshe mfano. Tusisubiri mpaka Mheshimiwa Rais anakwenda kwenye miradi ndiyo anawatumbua majipu. Mawaziri fanyeni hiyo kazi. Haiwezekani sisi Wabunge kwa sababu ni wanasiasa tunaropoka, lakini ndugu zangu hesabu haidanganyi. Bei ya bomba inajulikana, bei ya kutengeneza barabara inajulikana, bei ya kila kitu inajulikana, lakini unakuta mikataba tunajiumiza wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni tajiri. Leo tungekuwa tuna uwezo wa kuzikopesha nchi za Ulaya kama Ureno, kama Spain, tuna uwezo wa kuzikopesha, lakini sisi leo ndiyo tunakopa. Ni aibu. Tuna kila kitu katika nchi hii. Tuna utajiri wa ajabu katika nchi hii. Ni sisi wenyewe tunajitafuna. Ni mikataba mibovu ndiyo inatumaliza katika nchi hii. Lazima tuiangalie mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekuwa na mikataba halali leo nchi yetu ingekuwa na neema, ingeneemeka. Mheshimiwa Rais anafanya kazi mpaka anachoka, lakini wasaidizi ndugu zangu wamekaa maofisini, wanakula *AC* wanatuharibia nchi. Nimezungumza kila mara, mtu unamwona kabisa anaiba, muda wa mwezi mmoja ana

jumba la ghorofa; miezi miwili ana magari matatu. Mshahara wake unafahamika; anatoa wapi hizo hela? Halafu TAKUKURU wanasema wanamchunguza, wanamchunguza kitu gani? Ushahidi upo. Hawa ni kuwatandika tu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo tumefikia mwisho. Wachangiaji wote waliokuwa kwenye orodha ya leo wamepata bahati ya kuchangia. Kwa hiyo, niwashukuruni sana kwa michango yenu, ushauri mliotoa kwa Serikali, tutaendelea kesho.

Nina tangazo moja hapa kutoka kwa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo. Anapenda kuwatangazia Wabunge wote wanaotoka Wilaya zinazolima pamba kwamba kutakuwa na kikao juu ya zao la pamba wiki hii siku ya Ijumaa kuanzia saa 8.00 mchana katika Wizara ya Kilimo ambayo ni *opposite* na *VETA.* Kwa hiyo, mkaribishwa kwenye kikao hicho muhimu sana.

Sina tangazo lingine, kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho siku ya Jumanne tarehe 9 Aprili, 2019 saa 3.00 asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, kuagana ni kitu kizuri sana kwa Mabunge, upande huu narudia tena. *(Kicheko)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) aliinama ikiwa ni ishara ya kuwaaga Wabunge*

*(Saa 1.47 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 9 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*